Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Tatu – Tarehe 29 Januari, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## KIAPO CHA UAMINIFU

Mjumbe afuataye hapa chini aliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika nafasi yake ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja.

Mheshimiwa Spika, sote Watanzania tunakemea vikali sana mauaji ya ndugu zetu wenye ugonjwa wa ngozi kwa jina la Albino. Tunakemea na tunalaani kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu tumeweka utaratibu wa mtuhumiwa yeyote anayevunja sheria apelekwe kwenye chombo cha sheria (mahakama); ni kwa sababu zipi Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ameapa kuilinda Katiba ya Nchi, akatoa kauli ya kusema kwamba anayemgundua aliyemuua Albino, basi naye achukue sheria mikononi mwake ya kumwua.

Kama kauli hiyo tuliyosoma kwenye magazeti ni sahihi, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alieleze Bunge hili ni sababu zipi zilimfanya atoe kauli hiyo ambayo ni kinyume cha Katiba ya Nchi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana rafiki yangu Hamad kwa kuanza na swali hili kubwa na muhimu sana. Pengine kabla sijatoa maelezo kidogo, kwanza nitumie nafasi hii kwanza kuwashukuru sana kwa sbabu kwenye ziara ile, tuliongozana na Mheshimiwa Mama Sitta, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Lakini vile vile nilikuwa na Mheshimiwa Kagasheki na katika nyakati tofauti tofauti, nilipata vile vile Wabunge, Mheshimiwa Mshashu na wengine. Lakini vile vile Mheshimiwa Mwanri nilikuwa naye. Kazi kubwa niliyoifanya kwanza ilikuwa ni kujaribu tu kuonyesha kwamba Serikali tumechukizwa sana na hali ya mauaji inayoendelea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipata nafasi ya kuzungumza na makundi mbalimbali na tulifanya mikutano ya hadhara. Katika mazungumzo yale nilipata fursa na kwa kweli walitoa ushirikiano mzuri sana, vyama vya upinzani nao walikuwemo, CCM ilikuwemo, tulikuwa na madhehebu ya dini karibu yote, viongozi mbali mbali, AZAKI za namna mbalimbali pamoja na za Walemavu wa Ngozi.

Kwa hiyo, kwa uhakika ilikuwa ni mikutano ambayo mimi ilinipa faraja kwa sababu ilinisaidia sana kuweza kupata picha kamili juu ya tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni moja kati ya nchi ambazo zimekuwa na heshima kwa muda mrefu. Lakini nataka niseme, katika jambo ambalo limetutia doa kubwa na kusononesha sana Watanzania wengi ni mauaji yanayoendelea hapa nchini hasa kwenye eneo la Vikongwe na Walemavu wa Ngozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mikoa kumi iliyobainika, tukapewa taarifa zake, vikongwe 2866 wameuwawa. Ni wastani wa vikongwe 573 kila mwaka kwa vipindi vya miaka mitano. Sasa jambo hili ni kubwa na wengi wameuawa kwa kukatwa mapanga, wengine wamepigwa nyundo vichwani na sababu yake kubwa ni ushirikina. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la Ma-Albino limeibuka mwaka 2006. Tulianza na idadi ndogo sana ya watu 6 waliuawa 2007 na ghafla 2008 idadi hiyo ikapanda mpaka 28. Kwa hiyo tukawa na watu waliouwawa Walemavu wa Ngozi karibu 34. Nikiwa kwenye ziara hiyo, watatu wakauwawa.

Acha sasa wale ambao kwa namna moja au nyingine wameponea bahati, hawakuweza kuuawa na mfano mzuri alikuwa ni yule mtoto mdogo wa miaka miwili niliyemkuta Tabora kutoka Urambo.

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo niliyoyafanya, wale Watanzania waliokuwa wamehusishwa kwa namna moja au nyingine au waliona mauaji yakitokea, si mauaji ambayo tunaweza tukasema ni mauaji mazuri, hata kidogo. Hawa wauaji wanachotafuta ni viungo. Akipata bahati ya mkono, anaondoka na mkono, anaacha

unamwaga damu mpaka unakufa. Ile kesi ya Sengerema mliyoisikia juzi tarehe 22, muuaji yule alichofanya ni kukata mguu wa kulia, akaondoka nao, akamwacha yule baba anatokwa damu mpaka akafa. Na wale mliopata nafasi ya kuona kwenye luninga, watu wamekatwa viungo vyao vya mikono, wakakimbia navyo, potelea mbali kitakachotokea kwa hawa marehemu. Kwa hiyo, ilikuwa ni katika mazingira haya ambapo niliamua kufanya ziara katika mikoa ile. Walemavu walinisaidia sana, lakini pia vyombo vingine vilinisaidia vile vile.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa niliyoifanya ni moja tu; kwanza, kuhimiza vyombo vya dola kuwa makini na kusimamia jambo hili. Pili, nikaomba sana mikoa ile waendeleze elimu kwa nguvu sana kwa sababu moja ya eneo kubwa lenye udhaifu ni elimu ndogo katika maeneo yale. Nikahimiza sana ujenzi wa vituo vya afya kwa sababu najua pengine uhaba wa madaktari au upungufu wa huduma hiyo unaweza ukawa unachangia kwa kiasi kikubwa.

Nikaomba madhehebu ya dini watusaidie sana kujaribu kukemea jambo hili na nikawasihi wote waungane pamoja katika kupambana na mauaji haya yasiyokuwa na uhalali hata kidogo. Nikaviomba vyama vya siasa vyote kwa ujumla wake kwamba tuungane katika jambo hili kwa sababu linatugusa Watanzania wote. Nashukuru karibuni wote waliojitokeza walisimama kidete kabisa kuonyesha kwamba tutapambana na jambo hili mpaka siku ya mwisho.

Niliwasihi sana wananchi kwa ujumla wake kwamba tushirikiane na Serikali na vyombo vya dola, na makubwa niliyoyahimiza ni utoaji wa taarifa kwa vyombo vinavyohusika ili viweze kufanya kazi yake vizuri. Nikawaambia rejesheni sungusungu kwa sababu sungusungu pamoja na maovu yaliyoonekana kwamba ni mabaya, lakini bado kilikuwa ni chombo ambacho katika jamii kinaweza kusaidia sana.

Nikaomba Polisi washirikiane sana na chombo hiki wakisaidie kukiwekea utaratibu mzuri. Lakini niliamini kwa sababu wanazungumza lugha moja, wanaishi na watu hawa, wanaweza kuwa ni chachu nzuri ya kutusaidia kupata taarifa za msingi na kutoka pale, basi taratibu nyingine ziweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye suala lenyewe ambalo Mheshimiwa Hamad ameniuliza.

Mheshimiwa Spika, pengine kwa mtu ambaye hujapata nafasi ya kukutana ana kwa ana na watu hawa walemavu, wakati mwingine unaweza usione kile wanachokipata. Lakini, mimi nimekutana nao, nimewasikiliza, *it's painful*. Kwa hiyo, pamoja na juhudi nyingine zote nilizofanya…(mtaniwia radhi)…nilisema, wauaji hawa, hawawezi kuvumiliwa. Nikasema katika mazingira haya, nawaonya sana hawa wauaji, wahalifu hawa, wasidhani kama Taifa, kama Watanzania, tutaendelea kuwavumilia. Kwangu mimi nia yangu hasa ilikuwa ni kuwatahadharisha wajue kwamba tumefika mahali *we are fed up* na mauaji haya. Mimi niliamini kwa dhati tishio hili, lugha hii ya kuwatisha

itawaweka katika hali ya kuamini kwamba Serikali sasa imedhamiria jambo hili. Jamani, mauaji ya Ma-Albino si vizuri ukawasikia wanayoyaeleza, mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu Mheshimiwa Hamad, kama katika hili Watanzania wanaona Mheshimiwa Pinda lile ulilolifanya ni ovu kuliko yale maovu, vema! Lakini nia yangu ilikuwa ni nzuri sana, ilikuwa ni nzuri sana! Kwa hiyo, nataka mjaribu kunielewa na naomba Watanzania wanielewe, nia hasa haikuwa hiyo ambayo vyombo vingi vimeng'ang'ania kujaribu kulisema, wakaacha mambo mengine mazuri ambayo nimeyahimiza katika kupambana na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mwenyezi Mungu anisamehe sana kama nimewakosea, lakini nia yangu ilikuwa ni nzuri sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika zile *feelings* za ndugu zetu Albino wanaouliwa kinyama kabisa, na hata si ajabu kusema kwamba hawa wenzetu wanaofanya haya wamekiuka kile kiwango cha ubinadamu, maana Simba na Simba hawauani. Lakini inapofika binadamu anamwua binadamu mwenzake, yaani huyu binadamu ameondoka katika maumbile ya kibinadamu. Hizo *sentiments* sisi tuna-*share* naye sana.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aelewe kwamba kama alivyosema mwenyewe kwamba kuna vikongwe wengi sana wanauawa, kuna hawa Albino wanauwawa kwa wingi sana na vibaya zaidi kuliko wengine, kuna wizi wa mifugo nao unasababisha mauaji mengi sana. Lakini nchi yetu imeweka utaratibu wa sheria na Katiba.

Pamoja na kuelewa yote hayo na pamoja na *sentiments* ambazo amezionyesha hapa, lakini la pili ambalo ni la muhimu sana ni kwamba sisi tumeweka utaratibu wa vyombo vya dola kushughulikia haya, inawezekana kuna udhaifu mkubwa katika vyombo vyetu vya dola, sasa isitupelekee mahali kwa sababu kuna udhaifu wa dola, ndio unasababisha kukiuka misingi yetu ya Katiba na sheria.

Sasa mimi moja ambalo ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza tuna-*share* nasema kabisa kabisa na Watanzania wote na tunalaani vikali hicho kitendo cha mauaji, lakini vile vile ni vizuri tukaendelea kuheshimu misingi yetu ya Katiba na sheria, tukaimarisha taasisi zetu ili zipambane na hali hii…

**SPIKA:** Mheshimiwa, uliza swali tafadhali!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nauliza swali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliambie Bunge hili pamoja na hayo yote aliyosema ni juhudi gani madhubuti za kisheria ambazo vyombo vya dola vitafanya kuweza kuondoa tatizo hili ikiwa ni pamoja na ushauri tulioutoa kwamba hawa watoto wa Albino wapelekwe

kwenye madahalia ili wasaidie wazazi kuondokana na wasiwasi na watoto hao waweze kusoma. Kwa nini hatua hizo hazichukuliwi ili kupunguza hili tatizo? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri mimi ni Mwanasheria vilevile na ni mmoja kati ya watu ambao naamini sana katika hili analolisema Mheshimiwa Hamad, sana tu. Lakini nilichokuwa nasema tu ni kwamba kama Taifa tufike mahali kama anavyosema Mheshimiwa Hamad tudhamirie wote kwa dhati kabisa kufika mahali tuone kwamba jambo hili halifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiliniumiza sana mimi mara ya mwisho nilipoona Bunge la Jumuia ya Ulaya eti ndio linatoa azimio kujaribu kulaani mauaji ya Albino. Sikulipenda sana ingawa tulisema walifanya jambo jema. Sikulipenda tu kwa sababu walionekana kana kwamba wao wanaelewa vizuri zaidi juu ya tatizo hili kuliko sisi wenyewe Watanzania. Kwa hiyo, hapa tulipofika nikubaliane na Mheshimiwa Hamad, nafikiri kama Taifa basi tujikite katika kujaribu kupambana na jambo hili kikamilifu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hamad, ameuliza swali zuri sana na ilikuwa ndio jambo moja kubwa ambalo lilinifanya nijaribu kuzungumza na aaskari na watu wa usalama kwa nguvu kubwa sana. Mimi naamini kwa kauli zangu na viongozi hawa na namna tulivyokubaliana katika kujaribu kupambana na jambo hili, kutakuwepo na mabadiliko makubwa katika jambo hili.

Naomba viongozi wa vyombo hivi sasa watumie muda mwingi zaidi na mbinu nzuri zaidi za kujaribu kutumia hata rasilimali tulizonazo katika kujaribu kupata kukusanya taarifa katika maeneo haya ili tuweze kuwabaini wale wote wanaohusika na jambo hili. Sasa, ni kweli askari ni wachache lakini naamini wakidhamiria kwa taaluma zao, tunao uwezo wa kuweza kudhibiti wimbi hili la kikatili sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi na mimi niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Swali langu Mheshimiwa Spika lina vipengele viwili:-

Kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 9 kifungu kidogo cha (i) na (j) na ibara ya 27 kifungu kidogo (2), vifungu hivi vinaeleza kwamba Serikali itahakikisha kwamba utajiri wa nchi unatumiwa na watu wote na shughuli za uchumi hazinufaishi watu wachache na Serikali itasimamia uchumi wa nchi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vinavyokuja.

Swali la kwanza: Je, Serikali ina maelezo gani yanayoweza kuthibitisha vinginevyo kwamba vurugu zinazotokea sasa nchini, maandamano ya mara kwa mara chanzo chake si wananchi bali ni dalili za kushuka kwa utawala bora na kiini chake ni Serikali kuchelewa kuchukua maamuzi au Serikali kuchelewa kuchukua hatua dhidi ya ufisadi unaolitafuna taifa hili na ambao umelishushia heshima taifa letu? *(Makofi)*

Swali la pili: Kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 28 kifungu kidogo cha 4 kinasema Uhaini ndio kosa la juu kabisa katika nchi yetu; na kwa kuwa lengo la uhaini ni kuiangusha Serikali iliyochaguliwa kihalali; na kwa kuwa ufisadi unaweza ukayumbisha nchi na hata kuiangusha. Je, Waziri Mkuu atakubaliana na mimi kwamba upo umuhimu sasa wa kuiangalia Katiba yetu na kuifanyia marekebisho ili iweze kukabiliana na ufisadi mkubwa ambao umelishushia Taifa hili heshima kama vile mauaji ya Albino yalivyoshushia Taifa hili heshima. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kumjibu Mheshimiwa Mpendazoe swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni letu wote na mimi bado naamini Watanzania tunao uwezo wa kupambana na ufisadi kwa sura zozote zile. Unachokiona hapa ni mmomonyoko wa maadili hasa katika utumishi wa umma ndio jambo kubwa linalopelekea kutufikisha hapa.

Kwa hiyo, bado naamini ni vizuri tukawa na sheria kali za kupambana na uhalifu wa aina hii ya ufisadi na vyombo vyetu vya sheria vitekeleze majukumu yake inayotakiwa. Sasa, rai yako ni nzuri vile vile na Bunge hili ndio wenye mamlaka yote hayo. Kama leo mnataka kupitisha sheria ambayo inafanya kosa la ufisadi, ufisadi kwa maana ya rushwa, au ufisadi kwa maana ya wizi wa fedha za umma kwamba ni uhaini na uhaini adhabu yake ni kifo, vema, tunaweza tu, tunaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, akini nadhani itabidi basi tujikite katika mjadala wa kina zaidi tuweze kutoa ainisho ambalo litawezesha kutupa kile tunachokitaka. Rushwa kwa mapana yake ipo kila mahali na kama kila mahali itakuwa ndio *definition* ya ufisadi, mnaweza mkakuta tunarudi tena nyuma tukaanza kuulizana maswali mengi.

Lakini bado uamuzi uko kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kweli sisi kama Serikali tukipata mawazo ya msingi na tukalitafakari wote kwa pamoja, ni jambo kubwa na pengine tutalazimika kuchukua kura kidogo za maoni tuone Watanzania wote wanasemaje baada ya kujaribu kuainisha kosa la ufisadi tunalotaka liwe la uhaini, nafikiri linawezekana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja. Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili tumejadili mara nyingi matatizo yanayotokana na maandalizi na mchakato mzima wa Vitambulisho vya Taifa. Suala hili limechukua sasa zaidi ya miaka 10 na hapa katikati Taifa letu kupitia tenda zisizo sahihi limepoteza fedha nyingi na hatimaye tumepata mchakato ambao ulikuwa unaendelea. Hivi sasa, taarifa tuliyonayo ni kwamba mchakato huo nao sasa umeanza kuingia dosari, na umeingia dosari baada ya kamati inayohusika - *Evaluation Committee* pamoja na *Tender Board* kukamilisha mambo yake.

Mheshimiwa Waziri katika wizara inayohusika ameingilia *process* hiyo, na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 19 Desemba, 2008 umeandikiwa barua. *Reference* Namba ninayo na kila kitu naweza nikakupatia. Baada ya barua hiyo sijaona hatua iliyochukuliwa ikiwa dhahiri kabisa Mheshimiwa Waziri huyo amekiuka taratibu zote za *Public Procurement Act* pamoja na kanuni zake zote. Mambo haya yanaashiria dalili nyingi ikiwemo suala la rushwa inaweza kuwepo hasa la kutetea kampuni moja katika makampuni yote. Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza kuliambia nini Bunge hili ili Taifa hili lisiendelee tena kupoteza fedha nyingi za wananchi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya tu kwamba Mheshimiwa Dr. Slaa kawahi tu jambo hili, umetangulia mno. Nalisema hili kwa sababu mchakato haujafikia mwisho. Ungekuwa umefika mwisho na ukakuta kile ambacho wataalam walikuwa wamependekeza kimegeuzwa, kwa lugha hiyo unayoisema, ungekuwa na *point* moja nzuri sana.

Lakini mimi nasema hawajafika mwisho, kwa hiyo umetanguliza tu mawazo. Nami nataka niseme ni kweli unalolisema, kwa sababu kwenye jalada la Mambo ya Ndani pale *Confidential Folio 47* imenyofolewa na ndio imepelekea hili jambo kuzagaa. Sasa ni uvujaji wa siri lakini mimi hilo si *concern* yangu kwa sasa. (Makofi)

Ninachosema tu ni kwamba hili jambo mngengoja lifike mwisho ili tuwe na hoja ya msingi. Huyu ni Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Ndani, kama pengine ameona kuna jambo limejitokeza au kuna malalamiko yamejitokeza angeweza au anaweza kabisa kusema jambo hili ninyi mmelisikia, mmelipatapata au hata kuandika kabisa kuonyesha kwamba, hebu nipeni maelezo juu ya jambo fulani, kwa msisitizo mkubwa.

Lakini *so long as* mchakato haujafika mwisho, mimi nasema tusubiri ufike mwisho halafu ndio tutamhukumu vizuri sana huyo Waziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tafadhali kaa chini! Nadhani kipindi hiki tukikitumia kama ni malumbano na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutakuwa tunakwenda nje kabisa ya kanuni. Naona sasa kila anayeuliza anakuwa amejiandaa kubisha bila sababu za msingi.

Ukishapata fact si lazima umchokonoe Waziri Mkuu mpaka aende kukubaliana na wewe. Hapa sio majadiliano na Waziri Mkuu ni maswali kwa Waziri Mkuu, akishajibu amekupa *fact*.

Labda sasa unaposimama uulize linalohusu *fact*, sio useme unavyodhani wewe ndio sawa au utaratibu uliomo Serikalini haufai, hayo ni mambo mengine kabisa. Kwa hiyo, kwa tahadhari hiyo sasa, hebu tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Na mimi nadhani nakwenda kwenye *facts*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema kwamba tungelisubiri mpaka mchakato ukamilike. Sasa kuna mambo mawili hapa yametokea. Kwanza, Sheria ya Manunuzi iliyopitishwa na Bunge hili imeeleza kabisa kwamba kama kuna taratibu zozote zinazolalamikiwa, basi kuna ngazi za *appeal*, Waziri amevunja ile kanuni.

Bunge hili haliwezi kuvumilia kuona Waziri wake anavunja. Taarifa inapofika kwa Bunge ni lazima tuwe wakali kwa sababu sheria ile vinginevyo haina maana, tuiweke kwenye kabati. Je, Waziri Mkuu anatuambia nini sasa kwamba taratibu…

**SPIKA**: Mheshimiwa Dr. Slaa naomba nikusitishe hapo hapo. Hayo unayoyaongea ni wewe tu unayajua, kwa kawaida ndiyo maana kuna ku-*table* vitu hapa. Kwa hiyo, kama kweli wewe unaamini hilo unalolisema, upo utaratibu chini ya kanuni, jiandae yalete hapa na wote tuwe na *facts* tuzungumze.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ili tuendelee mbele naomba niwasomee Kanuni yetu ya Pili fasili ya (2); iwapo jambo au shughuli yeyote haijakuwekewa masharti katika kanuni hizi. Spika ataamua utaratibu wa kufuata katika jambo au shughuli hiyo kwa kuzingatia Katiba au Sheria zingine za nchi na Kanuni zingine zilizopo na kadhalika. Leo hii swali la Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na majibu kwa pamoja vimechukua dakika 20 kati ya dakika 30 za maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kutokana na hilo na kwa mamlaka mliyonipa chini ya Kanuni hii namba mbili fasili ya pili, naongeza muda wa dakika kumi na tano ili tuweze kupata maswali mengine. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa hakuna nchi yeyote duniani iliyoendelea kwa kutowekeza katika elimu hususan elimu ya juu, na kwa kuwa, Baba wa Taifa alihakikisha kwamba vijana wanasoma mpaka Vyuo vya Elimu ya Juu bure, lakini vilevile Rais wa awamu ya Nne Mheshimiwa Jakaya Kikwete wakati akihutubia wanafunzi alisema kwamba hakuna mwanafunzi wa Kitanzania atakayeshindwa kusoma kutokana na umasikini wake au wa Wazazi wake. Lakini zoezi linaloendelea sasa hivi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam la kudahili upya wanafunzi kigezo kikubwa kinachoangaliwa ni pamoja na ulipaji wa ada kutokana na daraja alilopangiwa na Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kutokana na hali hiyo kuna baadhi ya wanafunzi mpaka sasa hivi bado hawajaweza kudahiliwa kwa sababu wamekosa fedha.

Je, huoni kuwa zoezi hili linakingana na misingi aliyoweka Baba wa Taifa ya kutobagua wanafunzi kutokana na umaskini wao, na vilevile linapingana na tamko la Rais?(Makofi)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa tulikuwa tumetarajia kuwa wanafunzi 20,300 wangekuwa wamedahiliwa katika utaratibu huu tuliokuwa tumejiwekea, wanafunzi 17,200 tayari wamekwishadahiliwa na wapo vyuoni, wanafunzi 2,500 wao hawakuomba kurudi kabisa, wanafunzi 600 ni wale ambao fomu zao zimeonekana bado zina utata zikishakuwa *clarified* watakwenda chuoni, ninachosema ni kwamba kama wanafunzi 2,500 unaowazungumza ndiyo hao ambao unasema tunawanyima fursa ya kurejea vyuoni, mimi nasema hatujawanyima, aje chuoni, ajaze fomu tuitazame kama ametimiza masharti yaliyowekwa na uongozi wa Chuo Kikuu hakuna tatizo, atachukuliwa tu kama walivyochukuliwa wanafunzi wengine 17,200.

**MHE. SUSAN ANSELM. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika nakushukuru, nashukuru pia kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini nazungumzia pia hao wanafunzi 600 anaowazungumzia Waziri Mkuu ambao tayari wamekata rufaa.

Vilevile naomba niseme kwamba kuna sheria katika vyuo vyetu vya elimu ya juu kwamba mwanafunzi akikosa masomo kwa wiki tatu mfululizo maana yake amejifukuzisha chuo mwenyewe, sasa nilikuwa naomba kujua ni kwa nini hawa wanafunzi ambao tayari wamekata rufaa wasiruhusiwe kwenda shuleni sasa hivi ili waweze kuendelea na masomo ili baadaye wasije wakakumbwa na hiyo sheria ambayo inaweza ikawafukuzisha kama watakaa zaidi ya wiki tatu nyumbani.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi naamini katika mazingira yaliyopo hivi sasa, sidhani kama hilo Mheshimiwa Lyimo unalolisema litakuwa ndiyo kikwazo hata kidogo, hapa kikwazo ni wewe katika kushindwa kwako mpaka ukakata rufaa ni mambo gani umepelekea ukafika pale, hasa hilo ni jambo la kiutawala tu mimi nitakachoweza kumwambia sana Profesa Maghembe ni kusema rafiki yangu, kwa hawa 600 tusihangaike nao endelezeni na mchakato mpaka mfike mahali mjiridhishe na msiingize hiyo kanuni kwamba ndiyo kikwazo, utaratibu ule tumeuweka sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama litakuwa ni tatizo kubwa sana.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mara yangu ya kwanza;

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa sasa hivi nchi zote duniani zimeafiki kabisa mfumo wa utandawazi pamoja na nchi yetu ya Tanzania, lakini kwa utafiti ambao una uhakika kabisa umeonesha kwamba katika utandawazi nchi zilizoendeleza ndiyo zinazofaidika zaidi kuliko nchi maskini kama nchi yetu ya Tanzania.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba mfumo huu wa utandawazi hauathiri nchi yetu na kutupunguzia mapato yetu hasa mapato yetu kutoka kwenye madini, kutoka kwenye mbuga zetu za wanyama, na kadhalika?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, utandawazi ni dhana pana sina hakika sana kama nitakuwa mtalaamu wa jambo hili, najua ni jambo kubwa linahitaji wenyewe lakini labda nijaribu tu kusema kile ninachokijua kwa ufupi tu kwamba, utandawazi ni ile dhana ambayo inatupelekea tujumuike uchumi wetu wa kitaifa na uchumi wa kimataifa

kibiashara mnaweza mkakuta ni masuala ya uwezekaji, suala la mitaji kuingizwa hapa nchini, suala la teknolojia kuingizwa nchini. Kwa hiyo, ni jambo moja ambalo halikwepeki sana; ni jambo limekuwepo lakini karne ya 21 ilichokiona zaidi ni hii teknolojia ya mawasiliano ya habari ndiyo imekuza sana hiyo dhana na mpaka sasa unaona inatusumbua.

Meshimiwa Spika, lakini ni lazima tukubali kwamba hawa ni watu wanakuja kuwekeza; ni watu wanakuja kuweka mitaji yao. Kwa hiyo kwa kweli jukumu hasa la kulinda maslahi ya Nchi ni letu sisi Watanzania. Kwa hiyo, ni lazima tujipange vizuri tuone wanapokuja na mikataba yao. Je, tuna uelewa wa kutosha na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kujibu swali lako niseme tu kwamba tulichobaini sisi katika kipindi kifupi nilichokaa humo kama kiongozi wa shughuli hapa Bungeni, nimeona kwamba ni kweli tunahitaji kujipanga vizuri kwenye suala la mikataba. Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba Wizara hii ya Sheria na hasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni lazima tuiimarishe na tuiboreshe.

Mheshimiwa Spika, ni lazima vilevile tufike mahali katika maeneo ambayo hatuna uwezo nayo tukubali kutafuta watalaamu hata ikibidi kutoka nje kwa sababu ni jambo la msingi sana.

Lakini tumekubaliana vilevile katika hii kazi pengine hatuiwezi peke yetu, kwa hiyo tumeiomba *UNDP* na bahati nzuri walipokuwa hivi karibuni Liberia, Tanzania ni moja kati ya nchi tano ambazo zimekubaliwa kuingizwa katika mfumo wa kusaidiwa katika kuboresha uwezo wa masuala ya mikataba ambayo inahusiana na uwekezaji ili tuweze kupanuka zaidi mawazo na tuweze kuona tutafanyaje.

Mheshimiwa Spika, kwa hili ndiyo maana unaona hata ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali sasa tumeifanyia marekebisho kidogo, ili yule Katibu Mkuu asiwe Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kibaki ni chombo huru na masuala ya utumishi na utawala yabaki peke yake, kwa hiyo mimi naamini chini ya mawazo haya yote tuliyoyapata tunaweza pengine polepole kubadili uwezo utakaokuwa unahitajika.

Mheshimiwa Spika, lakini tumekubaliana na *UNDP* na hata sisi wenyewe ndani kwamba haiwezekani ukaimarisha ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali peke yake ni lazima Wizara zile za kisekta nazo tuziingize katika utaratibu huo na ikibidi tuwe na timu ambayo tunaijua kwamba hii ndiyo timu ya majadiliano lakini yenye mchanganyiko wa watalaam na bila kujali kwamba yupo ndani ya Serikali au nje ya Serikali, kubwa ni Utanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutajitahidi kutumia yote haya ili kulinda maslahi na utandawazi usije ukatuathiri sana, nakushukuru sana.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba swali langu la leo niliahirishe nitauliza siku nyingine.

**SPIKA**: Sawa, Ahsante sana.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo kwa Waziri Mkuu;

Hivi karibuni Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alifanya ziara Visiwani Zanzibar pamoja na Pemba, katika ziara hiyo alihutubia mikutano ya hadhara ambayo ilihudhuriwa na watu wa itikadi mbalimbali, na katika mikutano hiyo alitoa kauli za kisiasa ambazo zililaaniwa si tu na Wapinzani kama alivyoita lakini wale wote ambao wanaitakia mema Zanzibar, kwa mfano; Rais alisema wapinzani wasitarajie kuunda Serikali kwa muda mrefu ujao na pengine wasipate nafasi hiyo kabisa.(*Makofi*)

Kauli ya pili, alisema Wapinzani ni wapinga mapinduzi na hivyo wasitarajie kupewa nafasi ya kuongoza Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na kauli hizi ni lini viongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wataacha kuhubiri siasa za chuki na mfarakano wa Zanzibar ambao tayari mnajua ni waathirika wa siasa za mfumo wa vyama vingi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, hakufikia mwisho akauliza swali. Lakini nadhani nimemwelewa alichokuwa anasema na sina hakika unataka niseme nini, Rais wangu kasema, Kiongozi wangu kasema, sasa sijui unataka niseme kwamba kakosea.(*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nitapata taabu kidogo kumsemea Rais katika jambo hili na mimi naogopa sana kwa sababu umetumia vyombo hivi vya habari kwa maana ya magazeti sina hakika kweli kama hayo ndivyo yalivyowekwa hivyo, na sielewi mazingira yalikuwaje, na kwa kweli sina hakika tafsiri aliyokuwa anajaribu kuitoa kwa umma wakati ule ilikuwa ni ipi na sisi tunaitafsiri vipi.

Kwa hiyo, sitaweza kukusaidia sana katika hili isipokuwa ninachosema tu ni kwamba Zanzibar ni yetu wote, kubwa tuendelee kushirikiana pale Visiwani kujenga Visiwa vyetu vya Zanzibar tunachohitaji ni maendeleo ya wananchi wetu. (*Makofi*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kutokana na kauli hizi za Mheshimiwa Rais, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuwaambia Watanzania na dunia kwamba hauutambui mfumo wa vyama vingi vya Siasa, kwa sababu msingi wa vyama vingi vya siasa ni kwamba wananchi waliowengi ndiyo wanaochagua Serikali ambayo itaingia madarakani, lakini kwa sababu hizi ambazo amezizungumza ni kwamba si wananchi ambao wamechagua.

Je Serikali iko tayari kutangaza suala hili kwa wananchi kwamba mfumo huu ni kiini macho tu na kwamba unawahadaa Watanzania bure? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hilo siyo swali na wala halihusiani na swali la msingi, swali la nyongeza kwa mujibu wa kanuni ni lazima lihusiane na swali la msingi, sasa kusema Serikali haitambui vyama vya siasa, halihusiani hata kidogo, inawezekana kauli ya Mheshimiwa Rais ikawa imewaudhi baadhi ya watu lakini ndiyo siasa hiyo, wale waliudhika waitishe mikutano ya hadhara wajibu ndiyo mambo yanavyokwenda na ndiyo siasa ya vyama vingi.(*Kicheko*)

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana, mimi ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lini viongozi Wakuu wa Taifa letu hili la Serikali wataacha kutumia vibaya fedha za walipa kodi kwa kufanya shughuli za kisiasa za Chama Tawala CCM , wakati wa ziara rasmi za Kiserikali ambazo zinalipwa na walipa kodi ambao wote ni wa vyama mbalimbali na itikadi mbalimbali na wasio na Vyama, Mfano ziara ya hivi karibuni ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete Zanzibar ambayo pamoja na mambo mengine amekuwa akitembelea matawi na ofisi za CCM na akiweka mawe ya msingi, akihutubia mikutano ya hadhara ya Chama Tawala, viwanja vya Gombani Pemba na viwanja vya Kibanda Maiti Unguja, Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa naona leo mna matatizo! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, hivi kweli katika nchi gani kuna utaratibu kama huo mnaouzungumza. Angepatikana Rais wa *CUF* angeacha kabisa kutembelea matawi kwa miaka mitano hii inawezekana?

Tusilete nadharia ambazo hazipo duniani popote. Rais wa Marekani anasafiri na *Air Force One*, anakwenda kuhudhuria mkutano wa *Democratic Party* na huko ndiko tunakoiga. Anakutana na Kamati za *Democrats* katika majimbo mbalimbali na kadhalika, na anatumia *Air Force One*. Sioni mimi mwanasiasa akajitenga na chama, kama tuna mifumo ya vyama vya siasa haiwezekani tunaowachagua wakaondokana kabisa na vyama wakajiahirisha uanachama wao kwa miaka mitano halafu wakarejea tena, na kwa nini unakwenda kwa Rais. Hata ukishuka huku chini, kuna Mawaziri, kuna Wabunge, ni lazima mtu aweze kutekeleza mambo ya chama chake ili kiendelee kutawala. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ninachosema vile vyama ambavyo bado havijashika hatamu ya utawala wasubiri, waendelee kufanya harakati, itafika wakati nao tutaona watakavyofanya haya mambo.(*Kicheko/Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Novemba mwaka jana 2008 Serikali ilipokea ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge hili ya Nishati na Madini juu ya kuitaka *TANESCO* ikatae kununua mitambo iliyokuwa chakavu kutoka kwa *DOWANS.* Baada ya kupokea ushauri huo Serikali ikawa imeishauri *TANESCO* na ikawa imezuia kununua mitambo hiyo. Lakini wakati huo huo kulikuwa kuna kesi ambayo imefunguliwa na *DOWANS* Ufaransa ambayo ilikuwa inadai fidia juu ya kukatishwa kwa mkataba, na katika kesi hiyo pia *TANESCO* baada ya kupata agizo la kuzuia mitambo hiyo isinunuliwe, nao

wakaamua kuizuia mitambo ya *DOWANS* isiondoshwe katika maeneo yake ili kwamba katika kesi ile iliyofunguliwa iwapo *TANESCO* itashinda basi iwe fidia katika kufidia kesi hiyo.

Kama kesi ina pande mbili kuna kushinda na kushindwa. Kama *TANESCO* itashinda kesi hiyo na ikaja ikaitwaa hii mitambo ambayo ni mitambo iliyokuwa chakavu ya *DOWANS* haioni kwamba itakuwa inakiuka tena ushauri wa Serikali iliyoshauri kwamba mitambo hiyo isinunuliwe kwa sababu ni chakavu.

Je, iwapo *DOWANS* watashinda hiyo kesi na tayari hiyo mitambo imeshazuiliwa na *TANESCO* haioni kwamba tutakuwa tunaiingizia hasara Serikali kwani kutakuwa na fidia ya kesi ya msingi na pia kutakuwa na fidia kuhusiana na ile mitambo iliyozuiliwa?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nalikataa swali hilo kwa misingi ya sheria na Kanuni. Hatuwezi kukaa hapa tukaanza kukisia Mahakama zitafanya nini. Huo siyo wajibu wetu hata kidogo, kwa sababu hapo itakuwa ni kuingilia kazi za mhimili mwingine maana yake yote tunayotamka hapa yanaweza yakaja kuwa na mwonekano wa kuelekeza mkondo wa sheria uende vipi na hiyo ni kinyume kabisa na sheria.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana mambo ya maswali kwako yamekwisha.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ile ile niliyoifanyia marekebisho. Kwa mujibu wa Kanuni ya (2) nalazimika tena kuongeza dakika kumi na tano ili kipindi cha maswali ya kawaida nacho kifikie muda wake unaostahili.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 30

### Kuhamishwa Wananchi wa Kata ya Kigamboni

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na taarifa kupitia vyombo vya habari za kuwahamisha baadhi ya wananchi wa Kata ya Kigamboni na Makazi ya watu kwenye eneo hilo lililoanzia Kivukoni hadi Mji Mwema ili kumpisha Mwekezaji ambaye anakusudia kuwekeza katika eneo hilo.

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya suala hilo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuwahamisha wananchi wa eneo la Kigamboni linaloanzia Kivukoni hadi Mji Mwema kwa lengo la kumpisha Mwekezaji. Aidha hakuna Mwekezaji yeyote ambaye hivi sasa tayari ameainishwa wala kupewa kibali cha kuendeleza eneo lolote la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kulipanga upya eneo la Kigamboni kusudi liendelezwe katika sura ya Mji wa kisasa ndani ya Jiji la Dar es Salaam. Dhamira hii inalenga kutumia fursa zilizopo katika eneo hilo ambazo ni kwamba eneo hilo liko kando kando ya Bahari, eneo hilo lina visiwa, eneo hilo ni jirani na eneo la katikati ya Jiji *(Central Business District*) na kasi ya ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam unaosababisha kuwepo na ongezeko la mahitaji mbalimbali ya katikati ya Mji sambamba na mabadiliko ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali imeainisha eneo la mpango lenye ukubwa wa heka 5,550(ekari 13,875)l itakalohusisha Kata nne za Kibada, Vijibweni, Mji Mwema na Kigamboni. Pia Serikali imetoa tamko la kusimamisha uendelezaji na ujenzi katika eneo hili.

Aidha Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya Mwaka 2007 inaelekeza kuwa eneo likitamkwa kupangwa upya kimipango miji ujenzi husimamishwa ili kutoa fursa ya kuandaa mpango ambao hautakinzana na maendelezo yanayotarajiwa kufanywa katika eneo la mpango.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishatoa tamko rasmi tarehe 30 Oktoba, 2008 ambalo lilizingatia tangazo la Serikali Na. 229 la tarehe 24 Oktoba, 2008 la kusudio la kupanga upya eneo hilo ili Kigamboni uwe Mji Mpya wa kisasa wenye huduma za kijamii za kisasa na majengo wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yangu tukishirikiana na Manispaa ya Temeke tumo katika mchakato wa uhamasishaji na utoaji elimu kwa Umma kuhusu maudhui ya mpango huu, umuhimu wake na manufaa yake kwa wana Kigamboni na kwa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango huu, wakaazi wa Kigamboni hawatahamishwa kwa maana ya kupelekwa maeneo nje ya Kigamboni, bali maslahi yao yatazingatiwa na watashirikishwa katika kila hatua kwani watakuwa ni sehemu ya mradi.

Wale ambao maeneo yao yatapitiwa na barabara au huduma za jamii, watalipwa fidia stahiki kwa bei ya soko na watapatiwa viwanja huko huko Kigamboni, ndani ya eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao maeneo yao yatapangiwa shughuli zingine kama mahoteli, maduka, maeneo ya makazi, mabenki, nakadhalika. Watapewa fidia kwa bei ya soko ambayo fidia hiyo inaweza kuwa fedha taslimu au kujengewa nyumba mbadala au kuingia ubia na mwekezaji atakayehitaji kuwekeza katika kiwanja husika kulingana na ramani (*Master Plan*).

Aidha, wanakigamboni wenye uwezo wa kuwekeza ndani ya eneo la Mradi watapewa fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi wa eneo la Kigamboni wawe na ujasiri wa kukubali mabadiliko haya kwani kupitia mpango huu watapata huduma nzuri na za kisasa za barabara, vivuko, umeme, maji, usafiri wa majini, Mji uliopangwa na kujengwa kisasa na pia ajira zitapatikana kwa wingi kupitia miradi ya ujenzi wa majengo marefu, ujenzi wa barabara, mahoteli na kadhalika.

Lengo kuu la mpango huu ni kuboresha mazingira ya Kigamboni na wakazi wake.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri kwa kuwa amekiri kwamba wananchi wa Kigamboni wasiwe na wasiwe na wasiwasi wowote kwamba wataondolewa katika maeneo yao ila kwa sababu ya miradi mingine ya maendeleo.

(a) Kwa kuwa, Kigamboni ilitokea kwamba Viongozi wa Wilaya ambao wamepeleka ushauri kwa wananchi, wamefanyiwa vurugu hadi kuhamishwa na Polisi au kufukuzwa maeneo yale, ushiriki wa wananchi hao ambao Waziri ameusema hapa watashirikishwa utakuwa ushiriki wa aina gani wakati tayari vurugu kule zimeshaanza?

(b) Serikali imekuwa na utaratibu wa kuhamisha watu katika maeneo yao ya asili na kuwapeleka sehemu zingine kitu ambacho kinawaathiri sana Watanzania; na Mheshimiwa Waziri amekiri hapa kwamba atatoa fidia au watajengewa nyumba wale ambao watahusika na zoezi hilo; na kwa kuwa Serikali imekuwa ina mpango huo mfano Kipawa, Airport wananchi wamezuiliwa kujenga nyumba zao, wamezuiliwa kufanya ukarabati zaidi ya miaka kumi na hawajapewa fidia katika eneo hili.

Je, Wananchi hawa wa Kigamboni nao watakuwa katika eneo hili kama wananchi ambao hawajatendewa haki kama wananchi wa Kipawa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Spika, kwanza lile la mwitikio wa wananchi katika suala hili anasema wataitikiaje wakati tayari kuna vurugu.

Mheshimiwa Spika, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba hakuna vurugu Kigamboni. Mimi nimeongea na yule Meya kuhusu lile tukio kwa sababu na mimi nimesoma kwenye magazeti. Meya alichosema alisema kwamba alikwenda pale kueleza mipango mbalimbali ilipofika agenda ya mpango wa Kigamboni kipaza sauti kikazimika kwa sababu umeme ulikatika. Alipokuwa anaendelea kusema akawa hasikiki. Kwa hiyo watu wakawa wanavutika na ile agenda. Watu sasa wakawa wanatoka kule kumsogelea kumzonga ndio sasa Polisi wakaona hapa itakuwa hatari wakamwondoa. Amenihakikishia hakukuwa na vurugu.

Mheshimiwa Spika, magazeti kwa sababu ya kutaka kuuza magazeti wakasema kwamba kulikuwa na vurugu. Hapakuwepo na vurugu ni kwa sababu nimesema kuna mchakato kwa sababu tumeshaanza kuelimisha wananchi, wanaelewa na hakutakuwa na vurugu yoyote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhamisha wananchi nimeshasema, kwamba mradi wa Kigamboni ni tofauti na miradi mingine. Huwa kuna miradi mingine ambayo wananchi huwa wanaondolewa katika eneo kupisha kitu fulani, kama pale Kurasini kwa sababu tunapanua bandari ni lazima wale watu wa Kurasini tuwaondoe kwa sababu tunapanua Bandari na kuwapeleka maeneo mengine na tumeshawapa maeneo tayari.

Kwa Kigamboni hatuwaondoi kwa maana ya kuwaondoa eneo la Kigamboni watabaki katika eneo la Kigamboni ila tu tunawapanga upya na kwa Kisasa. *(Makofi)*

Na. 31

**Juhudi za Kumaliza Mapigano ya Koo**

**MHE. CHARLES N. MWERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na mapigano baina ya koo na koo za Kikurya kama vile Warenchoka na Wanchari, Wanchari na Wakira, Wamera na Wahanyanga, mapigano yaliyodumu muda mrefu na kusababisha wananchi wengi kupoteza maisha yao na kujeruhiwa:-

Je, Serikali inafanya juhudi gani za makusudi katika kumaliza mapigano hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kwa ruhusa yako napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwera Charles Nyanguru, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inafanya juhudi mbali mbali za kumaliza mapigano ya koo kama ifuatavyo:-

1. Mwaka 2004 Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Fredrick Sumaye, alifika katika Wilaya ya Tarime kwa shabaha ya kutafuta ufumbuzi katika matatizo ya migogoro ya ardhi katika Vijiji ambavyo koo zimekuwa zikigombea ardhi kwa muda mrefu sana.

Mnamo mwezi Novemba 2006 aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa alitembelea Wilaya husika na aliteua timu ya wataalamu sita ambao walizingatia maamuzi ya Mheshimiwa Fredrick Sumaye na kutoa utaratibu mpya wa utekelezaji wa mkakati huo wa kuleta ufumbuzi wa tatizo hilo la muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

Serikali imeimarisha hali ua ulinzi na usalama katika vijiji vya Buganjo Wilayani Rorya na Kubiterere katika Wilaya ya Tarime, maeneo yaliyodhihirika kuwa mapito makubwa ya wezi wa Mifugo. Lengo ni kudhibiti wimbi la wizi wa mifugo ambao ndiyo unazua mapigano ya koo za Wamera na Wahunyaga pamoja na koo ya Wanchari na Warenchoka. Vituo hivi vimesaidia kupata taarifa za awali za mapigano yanayopangwa na tumeweza kudhibiti baadhi ya magomvi kabla hayajatokea.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuhimiza hatua za kijamii na kiukoo zipewe uzito kama ifuatavyo:-

(a) Wazee wa kimila washirikishe Serikali katika maamuzi ya kuondoa mapigano.

(b) Kuwashirikisha viongozi wa Serikali za Mitaa ngazi zote katika kutatua matatizo ya migogoro ya ardhi.

(c) Serikali kuendelea kutoa wito kwa taasisi za kidini ziendelee kwa nguvu kueneza mahubiri miongoni mwa jamii pamoja na wanaharakati kwa shabaha ya kujenga umoja miongoni mwa koo mbalimbali.

(d) Mwisho, viongozi wa Serikali na vyama vya Siasa pamoja na Wabunge katika Mkoa wa Mara waongeze jitihada kushirikiana na Serikali Kuu kuleta suluhu katika matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, Serikali inatoa wito kwa wananchi wa Wilaya ya Tarime na Mkoa wa Mara, kwamba kwa ujumla kwamba ushirikiano wao na vyombo vya dola ni muhimu katika kukabiliana na mapigano hayo ya koo.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa vile vita hivi vimedumu kwa muda mrefu:-

(a)Je, Serikali italeta lini kikosi maalum cha kuzuia wizi wa mifugo sehemu za mpakani kama jirani zetu wa Kenya?

(b)Je, ni lini Serikali itawapokonya wanaokuwa wakitumia silaha, hao wezi wamekuwa wakitumia silaha kali za moto kama K47; ni lini Serikali itawapokonya hao wanaoiba mifugo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya mhehimiwa Mwera Charles Nyanguru, kama ifuatavyo:-

Ni kweli hali ya eneo na jimbo lake imeendelea kuwa ni hali ya matatizo, lakini napenda kumwambia kwamba sasa hivi tupo katika utaratibu ambao tutafanya Tarime na

Rorya iwe ni Kanda maalum ya polisi kama vile ilivyo Dar es Salaam na shabaha na lengo kubwa ni kwamba mbali na kwamba kuna hizi gomvi za koo, pia yako matatizo ya ardhi, lakini pia yako matatizo ya wezi wa mifugo ambao wanatoka nchi jirani.

Kwa hiyo, kwa lengo hilo la kuweka Kanda maalum katika Tarime na Rorya nafikiri tutakuwa katika njia ya kuweza kujibu na kukabiriana na tatizo hilo kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge.

Na. 32

**Uegeshaji wa Magari Barabarani Kusababisha Ajali**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya mambo yanayosababisha ajali za barabarani ni pamoja na uegeshaji wa magari hususan malori kandokando ya barabara kwa sababu yoyote ile:-

(a) Je, Serikali imeliona tatizo hilo?

(b) Kama Serikali imeliona. Je, ni lini itachukua hatua zipasazo dhidi ya uegeshaji huo holela?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani ya nchi, napenda kujibu swali la mheshimiwa Damas Paschal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, lenye sehemu A, B, and C, kama ifuatayo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeliona tatizo hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua kuweza kuondoa tatizo la uegeshaji wa malori kando kando mwa barabara. Kwa yale yanayoegeshwa kiholela hatua hizi ni pamoja na:-

1. Jeshi la Polisi linafanya operesheni doria barabara kuu kwa lengo la kudhibiti madereva wanaokiuka sheria na kanuni za usalama barabarani na kuwachukulia hatua mbalimbali.

2. Jeshi la Polisi kupitia kikosi cha usalama barabarani na kushirikiana na Wizara ya Miundombinu linaendelea kutoa elimu kwa madereva juu ya matumizi sahihi ya barabara.

3. Sheria ya barabara *Road Traffic Act* No. 30/1973 Cap.168 *Revised Edition* 2002, inafanyiwa marekebisho lakini pia itaweka mtazamo mpya kuhusu madereva wa magari aina zote na wamiliki wa malori na mabasi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malori yanayoegeshwa katika vituo vya *TRA* au Polisi hatua zifuatazo zimekuwa zikichuliwa:-

1. Mamlaka ya mapato *TRA* imepatiwa eneo kwa ajili ya kujenga ofisi za kukagulia mizigo mkoani Pwani ambalo litafanyiwa matayarisho ya kujenga ofisi zao. Kuanza kutumika kwa eneo hilo la maegesho kutaondoa tatizo la msongamano wa malori katika eneo la Mbezi, hivyo kupunguza ajali za barabari.

2. Wizara ya Miundombinu inayo mikakati ya kuboresha huduma sehemu ya mizani ambapo inatarajia kuhamisha iliyo karibu na barabara kwenda upanda wa pili ili kuondoa msongamano wa magari katika eneo la mizani.

3. Wizara ya Miundombinu vilevile kupitia *TANROAD* inaendelea na utekelezaji wa kupanua barabara hasa sehemu za kuegesha magari katika baadhi ya maeneo.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu haya ya serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, msingi wa swali hili ni ongezeko kubwa la ajali za barabarani hapa nchini. Ni kweli doria za Polisi, elimu kwa madereva, pamoja na sheria hii iliyotajwa kwamba mambo hayo yote yapo. Lakini nini matokeo haya, kwasababu tunaona ajali zikiendelea na zingine ni dhahiri kabisa za uzembe zikiendelea hapa nchini?

(b) Je, serikali imefanya utafiti wa kutosha na kupata uzoefu mahali pengine labda tuseme *best practice* ikaridhika kabisa kwamba hayo ndio majibu yatakayosaidia kutatua matazo katika nchi hii?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Ni kweli kumekuwa na wimbi la ajali na Watanzania wetu wengi, jamaa zetu ndugu zetu, rafiki zetu wameangamia kutokana na ajali hizi.

Kwa kweli tunakabiliwa na chamgamoto na hii tunakubaliana kama Serikali, tukiona wenzetu wa miundo mbinu tunajaribu kuweka taratibu tena ambazo zitatizama tatizo hili.

Lakini pia ningependa niseme hapa kwa kumjibu Mheshimiwa Mbunge Nakei, ni kwamba barabara zetu kwa sasa hivi, upana wa barabara ni mita saba, na hili pia moja ni tatizo; na kwamba tunawapa mafunzo madereva, na kwamba tunahakikisha kwamba gari zipo katika hali ambazo ziko sawasawa, ingawaje upo ukiukaji wa aina fulani lakini ukitizama upana wa barabara zetu nyingi ni mita saba na ukitizama upana wa magari, unakuta upana wa basi upana au upana wa lori, inakuwa karibu takribani mita 3. Kwa hiyo, kama gari zinapishana mita tatu kwa mita tatu katika barabara ya mita saba, unaona kuwa tofauti iliyopo inakuwa ni mita moja kwa magari kuweza kupishana.

Na wakati mwingine inakuwa wakati gari moja linataka lipite gari nyingine iliyoko mbele inakuwa haiwezi ikaona gari inatoka kule mbele. Sisemi kwamba ajali zinazotokea ni sahihi ama ni sawa. Tunafanya kila jitihada lakini pia nilitaka niseme

kwamba hata hali za barabara na upana wa barabara zenyewe kwa kweli unachangia na kwenye changamoto ambayo itabidi tuitazame kwa makini sana. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uegeshaji holela wa magari makubwa barabarani ni tatizo kubwa nchini kwetu na kwa kuwa kikosi cha usalama barabarani hakijaweza kudhibiti hali hiyo na pamoja jitihada zote hizo zinazofanywa na Serikali.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa wa kutenga maeneo ya dharura kwa ajili ya uegeshaji wa malori?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, mimi nilivyolichukulia ni kwamba ametoa mawazo na nataka kumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hayo mawazo tumeyachukua na tumeyapokea tutayafanyia kazi. Ahsante sana.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyombo vya usalama barabarani vimekuwa vikitoa elimu kwa madereva na kwa raia kuhusu matumizi ya usalama barabarani. Na kwa kuwa katika Jiji la Dar es Salaam *traffic light* madereva wanapita katika taa nyekundu na kusababisha ajali mbalimbali. Je, *traffic* hawaoni sasa ni wakati muafaka wa kutoa elimu ya matumizi ya taa za barabarani kwa madereva wa Jiji la Dar es Salaam na Tanzania kote? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli elimu tunatoa. Labda tuzidi tu kuweka kasi. Lakini pia niseme na niseme hapa Watanzania wote wananisikia wapo madereva ambao ni wakaidi, Elimu kweli wanaijua lakini wanafanya makusudi. Anaiona kwamba taa ni nyekundu na maana ya kuwa wekundu ule ni kwamba lazima asimame lakini basi anakuwa ni mkaidi. Kwa hiyo, elimu tunatoa lakini pia ukaidi wa madereva upo. Kwa hiyo, cha kufanya hapa ni kwamba pale ambapo inawezekana polisi wa *traffic* itabidi wawe wakali zaidi. (*Makofi*)

Na. 33

**Kuanzishwa Kambi ya JKT Rufiji**

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA** aliuliza:-

Kwa kuwa Rufiji ina ardhi kubwa yenye rutuba na maji mengi:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Kambi kubwa ya JKT kwa maana ya kulima mashamba makubwa ili yawe mashamba darasa kwa wananchi wengine?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa katika mkakati wake wa kurudisha tena utaratibu wa kujiunga na Jeshi kwa mujibu wa sheria, lina mpango wa kufufua makambi ya zamani na kuanzisha makambi mapya.

Hivyo, JKT litaiomba rasmi Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kulipatia Jeshi hilo ardhi isiyopungua ekari 1000 katika eneo lenye miundombinu ya barabara, maji na umeme ambayo itawezesha kambi itakayoanzishwa hapo kumudu kuhudumia askari wengi watakaokuwepo kambini hapo.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa kambi hiyo kutawezesha kilimo cha mashamba makubwa ya mazao mbali mbali kuanzishwa na hivyo kuwapa fursa wananchi wa Wilaya ya Rufiji kujifunza kupitia mashamba hayo.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa majibu yanayoridhisha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Lakini ninalo swali moja tu la nyongeza. Kwa vile hali ya chakula duniani ni mbaya sana hasa nafaka, na kwamba Rufiji inaweza kutoa nafaka za aina zote. Je, Waziri atanihakikishia kwamba wanapofufua kambi za *National Service* Rufiji itakuwa ya kwanza?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hali ya chakula duniani sasa hivi si nzuri sana, na ni kweli kwamba kuna wawekezaji wengi ambao wamekwishakuja kutaka ushirikiano pamoja na SUMA JKT katika uzalishaji wa chakula. Kwa hiyo, ninaweza nikamhakikishia Mheshimiwa Profesa Mtulia kwamba jitihada zitafanyika ili kwa kuwa Rufiji ina ardhi nzuri na maji mengi tutaipa kipaumbele katika uanzishwaji wa mashamba hayo. (*Makofi*)

Na. 34

**Sare za Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania**

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania *TPDF* hasa zile zenye mabakamabaka zimekuwa zikivaliwa ovyo na baadhi ya raia na vikundi vya sanaa hapa nchini bila Serikali kuchukua hatua zozote za kukataza uvaaji wa sare hizo:-

(a) Je, Serikali imeruhusu uvaaji wa sare hiyo ya kijeshi?

(b) Kama jibu la swali a ni hapana. Je, kwa nini uvaaji wa sare hiyo unaongezeka hasa kwa vikundi vya kwaya vya madhehebu ya kidini?

(c) Je, ni kitu gani kinachowavutia wana sanaa hao na baadhi ya raia kupenda kuvaa sare hiyo badala ya ile ya Jeshi la Magereza, Mgambo na kadhalika?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haijaruhusu uvaaji wa sare hiyo. Uvaaji wa sare kijeshi au zile zinazofanana na mavazi ya kijeshi ni makosa kwa majibu wa sheria ya Usalama wa Taifa yaani *National Security Act No. 3* ya mwaka 1970 kifungu cha 6 (1)(a).

(b) Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa uvaaji wa sare hiyo ni kwenda kinyume na sheria kunakotokana na ama ukaidi wa vijana wetu au kutokufahamika vizuri kwa sheria inayozuia uvaaji wa sare hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, wanasanaa wanavutiwa na vazi hilo bila ya shaka kwa kulipenda Jeshi lao bila kujua sheria zinakataza uvaaji wa mavazi ya aina hiyo ambayo mhusika akipatikana na hatia hukumu yake inabeba kifungo kisichozidi miaka 20.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti uvaaji holela wa sare za kijeshi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, limeshatoa tamko la kukemea vitendo hivyo kwa wafanya biashara na kwa wananchi. Aidha JWTZ limewataka wanaohusika na uingizaji wa bidhaa katika bandari zetu kuzuia mavazi ya aina hiyo yasiingie nchini. Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya sheria inayokataza kuvaa mavazi hayo.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumwuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba jamii bado haijaelewa sheria ya mwaka 1970 takriban miaka 40 iliyopita, na ndiyo maana ongezeko la uvaaji wa sera hizo umekithiri kwa sasa hivi na hadi sasa hata kwaya za baadhi ya madhehebu zimekuwa zikivaa. Pamoja na kwamba elimu inatolewa. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba Sheria hiyo ni ya siku nyingi na inatakiwa ifanyiwe marekebisho iletwe hapa Bungeni? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Spika, siamini kwamba sheria hii imepitwa na wakati kwa sababu inatoa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka 20. Hiyo ni sheria kali ambayo kwa kweli kama itasimamiwa vizuri inakidhi haja. Cha msingi kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba ni lazima tufanye kazi mbili kwa ziada. Ya kwanza, ni kuendelea kutoa elimu kwa umma ili suala hili lieleweke vizuri.

Lakini la pili, ni kuhakikisha kwamba tunazuia uingiaji wa mavazi haya katika maeneo ya bandari zetu na *Airports*. Suala hili likishughulikiwa vizuri nina uhakika tatizo hili tutalimaliza.

**SPIKA:** Naomba asaidiwe pale.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Kwanza, mshukuru Mheshimiwa Abdislaam Khatib aliyekusaidia hicho chombo. *(Kicheko*)

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Kwa kuwa suala hili la uvaaji wa nguo hizi zinazofanana na za kijeshi ni suala ambalo limewahi kuendelea kwa muda mrefu. Je, kama Wizara hatua gani iliwahi kuichukua kwa watu hao ambao wanavaa sare hizo na imekuwa kwa muda mrefu?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Spika, hatua kadhaa zimechukuliwa. Moja ikiwa ni kuhakikisha kwamba nguo zinazofanana na sare za jeshi zinazoingia nchini kupitia bandari zetu au viwanja vya ndege zinazuiliwa na kuteketezwa.

Aidha, huko nyuma kumekuwa na utaratibu maalum wa kuruhusu aina ya nguo hiyo kupitishwa tu katika nchi yetu kama zipo *trans* kuelekea nchi nyingine.

Lakini kwa zile ambazo zinakusudiwa kwa ajili ya Tanzania basi zimekuwa zikizuiwa. Hii ni hatua ya msingi kwa sababu nguo hizo hazitengenezwi nchini, na kama jitihada hizi zitaendelea kwa dhati tuna uhakika kwamba tatizo hili litatoweka.

Katika kila hatua ya mtengamano wa Afrika Mashariki, Serikali za Mitaa huwakilishwa ama kupitia Serikali Kuu ama kupitia kwenye umoja wao unaojulikana kama Umoja wa Serikali za Mtaa za Afrika ya Mashariki, yaani *East African Local Government Association*, ambao unashirikishwa kikamilifu katika hatua mbalimbali za utengamano. Kwa hivi sasa umoja huu kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya umekuwa unashiriki kikamilifu katika mchakato wa uhamasishaji wananchi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(b) Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 (a) cha mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya kinatilia mkazo kushirikisha wananchi katika maamuzi yote kwa kuwa Jumuiya hii mpya ni ya watu, yaani *Poples' Centred Community*. Kwa hiyo, ushirikiano uliopo sio wa viongozi bali unawahusisha zaidi wananchi. Mfano mzuri wa ushirikishwaji ni ule uliotumika wakati wa kuanzisha Jumuiya na hadi kusainiwa kwa mkataba. Aidha, wananchi walishirikishwa kikamilifu wakati wa kukusanya maoni ya wananchi juu ya kuharakisha au kutoharakisha uundaji wa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Hivyo hakuna maamuzi yoyote makubwa yaliyofanyika ama yatakayofanyika bila ya kupata ridhaa ya wananchi au Mabunge ya nchi wanachama ambayo yanawakilisha maoni ya wananchi.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, mimi niko kwenye Kamati ya Utendaji ya Shirikisho hili la Afrika Mashariki na kwa kuwa, umoja huu unakwenda vizuri sana na ni umoja unaojitegemea, unaowawakilisha wananchi wote, je, Waziri haoni kwamba ni muhimu chombo hiki kikapewa nafasi kwenye Sekretarieti badala ya kuwakilishwa na watu wengine?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba chombo hiki ni muhimu sana na kinafanya kazi nzuri. Lakini chombo hiki hakiwezi kuwa sehemu ya Sekretarieti kwa sababu Sekretarieti ina majukumu yake, lakini chombo hiki kinaweza kuwa taasisi shirikishi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

La msingi ni kwa chombo hiki kuleta maombi yake rasmi katika Jumuiya na baadaye Jumuiya itatazama vigezo kama vinafikiwa na ndipo itapeleka kwa Wakuu wa Nchi Wanachama ili kuona kama jambo hili linaweza kuwa taasisi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Na. 37

**Mifereji ya Maji Katika Barabara ya Himo - Arusha**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati barabara ya Himo – Arusha inajengwa mifereji yote ya maji toka Moshi Vijijini inayokatiza barabara ilielekezwa katika mito iliyopo ambayo ni mto Rai, Mto Wahindi na kadhalika na kwa kuwa, wakati wa masika kila mwaka Kata ya Msangara inakumbwa na mafuriko:-

(a) Je, ni lini Serikali itawaondolea kero wananchi wa maeneo hayo?

(b) Je, wananchi wanaopoteza maisha na mali zao kwa sababu ya mafuriko watafidiwaje?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati barabara ya Himo Arusha inajengwa mwaka 1996 mpaka 1998, Serikali ilizingatia usanifu na ujenzi unaokidhi sheria na sera za mazingira. Masharti ya ufadhili wa barabara hii uliofanywa na Benki ya Maendeleo ya Afrika yalikuwa ni pamoja na ripoti ya mazingira ambayo Serikali iliyatimiza. Hivyo, wakati barabara inajengwa makalvati na mifereji ya maji ya mvua ilijengwa kwa kufuata usanifu ambao ulizingatia mikondo ya asili na mito pamoja na vijito katika maeneo ilimopita barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, mafuriko yanayotokea mara kwa mara katika Kata ya Msaranga hayatokani na usanifu pamoja na ujenzi wa barabara hiyo isipokuwa yanatokana na uharibifu wa mazingira unaowezekana kuwa umefanyika kwa kuendesha

shughuli mbalimbali za wananchi. Kwa hali hiyo Serikali haihusiki na fidia yoyote kutokana na mafuriko hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kwa wananchi kuzingatia kanuni za utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuepuka kuchepusha maji kwenye mashamba kwa kuweka mifereji mipya na badala yake waache maji yapite kwenye mikondo ya asili ya mito ambayo ilizingatiwa wakati wa usanifu na ujenzi wa barabara ya Himo – Arusha.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Majibu ya Mheshimiwa Waziri yanaweza kuwa yalikuwa halali mwaka wa 1996, lakini mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira ya wakati huu ni tofauti na mafuriko yamekuwa yanatokea katika nchi hii kwa ajili ya mabadiliko ya hali ya hewa. Namwomba Mheshimiwa Waziri, akipata nafasi aende akaone yeye mwenyewe hali halisi; sio kweli ya kwamba makalvati yalijengwa kufuata mifereji au kufuata mito. Ilikuwa imeelekezwa na wakati ikijengwa nilikuwepo, tulipiga kelele lakini hawakutusikiliza. Kwa hiyo, ningependa aje aone mwenyewe hali halisi ilivyo na watu wanavyoathirika.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane naye tu kwamba wakati mwingine mabadiliko ya hali ya hewa kweli yanaweza yakasababisha hali ikabadilika kutokana na mazingira ya awali. Kwa hiyo, nipokee tu mwaliko wake kwamba tutashirikiana naye na nitakuwa radhi kwenda kule Moshi ili tuweze kuangalia mazingira hayo na tuangalie utaratibu wa kuweza kusahihisha hali hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho limeahirishwa kwa sababu limetolewa TAMISEMI na kupelekwa Miundombinu. Kwa hiyo, walikuwa wanajaribu kushughulika nalo TAMISEMI, baadaye limepelekwa miundombinu jana au juzi, kwa hiyo nimetoa muda kwa Wizara ya Miundombinu kulifanyia kazi na litaletwa siku nyingine. Kwa hiyo, maswali yamekwisha na kipindi cha maswali pia kimekwisha.

Matangazo tukianza na wageni; wageni wa Mheshimiwa Luckson Mwanjale kutoka MbeyaVijijini na Mkoa wa Mbeya kwa ujumla ni kama ifuatavyo:- Ndugu Williams Mwali, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya Vijijini, naomba asimame ili kumtambua, ooh hongera sana. Ndugu yetu huyu ni mlemavu wa ngozi lakini demokrasia haichagui, wananchi wanaona kwamba anafaa sana na kutokana na matokeo ya uchaguzi nadhani hakuna shaka kwamba anafaa kwelikweli. Ndugu Allan Mwaigaga, Meneja wa Kampeni, ahsante sana, karibuni sana. Leonidasti Gama, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya; Hassan Dumwala, Katibu wa CCM Wilaya ya Mbeya; Freddy Mtowanga, Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya; Merry Mwansengo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya; Samuel Ntenga, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM Wilaya; Anthony Mboma, Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya na Juma Dea, Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya. Nadhani ili chama cha siasa kifanikiwe ni lazima kiwe na mtandao mpana kama huu ninaousoma hivi sasa, uwe na vijana, wanawake. *(Makofi/Kicheko)*

Pia kuna familia ya Mheshimiwa Mbunge ambao ni Margareth Mwanjale, mkewe; Finess Mwanjale, dada yake; Subi Mwanjale, mwanawe na Juliana Mwasegile, nduguye

na Mheshimiwa Mbunge, Luckson. Karibuni sana na poleni na tabu ya misukosuko, lakini mmekwishafika mwisho na sasa mnavuna matunda ya kazi kubwa mliyoifanya.

Vile vile kuna viongozi wa Kanisa la Uinjilisti Tanzania, haijulikani hawa ni wageni wa nani? Basi nitawatambua kama ifuatavyo: Mchungaji Adam Ndogolo, Makamu Mwenyekiti wa Kanisa la Uinjilisti Tanzania. Aah, naona wanatoka huko huko Mbeya Vijijini, nadhani ndio walisaidia katika dua na sala. Mchungaji Julius Mwaiteleke, Meneja Karibuni *Centre* Mbeya; Hakimu Mwalupindi, dereva wa Kanisa na Emmanuel Mwashamba naye ni dereva wa Kanisa. Kwa kawaida huwa hatuwatambui madereva lakini kwa sababu mmetoka katika shughuli nzito basi mmepata upendeleo, karibuni sana.

Kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Mussa Hassan Zungu, ni wanafunzi 20 pamoja na walimu kutoka shule ya Sekondari ya Benjamin Mkapa ya Dar-es-Salaam, simameni pamoja na walimu. Karibuni sana hapa Dodoma. Tunawashukuru walimu kuwaleta wanafunzi kuweza kujionea *live* jinsi Bunge linavyofanya kazi yake. Karibuni na mnaporejea safari njema na wanafunzi msome kwa bidii, Tanzania inawahitaji nyote katika fani mbalimbali, ahsante sana.

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Hezekiah Chibulunje, ambao ni Robert Teu kutoka Kibakwe Mpwapwa; Alpha Chibulunje na mkewe Mariam Chibulunje, ahsante na karibuni sana.

Tunao pia viongozi wa Serikali ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, kama ifuatavyo: Malima Joram, Rais wa Serikali ya wanafunzi; Judith Abdallah, Makamu wa Rais wa Serikali ya Wanafunzi Chuo Kikuu Cha Dodoma. Naona hawa nao wanazingatia jinsia. Yupo Charles Lyimo, huyu anajiita Spika, Spika wa Bunge la Wanafunzi, bado una kazi ndefu ya kujifunza masuala haya. Kwa hiyo, ukitaka kupata *tuition* tena kwa bure basi tuonane onane nikiwa Dodoma. Sitozi chochote kwa sababu sina tamaa. Yupo Kasalali Emmanuel, Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi; Niyenzi Kilian, Waziri wa Katiba, Sheria na Utawala Bora. Laah! Eeh, hawa jamaa wamejipanga kweli kweli.

Pia yupo ndugu Joseph John, Waziri wa Habari; Emmanuel Ngira, Waziri wa Taaluma. Naona yeye anaendelea na vitabu tu, hayuko hapa. Yupo Amsabi Jeremiah, Waziri wa Fedha na Uchumi; Mtui Richard, Waziri wa Huduma za Chakula na Nyangusi Mausai, Waziri wa Mikopo ya Wanafunzi.

Looh! Halafu wapo Manaibu Mawaziri, Martin Josiah na Tumaini Samuel na Ernest Kaonga, Katibu wa Bunge la Wanafunzi; Denis Mungai, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Chuo Kikuu cha Dodoma. Mwenyekiti wa Tume, hayupo, ahsante sana. *(Makofi).*

Wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, ambao ni Dokta Bakari Nunduma, Mwalimu na Mshauri wa Mheshimiwa Mbunge, ambaye anatokea Chuo Kikuu Huria, yule pale.

Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka wa Simanjiro anao wageni wawili, bwana Edward Porokwa wa *Pingo's Forum* ni *AZAKI* hiyo, yule pale na bwana Moses Sangali, wanawakilisha *AZAKI* sita za Jimbo la Simanjiro. Karibuni sana kutoka Simanjiro.

Huo ndio mwisho wa matangazo ya wageni, sasa matangazo ya kazi zetu:

Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, anaomba leo mchana saa 07.00 Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma wakutane katika Ukumbi namba 231.

Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Sheria Ndogo wakutane leo ukumbi namba 219 mara baada ya kipindi hiki cha maswali.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwisho wa matangazo, Katibu tuendelee na shughuli nyingine.

## KAULI YA SERIKALI

### Kauli ya Serikali Kuhusu Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2008, Bunge lilijadili kuhusu hoja binafsi ya Mheshimiwa Dokta Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, iliyohusu haja ya Serikali kuboresha tasnia ya uwindaji wa kitalii nchini. Hoja hiyo ilifuatiwa na kupitishwa kwa Azimio la Bunge kuhusu ugawaji wa vitalu vya uwindaji na bei zake.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia hoja hiyo na kuwezesha utekelezaji wa Azimio la Bunge, Wizara iliunda kikundi kazi, yaani *task force* cha Wajumbe 13 ambacho pamoja na kufanya rejea ya taarifa zilizotangulia kilitakiwa pia kupitia nyaraka muhimu zote za nyuma na kutoa mapendekezo ya kuboresha biashara ya uwindaji wa kitalii Tanzania. Aidha, sambamba na kazi hiyo, Wizara hiyo iliitaka taasisi ya utafiti wa wanyamapori nchini, yaani *Tanzania Wildlife Research Institute,* kufanya tathmini ya vitalu vinavyotumika kwa uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, katika kazi hiyo *TAWIRI* walitakiwa kupanga vitalu katika makundi kulingana na ubora ambao unazingatia yafuatayo:-

(a) Aina na idadi, yaani uwingi wa wanyamapori waliopo;

(b) Mtawanyiko wa wanyamapori katika vitalu husika; na

(c) Ukubwa wa vitalu na hali halisi ya mazingira ya maeneo ya uwindaji ikiwa ni pamoja vitalu hivyo kupitika kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge Kuhusu Ugawaji wa Vitalu vya Kitalii. Hoja zilizotokana na Azimio la Bunge zinazohusu zaidi uboreshaji wa tasnia ya uwindaji wa kitalii na kuzingatia malengo yafuatayo:-

(a) Kuboresha ushiriki wa Watanzania katika tasnia;
(b) Uwazi na uwajibikaji;

(c) Namna ya kuongeza mapato;

(d) Mfumo bora wa kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii;

(e) Ufuatiliaji na uthamini;

(f) Usimamizi na uendeshaji wa uwindaji; na

(g) Kuiweka Tanzania katika soko la utalii duniani.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza matakwa ya Azimio hilo, Wizara imeanza kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa suala hili linazingatiwa ipasavyo katika Muswada wa Sheria ya Wanyamapori. Aidha, hatua za utekelezaji kulingana na azimio la hoja binafsi ya Bunge ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, namba moja ni kuboresha ushiriki wa Watanzania katika tasnia ya uwindaji wa kitalii. Katika hili tathmini ilifanyika na imebaini kuwa ushiriki wa Watanzania katika uwindaji wa kitalii ni mdogo. Hivyo, ili kuondoa kasoro zilizopo suala la ushiriki wa Watanzania litabainishwa katika Muswada wa Sheria hiyo. katika hilo Wizara itafanya marekebisho kwenye kanuni za uwindaji wa kitalii na zile za kusimamia maeneo ya hifadhi ya jamii, yaani *Wildlife Management Areas (WMAs),* ili yafuatayo yatekelezwe kikamilifu:-

(a) Kuruhusu umiliki wa hisa katika kampuni, ambapo Watanzania watamiliki si chini ya 25% ya hisa zote. Aidha, taratibu za kuhamisha umiliki wa kampuni zitaainishwa.

(b) Kumilikisha vitalu kwa kampuni za kigeni ambazo hazitazidi 15% ya kampuni zote za uwindaji wa kitalii.

(c) Kampuni zote za uwindaji kuwa na wawindaji bingwa wa Tanzania kwa kiwango kisichopungua 50% ya wawindaji bingwa wote waajiriwa wa kampuni husika.
(d) Kuboresha utoaji wa mafunzo kwa wawindaji bingwa na wamiliki wa viwanda vya kutengeneza taswira na nyera, yaani *taxademists.*

(e) Kupunguza urasimu katika kuanzisha maeneo ya hifadhi ya jamii, yaani *Wildlife Management Areas (WMAs).*

Mheshimiwa Spika, namba mbili ni Uwazi na Uwajibikaji. Katika hili wadau wengi wa tasnia ya uwindaji wanalalamika kuwa mfumo wa sasa wa ugawaji wa vitalu hauko wazi, hivyo Wizara itafanya yafuatayo:-

(a) Kuweka vitalu vya uwindaji katika madaraja kulingana na ubora wa rasilimali iliyopo.

(b) Kuingiza Kamati ya Ushauri ya Ugawaji Vitalu kwenye Sheria, ambayo sasa iko kwenye Muswada.

(c) Kuweka wazi mfumo wa ugawaji wa vitalu kwa kutangaza kwenye vyombo mbalimbali vya habari.

(d) Kutangaza vitalu vyote mara vinapokuwa wazi.

(e) Kuweka mfumo wa ugawaji vitalu kwa kuzingatia madaraja ya ubora.

Mheshimiwa Spika, namba tatu, ni kuhusu namna ya kuongeza mapato na mfumo bora wa kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii. Ili kuongeza mapato na kuweka mfumo bora wa ugawaji wa vitalu, Wizara inakusudia kufanya yafuatayo:-

(a) Kupanga bei ya vitalu kulingana na ubora na madaraja yake.

(b) Kuweka mfumo wa wazi na wenye tija wa kugawa vitalu, yaani kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo mnada, zabuni na ugawaji wa kutumia Kamati ya Ushauri.

(c) Kuangalia upya mfumo wa safari, *packages* kwa maana ya aina ya idadi ya wanyama watakaostahili kuwindwa na mgeni mmoja kwenye safari moja ya uwindaji.

(d) Kukuza utalii wa picha katika vitalu kipindi ambacho uwindaji haufanyiki.

(e) Kuongeza ada ya kusafirisha nje ya nchi nyara zitakazotokana na uwindaji wa wenyeji ambapo itakuwa 20% ya kiwango cha ada ya uwindaji wa kitalii kwa mzawa, yaani *citizen* na 33% kwa mgeni mkazi, yaani *resident non citizen* kwa kila aina ya nyara.

(f) Kuweka mfumo wa kutumia kompyuta katika kutoa vibali, kukusanya na kuchambua takwimu za mapato, yaani kufanya *computerised revenue collection system*.

(g) Kupitia upya kanuni kwa lengo la kuongeza kipindi cha uwindaji wa kitalii kwa baadhi ya maeneo.

(h) Kuanzisha utaratibu wa kulipia ada za wanyama kabla ya kuwinda, yaani kuwa na *upfront payment* ambayo pia itakuwa ni *non refundable.*

(i) Kuongeza idadi ya vitalu kwa kuvigawanya vitalu vikubwa na vyenye sifa stahili.

Mheshimiwa Spika, namba nne, ni kuhusu ufuatiliaji na uthamini, yaani *monitoring and evaluation* ya shughuli za vitalu. Wizara imekusudia kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha sehemu ya ufuatiliaji na uthamini katika Idara na taasisi husika;

(b) Kuandaa mfumo ulioainishwa katika kukusanya na kuhifadhi takwimu na taarifa mbalimbali; na

(c) Kujenga uwezo wa Idara na taasisi zake na watumishi katika kukusanya, kuhifadhi na kuchambua takwimu.

Mheshimiwa Spika, namba tano, inahusu usimamizi na uendeshaji wa uwindaji. Katika hili Wizara imekusudia kuchukua hatua zifuatazo:-

1. Kuongeza idadi ya watumishi wenye sifa katika usimamiaji, uwindaji wa kitalii na kuwaongezea motisha.

2. Kuziwezesha kisheria Halmashauri za Wilaya na *WMAs* kuingia mikataba na wawekezaji katika maeneo ya uwindaji yaliyo chini yao.

3. Kuweka mfumo wa kufuatilia utendaji wa watumishi wanaosimamia uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, namba sita, inahusu kuhakikisha Tanzania inakuwa kwenye soko la utalii duniani. Katika hili Wizara imejipangia kutekeleza yafuatayo:-

1. Kushiriki mara kwa mara katika maonesho ya Kimataifa ya uwindaji wa kitalii.

2. Kuweka viwango vya chini vya ajira kwa watumishi wanaojihusisha na kuhudumia watalii na shughuli za kuandaa nyara.

3. Kuweka mfumo wa kuhakiki na kufuatilia mfumo wa utekelezaji wa viwango stahiki vya kuhudumia watalii na kuandaa nyara.

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa Vitalu baada ya mwaka 2009. Kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283 na kanuni za uwindaji wa kitalu za mwaka 2000 pamoja na marekebisho yake, vitalu vya uwindaji wa kitalii vinagawiwa miaka miwili kabla ya kumaliza kipindi cha uwindaji, yaani *hunting term.* Kwa kuwa, kipindi cha sasa cha uwindaji kinamalizika mwaka huu wa 2009, Wizara ilipaswa kugawa vitalu mwaka 2007, yaani miaka miwili kabla ya 2009 kwa ajili ya uwindaji wa kipindi kipya cha kuanzia mwaka 2010. Ugawaji wa vitalu haukufanyika mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sababu zilizosababisha ugawaji wa vitalu usifanyike mwaka 2007 ni kama ifutavyo:-

(a) Kulikuwa na kutokuelewana kati ya wadau, wamiliki wa kampuni za uwindaji wa kitalii na Serikali, hali ambayo ilisababishwa na mabadiliko ya viwango vya ada za uwindaji wa kitalii zilizotangazwa kwenye Mkutano wa Bunge la Bajeti la mwaka 2007/2008. Hali hiyo ilisababisha baadhi ya kampuni kufungua kesi Mahakama Kuu.

(b) Mchakato wa kuunda Sheria mpya ya Wanyamapori ambayo ingehusisha pia taratibu mpya za uwindaji wa kitalii ulikuwa kwenye hatua mbalimbali katika ukamilishwaji wake.

(c) Kuongeza ushiriki wa Watanzania katika biashara ya uwindaji wa kitalii.

(d) Kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ugawaji wa vitalu ili kuchangia zaidi pato la Taifa.

(e) Taarifa ya tathmini ya vitalu iliyofanywa na *TAWIRI* ilibaini kuwa muda wa takribani miaka miwili unatakiwa ili kuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya kutenga vitalu katika madaraja, hivyo kipindi cha mpito kitatoa mwanya wa kukamilisha tathmini hiyo.

Kuhusu ugawaji wa vitalu kwa kipindi cha mpito. Kwa kuwa masuala yote muhimu hayakutekelezwa kwa muda stahiki, mabadiliko makubwa ya biashara ya uwindaji wa kitalii yamechelewa. Ili kuepuka athari zinazoweza kutokea katika kipindi ambacho mchakato wa sheria mpya na kanuni zake unaendelea, kama vile kushuka kwa mapato ya Serikali na Serikali kushtakiwa kwa kukiuka makubaliano ni muhimu Serikali kuweka mazingira mazuri ya kugawa vitalu kabla ya kuingia katika mfumo mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, kipindi cha mpito kinatakiwa ili kutoa nafasi kwa Serikali kutekeleza mambo muhimu yanayohusu changamoto zifuatazo:-

(a) Kukamilisha sheria nakupitia na kuandaa kanuni na miongozo husika katika mwaka wa fedha 2009/2010.

(b) Kukamilisha tathmini ya ubora wa vitalu na upangaji wa madaraja.

(c) Kufuatilia na kutathmini mwenendo wa soko la biashara ya uwindaji wa kitalii hususan kipindi hiki cha hali ngumu ya uchumi duniani ambapo watalii wenye kipato kikubwa wamepungua.

(d) Kutoa fursa kwa kampuni ya uwindaji na wakala zao kuwa na uhakika na uhalali wa kupokea miadi na kusaini makubaliano ya uwindaji wa kitalii katika kipindi cha miaka tatu ijayo, yaani mwaka 2010, 2011 na 2012, kipindi cha mpito cha ugawaji wa vitalu.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto zilizopo Wizara imeweka kipindi cha mpito ili kuwezesha yafuatayo kufanyika:-

(a) Kukamilisha kanuni na taratibu za Sheria mpya ya Wanyamapori katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 ili kuwezesha ugawaji wa vitalu kufanyika mwisho wa mwaka 2010 kwa kuzingatia utaratibu mpya ambao utakuwa umewekwa. *(Makofi)*

(b) Kutoa fursa ya miaka miwili yaani 2011/2012 kulingana na sheria yaani kanuni ya 10(2) ya kanuni za uwindaji wa kitalii za mwaka 2000 na marekebisho ili waombaji watakaopewa vitalu mwaka 2010 waweze kujitangaza na pia kuweza kuingia mkataba na wageni wawindaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia hayo utaratibu mpya wa uwindaji wa kitalii utaanza kutekelezwa rasmi mwaka 2010 ambapo kulingana na sheria ugawaji wa vitalu kwa kipindi cha miaka mitano utafanyika. Hatua hii itatoa kipindi cha miaka miwili cha kuziwezesha kampuni zilizogawiwa vitalu kujitangaza na kuuza safari za uwindaji wa kitalii kwenye vitalu husika.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo wa kipindi cha mpito hautaathiri mchakato wa kuanzisha na kuendesha maeneo ya jumuiya za hifadhi ya wanyamapori za jamii yaani WMAs. Hivyo vitalu vilivyopo kwenye maeneo ya WMAs zilizopo na zitakazoanzishwa vitasimamiwa kwa kanuni za taratibu za WMAs katika kuhakikisha wananchi wananufaika na rasimali ya wanyamapori iliyoko kwenye maeneo yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mmojawapo wa Viongozi katika *Steering Committee* tulikubaliana kwamba kwa jambo muhimu kama hili lipitie mchakato ambao utawezesha Waheshimiwa Wabunge kuweza kuchangia. Lakini kwa vile ilivyoletwa sasa hivi inatufanya sisi kufuatana na kanuni yetu tupate mwongozo

kutoka kwako, inatupa ugumu kuweza kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, ningependa utuelekeze tutafanyaje.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cheyo, tulichoruhusu hapa ni Serikali kutoa taarifa kupitia kauli, si kwamba kwa kupitia hivyo basi mjadala umefungwa, ukitazama vyema kanuni zetu ziko njia mbalimbali kwa asiyeridhika na taarifa hii ya Serikali kuweza kuleta hoja mahususi ambayo inaweza ikajadiliwa humu Bungeni. Kwa hiyo mpira uko kwenu, hilo lililofanyika sasa sio kwamba linafunga mjadala. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni zetu za Bunge, taarifa hii ambayo imetolewa na Serikali hivi sasa kwa kuwa inahusu sehemu muhimu sana ya uchumi wa nchi na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana toka kwa wananchi na wadau mbalimbali wa masuala ya uwindaji wa kitalii, naomba sasa kwa mujibu wa kanuni hoja hii uipangie muda iweze kujadiliwa na Wabunge. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa utaratibu sio huo baada ya Kauli ya Waziri kwa sababu inakuwa sio taarifa ambayo ni taarifa zile za kawaida zilizoletwa mezani ili kusomwa. Huwezi kuanza mjadala hapo hapo au mchakato ukaanzishwa hapo hapo, inatakiwa hoja mahususi iletwe kwangu, niitafakari na kupanga muda muafaka. Niseme tu taarifa nilizonazo ni kwamba Mheshimiwa Kimbita, Mbunge wa Hai, kuna kitu fulani ameandika sijui sekretarieti itatusaidia, kwa hiyo, hayo tuyaache tutaendelea, bado tupo hapa, mbona mna haraka sana, mambo haya hayawezi kuisha kienyeji, yatakwisha kwa kutenda haki kwa wananchi wa Tanzania. Popote ambapo kuna kasoro napenda niwahakikishie na muwe na imani nami, hatutaliachia jambo ambalo pengine linakwenda kwa kasoro. (*Makofi*)

Basi likachukua mkondo tu wa kulindana lindana mpaka mwisho, yako mazingira mengine siwezi kuyasema hapa kwa sababu ni Mwenyekiti wa kikao hiki, lakini yote haya nadhani yatakuja na naomba sana Serikali ijiandae. (*Makofi*)

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho kwenye Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2008
### *The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2008)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nakupa pole wewe na familia yako pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao walipata misiba ndani ya mwaka jana. Pia natoa pongezi kwa wananchi wa Mbeya Vijijini kwa kukipa ushindi Chama Cha Mapinduzi na mgombea wake kuibuka mshindi wa kiti cha Ubunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia sehemu ya VIII ya Muswada inayohusu marekebisho ya Sheria ya Uchawi, *Cap 18*, kwa sababu marekebisho haya naamini yatasaidia sana katika kutoa haki kwa wenzetu wengi wenye ulemavu wa ngozi, ambao kwa sasa wanawindwa na kuuawa ovyo bila hatia kwa imani tu potofu za kichawi kwa kuamini kuwa *Albino* na viungo vyake ni chanzo cha utajiri. Naamini kwa marekebisho yanayopendekezwa vyombo vya kutoa haki vitapewa meno zaidi ya kushughulikia masuala ya kiuchawi kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba sana adhabu kwa watakaothibitika kuwa ni wauaji wa ma-*albino* ziwe kali sana. Huenda itaweza kuwa fundisho kwa wengine kwa sababu mpaka sasa kuna matukio ya mauaji ya *Albino* ambayo wahalifu wanafahamika dhahiri lakini bado kesi zao sifahamu ni kwa nini zinacheleweshwa, kutokana tu na taratibu za mizunguko zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo napendekeza adhabu ziwe kali na ziwekwe hadharani ili kukomesha mauaji yasiyo na sababu kwa watu wasio na hatia yoyote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA ADBALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza pole na msiba wa ndugu, pole sana.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hiyo, ningependa kuchangia katika mambo mawili tu.

Moja, Vyeti vya usajili wa Vizazi kuwa karibu na wananchi na pili Leseni za usafirishaji wa pikipiki (Bajaji).

Mheshimiwa Spika, nikianzia na vyeti vya usajili wa vizazi, kuwa karibu na maeneo wanakoishi wananchi, ni muhimu sana. Sasa hivi tunahitaji sana watu wajisajili kwa manufaa ya umma na manufaa yao wenyewe. Lakini wananchi wanashindwa kwenda mbali kusajili watoto wao. Vyeti vya kuzaliwa ni muhimu sana, vinahitajika kwa mambo mengi ikiwa ni pamoja na:-

- Kuanza shule za msingi, wakati wa usajili.
- Kwenda sekondari unapoanza kidato cha kwanza.
- Kupata Ajira unahitaji pia cheti cha kuzaliwa.
- Kupata *passport.*
- Hata kuwa ushahidi wa mirathi katika familia inapofanyika. ushahidi wa uraia wa nchi fulani.

Lakini utaona kuwa mtu mzima amekosa kusajiliwa kwa sababu tu ya matatizo yaliyompata kwa miaka ya nyuma ikiwa ni umbali ambao ni tatizo kubwa. Kwa hiyo, naunga mkono kuwa suala la kusogeza vituo kwa raia ni muhimu sana kwa sababu wazazi wengi watakuwa na fursa ya kwenda kuwaandikisha watoto wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la hoja ya leseni ya usafirishaji. Naunga mkono kwa asilimia mia moja kuhusu suala la usafiri wa pikipiki au Bajaji kwani vifaa hivyo vinaweza kupenya vijijini kuliko magari au *taxi* nyingine. Pia vina unafuu wa bei ya ununuzi na unafuu wa bei ya kukodi. Kwa hilo, natoa pongezi kubwa sana.

Wananchi sasa watapata unafuu wa usafiri vijijini. Ila tu Madereva wapewe sheria zile za usalama barabarani ili abiria wawe salama. Suala la baiskeli nalo tuliangalie upya litakuwaje?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. HERBERT JAMES MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kupongeza marekebisho kadhaa yaliyotolewa katika Muswada huu. Naomba kutoa mapendekezo yafuatayo kuhusu Sheria ya Bima ya Afya katika Kifungu 25 na 26. Pamoja na kuunga mkono na kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Madiwani kupewa nafasi ya kunufaika na huduma za Mfuko huu, napendekeza yafuatayo:

Madiwani waliotumikia zaidi ya vipindi viwili mfululizo, waendelee na familia zao kunufaika na huduma za Bima za Mfuko wa Afya hata baada ya muda wao kumalizika.

Kuhusu Sheria ya Leseni ya Usafirishaji, unaposoma madhumuni na sababu, tafsiri ya Kiswahili ndani ya Muswada huu utaona kwamba Sheria inalenga na imetaja wazi pikipiki za magurudumu matatu lakini *Part* XI ya Sheria yenyewe sehemu ya 42(c) inatafsirika kama "Matumizi ya pikipiki kwa huduma za umma, pikipiki zote za magurudumu mawili na magurudumu matatu". Lengo ni kuweka hilo bayana ili usiwepo mgongano katika tafsiri halisi. Katika hili naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada wote.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa njia ya maandishi kuipongeza Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Johnson P.M. Mwanyika kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini kuwa Sheria hizi zitawekwa wazi ili ziweze kutenda haki na kulinda maslahi ya Watanzania hasa wale wenye maisha duni ili waweze kuendelea kujitahidi kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie matumizi ya vyombo vya usafiri. Ni ukweli usiopingika kuwa Watanzania tunapishana uwezo, hivyo kila mmoja hujitahidi kupata usafiri kulingana na uwezo wake na matumizi yake. Hivyo basi, Watanzania wengine hutumia baiskeli, pikipiki, pikipiki ya miguu mitatu (Bajaji), mikokoteni, na kadhalika kwa kusafiria na kubebea mizigo yao kutoka eneo moja hadi eneo lingine. Naishauri Serikali kuiweka wazi Sheria kwa kuainisha vyombo hivi vyote.

Mheshimiwa Spika, bila kuiweka wazi Sheria hii itasababisha wananchi kuendelea kupata misukosuko kwa Polisi wa Kitengo cha Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, sheria ya huduma ya tiba kwa wazee na wanafunzi. Nikianza na Wazee, naendelea kuipongeza Serikali jinsi inavyoendelea kujitahidi kutoa huduma ya tiba kwa Watanzania kwa taratibu mbalimbali mfano Bima ya Afya, Afya ya Jamii na Matibabu bure kwa watoto wadogo hadi miaka mitano, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo sasa wa kutoa matibabu bure kwa wazee wasiojiweza kuanzia miaka sitini na zaidi bado unawapa usumbufu wazee wakiwemo wastaafu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke utaratibu ulio rahisi na wa wazi uwe ndani ya Sheria ili huduma hiyo kwa wazee isiwe na vikwazo ama mzunguko wanapofika hospitalini, kwa maana Wizara ya Afya itoe vitambulisho rasmi nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichangie kuhusu wanafunzi. Kwa kuwa wanafunzi wengi kwa ngazi ya chekechea hadi Chuo Kikuu ni kutoka familia maskini, naishauri Serikali itoe msamaha wa malipo ya tiba kwa kada hii ili kupunguza vifo au matatizo wanayopata wanafunzi wauguapo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usajili wa vizazi na vifo**,** naipongeza Serikali kwa kuwa inafahamu umuhimu wa kila Mtanzania kuwa na cheti cha usajili cha kuzaliwa na pia cheti kwa marehemu. Natambua kuwa huduma hii hutolewa kwa Mkuu wa Wilaya, Kitengo cha Usajili wa Vizazi na Vifo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wanapata shida sana kufika kwa Mkuu wa Wilaya kupata utaratibu wa usajili wa kuzaliwa au cheti cha kifo, naishauri Serikali huduma hii kutolewa kwenye Ofisi ya Mtendaji wa Kata ama kwenye Vituo vya Afya ili kuwapunguzia wananchi gharama za usafiri kufika Wilayani. Sheria ikipeleka huduma hii karibu na walengwa naamini kila Mtanzania atakuwa na cheti cha kuzaliwa ama marehemu kupatiwa cheti cha kifo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni matumaini yangu kuwa maoni yangu yatafikiriwa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichangie kidogo tu juu ya Muswada huu katika maeneo mawili tu.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza, Kabidhi Mkuu kusimamia mirathi. Naunga mkono hoja hii au sheria hii, lakini naomba sehemu hii ya mirathi itumike sawasawa na iende na wakati, kwani, wahusika wengine hupata adha kubwa ya kufuatilia mirathi (kesi) na hasa wajane wenye watoto wadogo. Kweli inasikitisha sana kuona watoto wa marehemu wanashindwa hata kwenda shule kutokana na kesi kukaa muda mrefu bila kumalizika. Naomba sheria hii iambatane na muda maalum wa kwisha kwa kesi za mirathi.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la Mfuko wa Bima ya Afya. Napongeza marekebisho na kuongeza wadau (Madiwani) kuwa wahudumiwe na Mfuko huu wa Bima ya Afya. Tatizo moja tu ninalotaka lirekebishwe ni kwamba, Mfuko huu umekuwa ukiboreka siku hadi siku katika kutoa huduma kwa wateja wao, lakini, tatizo bado kuna upungufu wa Madaktari katika Kitengo hiki, wagonjwa wakifika *sometimes* hawaonwi kwa wakati muafaka na Daktari au hakuna kabisa. Pia dawa katika dirisha lao zinakuwa hakuna, hivyo wagonjwa hulazimika kwenda kununua kwenye maduka ya nje na pia kupata matatizo ya kukosa dawa kwa kisingizio cha kuwa dawa ile ni bei kubwa. Mgonjwa analazimika kununua kwa fedha yake kwenye duka ambalo halipo kwenye orodha ya Mkataba na Mfuko wa Bima ya Afya.

Hivyo basi, ushauri wangu ni kwamba, sheria iangaliwe vizuri ili kuwekwe utaratibu wa kuruhusu Mfuko wa Bima ya Afya kuwa na Madaktari wa *Part time* ila walipwe moja kwa moja na Mfuko, ili kukidhi mahitaji ya wateja wake na kuepuka lawama za mara kwa mara. Pia, Mfuko ununue dawa zake zote dirishani kwake ili kuepuka lawama za kwamba Bima ya Afya hawana dawa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru, pia niwashukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Waziri Kivuli wa Wizara hii kwa kuleta Muswada huu. *(Miscellaneous Amendment) Bill, 2008.*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuna umuhimu wa vijana waendesha baiskeli kusajiliwa kwa ajili ya shughuli za kusafirisha abiria. Nchi zetu za jirani mfano, Kenya, Uganda, vijana wamejiajiri na Serikali ya nchi zao zinawapa msaada wa kutosha. Wakati sasa umefika basi baiskeli, pikipiki zipate kuwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uchawi, kwa uelewa wangu hakuna Serikali inayoamini mambo ya uchawi, isipokuwa kwa yeyote atakayepatikana na hatia ya kuua mlemavu wa ngozi (*Albino*) sheria ishike mkondo wake. Kwa mfano, mauaji yakitokea, wahusika waliokutwa na mguu au mkono wa mlemavu wa ngozi, mganga wa jadi aliyeshawishi kwenda kuua na aliyetoa pesa kwa muuaji, wote wawe ni watuhumiwa na wapelekwe kwenye vyombo vya Sheria na Sheria ishike mkondo wake na Mahakama ishughulikie mapema kesi za namna hii ili wananchi wawe na imani na chombo chao, hii ni pamoja na Polisi kufanya uchunguzi mapema. Mahakimu waongezwe katika Mikoa ambayo inaongoza kwa mauaji hasa Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uandikishwaji wa watoto wanaozaliwa na vifo. Ni vizuri Sheria hii itaje wazi ni chombo gani cha kushughulikia uratibu wote. Hata kwenye Vijiji, Kata au Tarafa, bila kuwa makini hasa sehemu za mipakani kama vile Tarime, vyeti vya kuzaliwa vinaweza kutolewa kwa wananchi ambao si Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ni vema Serikali kuzingatia ushauri.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika naomba kuchangia Muswada huu katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kuhusu pikipiki za magurudumu matatu, ni nzuri kuingiza kibiashara kubeba abiria lakini je, sasa hivi wanabeba watu kwa sheria ipi? Wanalipa kodi kwa nani na usafiri wao ukoje *(Plate Number*)? Sheria inapopita nashauri sasa wote walipe malimbikizo kuanzia *Plate Number* ilipoandikishwa na walipe wote.

Mheshimiwa Spika, baikeli nazo ziruhusiwe vijijini tu na wapewe namba maalum ili walipe kodi kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu maharimu kujamiiana. Sheria ifafanue maana baadhi ya makabila, koo, mila, dini mfano Islam, wanakubalika kuoana ndugu katika ukoo. Naomba Sheria ichambue wazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, awali kabisa nampongeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu pamoja na watendaji wengine wote waliohusika katika kutuletea mabadiliko haya ya Sheria zetu mbalimbali. Pili naunga mkono mabadiliko yote na hivyo naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, shida au tatizo langu sijasikia kama *pick-ups* zitaruhusiwa kubeba abiria. Kule kwetu milima ni mingi sana hivyo maeneo mengi usafiri wa baiskeli au bajaj hauwezekani, hivyo tegemeo letu ni *pick-ups* maarufu kama *Toyota Stout*. Hivyo, napendekeza nazo ziruhusiwe maadam wasizidishe kiwango.

**MHE. MARIA IBESHI HEWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu Sheria ya Vizazi na Vifo. Pamoja na kuleta mapendekezo mazuri ya kuirekebisha Sheria hii, nashauri ifuatavyo:-

Serikali isijikite moja kwa moja na taasisi au maeneo ya afya/zahanati, bali pia wajaribu kuangalia maeneo mengine muhimu yanayoeleweka na kutumiwa mara kwa mara na wenyeji wa eneo hilo, kwa mfano, Mahakamani, Ofisi za Watendaji, Kata, Kitongoji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuzungumzia Sheria ya Leseni na Usafirishaji. Katika marekebisho ya Sheria hii, nashauri yafuatayo:-

Baiskeli zitambulike pia katika matumizi kama vyombo vingine vinavyotumika katika kuongeza kipato cha wananchi. Hivyo, wapewe leseni pia. Sambamba na hilo wapewe elimu hii ni kwa nini wanapaswa kutendewa hivyo watumiaji wa vyombo hivyo.

Pamoja na kurahisisha upatikanaji wa vyeti hivyo, swali, je, wale ambao walichelewa kupata vyeti na umri ukapita, nani atawaelimisha kujua waanzie wapi ili nao wajue wana haki ya kupata vyeti hivyo? Nashauri wahusika wawape elimu mapema ya kuelewa kuwa nao wana haki ya kupata vyeti hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake na kuufikia mwaka 2009. Pia nampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya tatu, naishauri Serikali kusogeza huduma ya usajili wa vizazi na vifo hadi ngazi ya Kata. Itasaidia kuondoa usumbufu kwa wananchi wa kutembea umbali mrefu kutafuta haki yao.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya sita, ni vizuri kwa wastaafu au kwa mwanachama ambaye uanachama wake utakoma kwa kifo, basi mjane aendelee kuhudumiwa na Mfuko wa Bima ya Afya. Mfuko huu utoe mwanya kwa Waheshimiwa Madiwani endapo nafasi yake itakoma kwa kukosa Udiwani, aruhusiwe kuendelea kuchangia kama anahitaji. Kwa kuwa huduma ya afya ni ya kila Mtanzania, ni vizuri waruhusiwe wote kujiunga kama wanaweza.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya nane, Serikali ifanye uangalifu sana juu ya Sheria ya Uchawi vinginevyo hali ya mauaji itakuwa kubwa. Ni vyema walemavu wa ngozi wawekewe sheria itakayopelekwa hadi ngazi ya kijiji na adhabu yake. Serikali isitafute ushahidi kwa wanaohusika na mauaji ya walemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya kumi na moja, inayohusu Leseni ya Usafirishaji kwa pikipiki za magurudumu matatu, naiomba Serikali itoe ufafanuzi kwa pikipiki za magurudumu mawili. Kama itasomeka pikipiki za magurudumu matatu, pikipiki nyingine hazitaruhusiwa, naomba iwe wazi. Pia usafiri wa baiskeli maarufu kama daladala nazo naomba ziruhusiwe na ziwekwe wazi kuliko ilivyo. Leseni za kuendeshea nazo ziwekwe wazi katika Sheria ya Usafirishaji, pamoja na Bima yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia mambo ambayo yananisumbua hapa Bungeni. Naomba ufafanuzi na siyo wa juu juu, kuhusu baiskeli hasa Bukoba kwa sababu wakizuiwa Bukoba tu, sehemu nyingine zinafanya kazi hata wale wanaotegemea kupanda huku wakiwa wamebebana na wake zao na mizigo yao watakamatwa. Je, mbona hao sikusikia Sheria hii inasemaje? Je, baiskeli zilizokamatwa muda mrefu zipo Polisi Bukoba mpaka zimekuwa na kutu, huo sio uharibifu?

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii itamke kuwarudishia wananchi au wawapeleke Mahakamani ijulikane, kama sivyo ni unyanyasaji. Naomba itamkwe hapa warudishiwe na je, Sheria inasemaje hapo? Pia Sheria inasemaje kuhusu walioumizwa

na Askari Polisi? Nimechoka sana, imekuwa ndio neno la kila siku hapa Bungeni kama tunavyosema, mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe, je, vipi? Chonde chonde kwa wananchi wa Bukoba.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Napenda kuchangia kwa maandishi katika Muswada wa Sheria Kufanya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya 2008.

Mheshimiwa Spika, marekebisho na kufuta baadhi ya vifungu katika Sheria ya Vizazi na Vifo, Sura ya 108, ni wakati muafaka sasa Serikali itakiwe kuwa na takwimu sahihi za wananchi wake na kupanga vema mipango yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri utaratibu huu uanzie kwenye Wizara hadi kushirikisha Serikali za Mitaa kwa kupewa elimu ya kazi hii pale wananchi wanapofariki au kuzaliwa ili kupata takwimu sahihi kwa kuisaidia (*RITA*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bima ya Afya, Sura ya 395, kufuta fungu 2(1) na kuliandika upya ili Watumishi wa Umma Wastaafu kuendelea kupata mafao, ili Mfuko huu ufanye kazi yake bila ya usumbufu pale wahusika wanapokwenda kupata huduma huambiwa dawa zikizidi kiwango fulani cha fedha wanunue wenyewe. Pia sheria imepanua wigo kwa Madiwani wasiokuwa Wabunge kunufaika na Mfuko huo

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Leseni ya Usafirishaji wa pikipiki za miguu mitatu kusafirisha abiria, sheria imekuja wakati muafaka, wananchi watanufaika na mpango huu wa usafiri lakini ningependa kutoa ushauri kwamba, usafiri huu katika Jiji la Dar es Salaam usiingie katikati ya Jiji kwani utaleta usumbufu mkubwa na kusababisha ajali na pia kuzifanya *taxi* ambazo zitalipa kodi zaidi kukosa soko kwa kuwa hizi bajaji za miguu mitatu zinatoa fedha kidogo usafiri huu uwe sehemu za vituo vya mabasi nje ya Kati ya Jiji, mfano Mwenge, Ubungo Mbezi, Mbagala, Gongo la Mboto na kadhalika zitakuwa zinabeba abiria na kuwapeleka maeneo mbalimbali ambayo usafiri mwingine haufiki.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa kutujalia kufika mwaka huu 2009. Pongezi kwa Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Kurekebisha Sheria Mbalimbali.

Serikali imefanya jambo la muhimu kuhalalisha usafirishaji wa pikipiki na bajaji kwani katika baadhi ya maeneo suala la kusafirisha watu kwa pikipiki liligeuka la kisiasa, kwa kuwa Polisi (*Traffic*) kwa kulinda sheria iliyokuwepo ilibidi kuwaadhibu na wahusika walielekeza lawama na malalamiko kwa Chama Tawala na katika baadhi ya maeneo limeleta mtafaruku mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mamlaka husika itabidi kuweka utaratibu mzuri wa kutoa leseni za hivyo vyombo na katika baadhi ya maeneo zisiruhusiwe hasa katikati ya miji maana siku hizi na magari ni mengi na kwa uzoefu tumeona ajali nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuutambua usafirishaji wa pikipiki na bajaji vijana wengi watajiajiri na hata mamlaka husika zitaongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mwanasheria Mkuu kwa kuleta Muswada huu na naunga mkono hoja.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kutoa ushauri wangu mdogo tu juu ya Muswada huu. Ninaomba kuzungumzia jambo moja tu, nalo ni kuhusu kuruhusiwa baiskeli kuchukua mizigo na abiria kwani hivi sasa kazi hii inafanyika hasa katika Kanda ya Ziwa na kuna baiskeli nyingi zimekamatwa kule Bukoba nazo ziruhusiwe na wananchi wapewe baiskeli zao ili watafutie riziki.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni masikini, hivyo wananchi wetu wakipata nafasi ya kujipatia riziki za jasho lao, waruhusu tusiweke vipingamizi. Ahsante.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza; miaka ya hivi karibuni kumejitokeza familia kugombea mwili wa marehemu. Kila upande wa marehemu hudai lazima azikwe kwa au mume au mke. Je, sheria ya sasa haiwezi ikarekebishwa na kuonyesha wazi wazi sehemu ya kuzikwa badala ya ndugu kugombea maiti?

Mheshimiwa Spika, pili, hivi sasa majalada yote ya aina ya mashtaka fulani fulani lazima yapelekwe Dar-es-Salaam kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Marekebisho yanayotarajiwa kufanyika yaangalie hali ya mikoa iliyo mbali. Ni vyema mtakaowafikiria kukasimu wawe karibu na Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tatu, mbona sheria haijatamka rasmi kuhusu uhujumu unaofanyika kupitia Vyama vya Siasa kwa kutoa hongo ili wachaguliwe kwenye nafasi zinazotoa mianya ya kujilimbikizia mali ya umma. Mfano watoa hongo hujitahidi sana kutoa rushwa na akishapata nafasi anayoitaka, hutumia nafasi hizo kwa au kuiba fedha za Serikali au za Mashirika.

Mheshimiwa Spika, nne, wapanda pikipiki, bajaji na baiskeli waingizwe kwenye sheria wafanye kazi hiyo kwa kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Spika, tano, je, sheria inasemaje wakati magari yakiharibika kwenye barabara kuu kuweka mawe na matawi ya miti kama ishara ya hatari mbele.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilipoahirisha Bunge jana, wasemaji waliojipanga kwa Muswada huu wa mabadiliko ya Sheria Mbalimbali walikuwa wamekwishakamilisha kutoa hoja zao. Kwa hiyo, sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili aweze kuhitimisha kwa kufanya majumuisho na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi ili niweze kuhitimisha hoja yangu. Nianze kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi, nao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Guido Gorogolio Sigonda, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Ania Saidi Chaurembo, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mheshimiwa Mwera Charles Nyangulu, na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

Waliochangia kwa kuongea ni hawa wafuatao: Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala; Mheshimiwa Fatuma Maghimbi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na wa mwisho ni Mheshimiwa Festus Limbu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuishukuru tena Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Lubeleje, kwa maoni waliyotoa. Aidha, nimefarijika sana na mchango wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Nawashukuru sana watu wote kwa michango yenu mizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikianza kwa haraka haraka kuyazungumzia maeneo muhimu yaliyochangiwa naomba nieleze kama ifuatavyo:-

Michango ya Waheshimiwa Wabunge inaweza kugawanywa katika maeneo makuu matano nayo ni haya yafuatayo:-

(i) Uandikishaji wa vizazi na vifo.

(ii) Mfuko wa Bima ya Afya.

(iii) Leseni ya usafirishaji wa abiria.

(iv) Sheria ya uchawi.

(v) Mengineyo ambayo nayo pia ni ya muhimu.

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la uandikishaji wa vizazi na vifo waliochangia ni hawa wafuatao: Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah,

Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Mwera Charles Nyanguru na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

Mheshimiwa Spika, mambo waliyoyazungumzia ni haya yafuatayo: Huduma ya usajili wa vizazi na vifo ipatikane kwa urahisi ikiwa ni pamoja na vituo vya afya na zahanati vijijini. Kuhusu watu ambao hawakuandikishwa je, utaratibu ukoje kwamba kuwe na uimarishaji wa wakala wa usajili, ufilisi na udhamini na Serikali imejiandaa vipi kuhusu uandikishaji wa vizazi na vifo?

Mheshimiwa Spika, majibu yangu ni kama ifuatavyo: Ushauri huu tumeupokea, kwa sasa usajili unafanyika hadi ngazi ya vijijini, lakini utoaji wa vyeti kisheria unatolewa na Msajili wa Wilaya. Hivyo basi, utaratibu unaofaa utawekwa katika kanuni ili kizazi au kifo kikishakusajiliwa kipelekwe kwa msajili ili apate kutoa vyeti.

Mheshimiwa Spika, pili, ikumbukwe kwamba katika marekebisho yanayoletwa sasa mbele yenu Msajili Mkuu amepewa uwezo wa kuwateua Wasajili ambao watakuwa na uwezo wa kutoa vyeti uko katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watu ambao hawakuandikishwa, utaratibu wa kuandikishwa uko katika Sheria na Serikali itaendelea kuimarisha huduma za RITA.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed Rished aliuliza swali kuhusu utaratibu maalum wa kupata vyeti vya kuzaliwa kwa watu waliochelewa kuandikishwa. Mfumo wa kuandikisha ulikuwepo tangu enzi za ukoloni isipokuwa ulikuwa wa kibaguzi. Serikali ina lengo la kuimarisha mfumo huu kwa kutoa huduma za usajili katika hospitali, zahanati za Serikali, Ofisi za Tarafa na Kata. Aidha, utaratibu wa kupitisha maombi ya kuandikisha vizazi na vifo utarekebishwa, sasa waombaji wanaweza kuandikisha vizazi na vifo kwa kutoa vielelezo vyenye kuthibitisha kuzaliwa au kutambulishwa na viongozi wa Serikali katika maeneo yao. Elimu zaidi inaendelea kutolewa juu ya upatikanaji wa huduma hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Martha Mlata, alizungumzia juu ya kesi za mirathi kuchukua muda mrefu kumalizika na kwamba sheria iweke ukomo wa kipindi cha kumaliza kesi hizo na jibu ni kwamba sheria ya utaratibu wa uendeshaji wa kesi za mirathi umewekwa wa kesi kumalizika katika kipindi cha miezi sita hadi mwaka mmoja na kwa taarifa Mheshimiwa Jaji Mkuu amezipa mamlaka Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi kusikiliza kesi hizo. Kabla ya hapo kesi hizo zilikuwa zinasikilizwa na Mahakama Kuu na Mahakama za Mwanzo tu. Tuna imani kwamba utaratibu huu utapunguza kwa kiasi kikubwa muda wa kushughulikia kesi hizo za mirathi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni kuhusu Mfuko wa Bima ya Taifa, huu umechangiwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Herbet James Mntangi, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa John Cheyo, na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyozungumziwa ni haya yafuatayo: Madiwani waendelee kupata huduma hata baada ya kipindi cha uongozi kwisha, wafanyakazi waliostaafu kabla ya sheria hii kuanza wafikiriwe pia Wabunge nao watambuliwe na sheria hii na mwisho Wenza nao waendelee kupatiwa huduma hii hata wakiwa wamestaafu au mmoja kufariki.

Mheshimiwa Spika, majibu yake ni kama ifuatavyo: Diwani aliyemaliza kipindi chake ataendelea kupata huduma zitolewazo kama atatimiza masharti ambayo yatawekwa katika kanuni zitakazotengenezwa pindi Muswada huu utakapopitishwa na Bunge. Kanuni hizi zitahusu pia watumishi wengi na wastaafu ukiwajumlisha wale waliostaafu kabla ya sheria hii kuanza kufanya kazi. Kuhusu Bima ya Afya, kwa Waheshimiwa Wabunge, suala hili limo kwenye sheria ya *National Assembly Administration Act*, ya mwaka 2008 kinachosubiriwa ni utungwaji wa kanuni na utaratibu wa kupata huduma hiyo ambayo nina hakika hivi sasa inafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu matibabu ya wenza, matibabu yatahusu pia wenza na suala hilo pia litajumuishwa katika kanuni baada ya marekebisho haya kupitishwa na endapo mmoja kati ya wenza atafariki aliyebaki ataendelea kupata huduma kwa kipindi chake cha maisha yake yote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa John Cheyo, walizungumza kwamba, suala la dawa liwekewe mamlaka ya udhibiti, au TFDA iongezewe jukumu hilo. Serikali italiangalia suala hili la dawa hasa upande wa bei na uwezekano wa kuongeza jukumu hilo kwa mamlaka ya TFDA. Ushirikiano kati ya mfuko wa *CHF* na *NHF* ili kuwahudumia wazee wakulima na wafanyabiashara, ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itawasiliana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu suala hili. Serikali ilikwishaagiza Mfuko wa Bima ya Afya kushirikiana na mfuko wa *CHF* ili kuboresha huduma, Wizara ya Afya na TAMISEMI ziko katika mchakato wa kukasimu madaraka yao kwa *NHF* ili isaidie Mfuko. Hatua hii itawezesha wafanyabiashara na wakulima kufaidika na Mfuko huu.

Mheshimiwa Martha Mlata, Mfuko uwe na Madaktari wake na ununue dawa zake na kuziweka dirishani; jukumu la kuajiri watumishi wakiwemo Madaktari na kununua dawa ni jukumu la Serikali sio jukumu la Mfuko. Hata hivyo, Serikali imeanza kutekeleza mpango maalum wa afya ya msingi unaolenga kuongeza watumishi wataalam katika Sekta ya Afya na kuboresha huduma mbalimbali zikiwemo huduma za dawa kwa wananchi na wanachama wa Mfuko.

Mheshimiwa Fatuma Maghimbi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani pamoja na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilitoa mapendekezo yafuatayo: Serikali iwe makini katika uendeshaji wa Mfuko wa Bima ya Afya, pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uendeshaji wa Mfuko huo na kuongeza vifaa vya matibabu. Ushauri huo ni mzuri na kwa sasa Mfuko umeanzisha programu ya elimu ya Kata kwa Kata kwa nia ya kuelimisha wadau wananchi na wanachama kuhusu haki na wajibu wao katika huduma zitolewazo. Kuhusu vifaa vya matibabu, Serikali itaendelea kutenga fedha mwaka hadi mwaka ili kuboresha eneo hili la vipimo na uchunguzi na maabara. Mfuko kwa upande

wake unachangia juhudi za Serikali kupitia mpango maalum wa mikopo nafuu ya vifaa tiba. Hadi sasa Mfuko umetoa vifaa vya tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 300 kwa vituo 24 vya matibabu ya umma na binafsi vilivyosajiliwa kwa mkopo nafuu.

Mheshimiwa Spika, eneo la (c) linalohusu Leseni ya Usafirishaji wa Abiria, maoni yalitolewa na Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Rished Abdallah, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Mwera Charles Nyanguru, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

Mheshimiwa Spika, maoni ni kwamba, Serikali ifikirie uwezekano wa baiskeli kama chombo cha usafirishaji wa abiria kibiashara kwa kuwa baiskeli ndizo zinatumika hadi vijijini. Maelezo yetu ni kama ifuatavyo: Wamiliki wengi wa baiskeli ni watu wa kipato cha chini ambao hawawezi kumudu malipo ya ada za bima pindi itokeapo ajali kwa abiria. Pia Makampuni ya Bima yanaweza yakaweka ada za juu sana kwa kinga kwa abiria na kutokana na wamiliki wa baiskeli wengi kuwa na kipato cha chini watashindwa kumudu na hivyo watajiingiza kufanya biashara bila kuwa na kinga. Hivyo ilionekana kwamba ni vyema jambo hili liachwe kwenye mamlaka za Halmashauri, Miji na Wilaya ili zidhibiti na kusimamia uendeshaji wa chombo pembezoni mwa Miji, Vijiji ili kuongeza mapato ya Halmashauri. Wenzetu wa Tanga na Shinyanga wameshaanza kuwa na sheria ndogo na wanasimamia baiskeli hizo na hii imewasaidia kuongeza mapato yao katika Halmashauri zao.
Kwa kuziondoa baiskeli kutumika kibiashara mijini kutawasaidia mambo yafuatayo: Kupunguza msongamano katikati ya Miji na Majiji, kupunguza ajali mijini na hili linaendana na Sera ya usafirishaji ya kutaka chombo kilicho salama kutumika kwa abiria.

Aidha, miundombinu iliyopo hivi sasa katika miji yetu hairuhusu kutumika baiskeli kibiashara ukilinganisha na wenzetu wa nchi zinazoendelea walio na njia maalum kwa vyombo hivi. Kuhusu baiskeli kukamatwa Bukoba na katika maeneo mengine, hili suala ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali italifuatilia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, alizungumzia suala kwamba alipenda kujua kwa sasa pikipiki zinabeba abiria kwa sheria ipi, halafu wanalipa kodi kwa nani? Pia anashauri sheria hiyo ikipita walipe malimbikizo yote tangu walipoanza kufanya shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yataruhusu pikipiki zilizotajwa kubeba abiria, kuhusu suala la malipo ya malimbikizo kwa sasa hivi haiwezekani kufanyika kwani itakuwa vigumu kupata ushahidi wa kuthibitisha suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Fuya Kimbita, anasema *pickup* ziruhusiwe kubeba abiria kwani kule kwenye milima pikipiki na bajaji haziwezi kutumika. Maelezo yetu ni kwamba, utaratibu wa kutumia *pickup* kubeba abiria upo kama ilivyokuwa kwa

magari yanayojulikana kama chai maharage. Kinachotakiwa ni kufuata utaratibu uliowekwa na mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, eneo la (d) kuhusu Sheria ya Uchawi, maoni yametolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Charles Mwera Nyanguru. Maoni yao ni kama ifuatavyo: Serikali iendelee kuchukua hatua kali kwa watuhumiwa wanaoua watu wenye ulemavu wa ngozi kwa imani za kishirikina na kwamba kuwe na sheria mahususi ya kuwalinda walemavu wa ngozi. Maelezo yetu ni kama ifuatavyo: Ushauri huu ni mzuri na Serikali iko makini katika kuhakikisha kwamba watuhumiwa wote wanafikishwa mbele ya sheria pindi wanapokamatwa.

Adhabu ya kosa la mauaji imeanishwa kwenye Kanuni ya Adhabu, tunakubaliana na ushauri kuwa wananchi wajiepushe na imani za kishirikina kwani madhara yake ni makubwa. Aidha, wananchi wanatakiwa kuachana na imani hiyo potofu na tamaa ya kujipatia utajiri wa haraka bila kujishughulisha. Lazima sisi sote tujitahidi kutumia rasilimali tulizopewa bure na Mwenyezi Mungu badala ya kutafuta njia za kijinga za mkato. Kuhusu kuwa na sheria mahususi, tunasema kwamba sheria zilizopo hivi sasa kwa maoni yetu zinajitosheleza.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengineyo ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa wafuatao: Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, alitoa maoni kwamba Mkurugenzi wa Mashitaka akasimishe madaraka kwa watendaji wa Mkoani na Wilayani. Tunasema kwamba ushauri huu tumeupokea na ndiyo lengo hasa la marekebisho yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala imetoa maoni kwamba elimu kwa umma juu ya mabadiliko ya wadhifa wa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya kutenganisha wadhifa wa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria itolewe kwa wananchi. Serikali imepokea ushauri huu na itaufanyia kazi kwani ni kweli kwamba watu wengi walikuwa wamezoea vyeo viwili kushikiliwa na mtu mmoja. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kulizungumzia suala hili leo hii asubuhi.

Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, inatoa maoni kwamba Serikali itatue matatizo yanayozikabili taasisi zinazoshughulika na utoaji wa haki ili kupunguza msongamano wa mahabusu Magerezani. Maelezo yetu ni kama ifuatavyo: Serikali ipo katika mchakato wa kuboresha maslahi kwa watumishi ambayo yataleta tija itakayosaidia kupunguza mambo mengi yanayoikabili sekta ya utoaji haki nchini. Pia imetoa maoni yafuatayo: Imetoa ushauri kwa Serikali kutumia vyombo vya habari vya watu binafsi na asasi zilizo za Serikali ili zisaidie kuelimisha jamii kutokomeza vitendo vya kimapenzi na watu wenye uhusiano wa kindugu. Ushauri huu ni mzuri na kwa kulitambua hilo ndiyo maana Serikali inaleta marekebisho haya ili pale panapotokea kosa kama hili sheria ichukue mkondo wake pale pale pasipo kungojea kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka au Wakili wa Serikali Mfawidhi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ponsiano Nyami alitoa ushauri juu ya kosa la kujamiana kati ya ndugu na ndugu kwani kuna baadhi ya makabila na dini yanaruhusu ndugu kuoana. Maelezo yetu ni kwamba sisi sheria za nchi yetu haziruhusu maharimu kuoana au kujamiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imetoa maoni yafuatayo: ushauri kuhusu Serikali kuendelea kupambana na tatizo la rushwa kwa nguvu zake zote. Tunasema kwamba ushauri huu ni mzuri na Serikali inapigana na rushwa kwa nguvu zake zote na tunashauri wananchi pia watuunge mkono kwenye hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya kisheria. Napenda nirudie tena shukrani nilizotoa kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Msomi Mheshimiwa Fatma Maghimbi kwa mchango wake. Nianze na lile fungu la 52 la sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27 Ibara ya (9) ya mapendekezo ya marekebisho. Nadhani atakubaliana nami kwamba labda sheria aliyoiangalia yeye siyo ile tuliyoitaja kwenye marekebisho yanayopendekezwa. Labda aliyopewa ni sheria ile ambayo ilikuwa haijajadidiwa yaani *the original version*. Kama ataiangalia kwa undani fungu lililopo kwenye Sura ya 27, *revised edition* ya mwaka 2002 ataona kwamba tulichokiweka kwenye mapendekezo yetu hakihitaji masahihisho yoyote yale.

Mheshimiwa Spika, cha pili ni marekebisho kwenye ibara ya 25 ya Muswada ambayo amedai haiendani na sheria inayorekebishwa. Kwa heshima na taadhima naomba nisikubaliane naye kwa hoja hii aliyoitoa msomi. Siyo kweli kwamba marekebisho yaliyopendekezwa hayaendani na sheria tajwa. Fungu analolitaja lilifanyiwa marekebisho na Bunge hili chini ya Sheria namba 25 ya Mwaka 2002. Hivi sasa linasomeka kama ilivyo katika fungu ambalo tunakusudia kulifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ibara ya 44 ambayo inataja fungu la 23(5)(d) na kwamba Sheria ya Ardhi Sura ya 113 haina fungu lenye (e) (d) na (c). Kwa heshima napenda kukubaliana naye juu ya rekebisho hilo, ni kweli fungu lililokusudiwa kufanyiwa marekebisho ni 23 (3) (d) la sheria hiyo. Haya ni makosa ya uchapaji na namshukuru kwa angalizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba tuwe pamoja na tuiunge Serikali mkono kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa majumuisho hayo

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na shughuli zozote nyingine nimepokea ombi linalohusu haki za Bunge kwa mujibu wa Kanuni za Bunge 51. Nimepokea ombi hili kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya. Kwa kifupi ameniandikia na ameniletea nakala ya barua kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Nilipoisoma kwa maudhui yake barua hiyo ya tarehe 16 Januari, 2009 inaelekea kama, kwa sababu sina uamuzi mpaka mtakapoamua ninyi, inaelekea kuvunja maamuzi ya Bunge. (*Makofi*)

Sasa kanuni zinasema hivi: Kanuni ya 51 (1) "Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na haki za Bunge atafanya hivyo wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli za Bunge uliowekwa na kanuni hizi."

Inaendelea lakini ya muhimu hapa ni (4) inasema: "Mambo yanayohusu haki za Bunge yatawasilishwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa katika kanuni hizi na endapo wakati wa kikao chochote cha Bunge jambo lolote litazuka ghafla ambalo litaonekana linahusu haki za Bunge, shughuli zitasitishwa kwa madhumuni ya kuliwezesha jambo hili kuwasilishwa na kuamuliwa isipokuwa tu kama wakati huo ni wa kupiga kura."

Nikizisoma hizi 51(1)-(4) nimeridhika kwamba kuna tatizo hapa linalohusu kuingilia haki za Bunge na kwa mujibu wa Kanuni ya 30(4) (k) inayoweka mpangilio wa shughuli za Bunge inayosema: "Mambo yanayohusu haki za Bunge yanatangulia hoja za Serikali" yaani yana umuhimu kuliko hoja za Serikali.

Kwa hiyo, nimeamua basi kwamba Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya alete hoja yake kwa maandishi leo na kesho baada ya maswali wakati wowote tutaipangia iweze kujadiliwa ili Bunge liamue vitendo hivi na taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kama vinakiuka ama havikiuki haki za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Kwa hiyo, tunaendelea.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho kwenye Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2008
***The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2008)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nachangia nilisema kwamba Waheshimiwa Madiwani kwa sababu zilezile wamerudishwa katika huu Mfuko na wenyewe wanapomaliza muda wao waendelee kuhudumiwa na huo Mfuko. Pia nimeleta *amendment* kwa ajili ya hoja yangu, sasa kama kuna maelezo zaidi labda anipe mtoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John M. Cheyo ameleta mapendekezo ya mabadiliko kwenye kifungu hicho cha 27 na kama anavyosema yeye yanakusudia kwamba Madiwani waendelee kuhudumiwa na Mfuko hata baada ya kumaliza vipindi vyao, ndivyo inakusudiwa. Eeh! gharama je?

Nadhani mimi ningemsihi Mheshimiwa John Cheyo kwa sababu hatujalimaliza pia la Waheshimiwa Wabunge kwa nini haya kwa sababu yanafanana ni watu wanaochaguliwa kwa vipindi maalum isingekuwa vema tulifikie wakati huo ama tuliamue sasa?

Mheshimiwa John M. Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Mwanasheria lakini hii ni Sheria ambayo tunaitunga sasa, sasa tukiiacha hapa kama ilivyo ndiyo kusema hili jambo linakuwa ndani ya Sheria na Sheria inawaambia wasite au isitishwe hiyo huduma mara wanapomaliza muda wao. Lakini kwa kuwa namsikia vizuri mtoa hoja ni vile alielekea kukubaliana na jambo hili, labda apewe nafasi.

**MWENYEKITI:** Kabla sijakuita nimemuona Mheshimiwa Andrew John Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama tu kwa sababu tuko katika kipindi kwenye Kamati ndiyo tunaweka msingi wa ubora wa Muswada ambao unapendekezwa na Serikali.

Kuhusiana na pendekezo alilolileta Mheshimiwa John M. Cheyo linakwenda kinyume kabisa na kusudio la Serikali kwa sababu mapendekezo haya kama Bunge litakubali ndiyo yatawezesha kwa mara ya kwanza kuwaingiza Waheshimiwa Madiwani katika mpango huu. Pendekezo lake ni kuwaondoa kabisa, anasema futa kifungu kinachopendekezwa na Serikali kwenye Muswada, maana ya *delete* ni kufuta yaani ondoa. Sasa ukishaondoa hiyo maana yake ni kwamba, ukienda kuisoma Sheria mama hutakuta kundi la Madiwani.

Sasa ipo hoja kipindi cha uhai wao tu au na baada. Tumemsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, kalieleza hilo. Sasa nadhani tukubali hoja ya Serikali kwa sababu imefanyiwa kazi ya msingi sana na vizuri sana na wewe umeligusia hilo. Suala hilo lina gharama, huwezi ukaibuka tu bila kufanya *actuarial analysis* ya kuweza kuona Mfuko huu utaweza ku-*support* vipi, *implications* zake ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana kwa haya tusiende tu kwa sababu tunataka tulione lakini ni utaratibu ambao tunaweza tukauweka vizuri, tunaanza sasa na baadaye *implications* zake tutaziona vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu!

Baada ya ufafanuzi unaotokana na uzoefu mpana sana alionao mwenzetu Mheshimiwa Andrew J. Chenge ni dhahiri kiufundi hapa Mheshimiwa John M. Cheyo badiliko unalolileta linawaondoa kabisa kwa sababu ukisha *delete*, maana yake umewaondoa hata kile kidogo ambacho kimekusudiwa na Serikali kinakuwa hakipo.

Kwa hiyo, lina matatizo hayo ya kiufundi na kwa sababu linalopendekezwa na Serikali lina nafuu zaidi kuliko hili lako, basi nalikubali hili la Serikali na siku za usoni kama itabidi hata wanapoondoka Udiwani wapewe fursa hiyo, tutaliangalia kwa wakati wake.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

**MWENYEKITI:** Mbona kimya hakiafikiwi mbona kimya tena? (*Kicheko*)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*

Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

**MHE. PONSIANO DAMIANO NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 37 kinachohusiana na Sheria namba 162 kuhusu Maharimu.

**MWENYEKITI:** Maharimu?

**MHE. PONSIANO DAMIANO NYAMI:** Yaani kujaamiiana

**MWENYEKITI:** Ooh! Kiswahili kinazidi kukua, haya.

**MHE. PONSIANO DAMIANO NYAMI:** Maharimu ni wale wenye uhusiano wa damu yaani kama vile ndugu mtoto wa Mjomba, Shangazi na kadhalika kwa wale ambao hawafahamu neno maharimu. Sasa Sheria yetu ni wazi imekataa kujamiiana na watu hao na naikubali siyo kwamba naikataa. Lakini kuna taratibu nyingine ambazo ni muhimu sana za dini kama nitakosea mtanisahihisha.

Kwa mfano dini ya Kiislam, naweza nikawa na mtoto lakini pengine nina mdogo wangu nitolee mfano, Mwananzila hivi ni mdogo wangu na yeye ana mtoto wake, sasa mtoto wangu ni wa kiume au wa kike wanaweza wakaoana na mtoto wa mdogo wangu Mwananzila, Sheria hiyo inakubali na hao ni Maharimu.

Sheria yetu inakaa je, hao watakapokuwa wameoana Sheria itachukua mkondo wake au kutawekwa kaneno fulani kanakokubali mila au baadhi ya dini zinazohalalisha hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufafanuzi katika Sheria je haiwezekani Serikali ikatafuta ka-*clause* angalau kuongeza hapo kwa sababu tayari kuna

uhalali kwa maeneo mengine na ni halali na makabila kama vile Waarabu na wenyewe tunao, Wahindi pia tunao na wenyewe wanakubali kwamba wana ndugu hao wanaweza wakaoana, mjomba kwa shangazi, binamu ni halali kwao. Sheria yetu pamoja na kukataza hilo haiwezi ikatambua hilo? Naomba ufafanuzi na ninaomba pendekezo hilo Serikali tu ikubali mambo yaishe.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto taarifa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wajaribu kutofautisha mila za Kiarabu na mila za Kidini. Taratibu za dini ya Kiislam zipo kwenye *Qur-an*, matendo ya mila za Kiarabu yapo kwa Waarabu, kwa hiyo mfano ambao Mheshimiwa Mbunge ameutoa wa mtoto wa baba mkubwa na baba mdogo ni mila za Kiarabu siyo taratibu za dini ya Kiislam ambazo zimo kwenye *Qur-an*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hiyo taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa ufafanuzi huo na sasa labda Mwanasheria Mkuu, lakini nilivyoelewa ni tofauti kidogo lakini pengine Mwanasheria Mkuu tusaidie.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kanuni za Adhabu iko wazi kabisa katika eneo hilo, inazungumzia juu ya kitu kinachoitwa *Incest by males au Incest by Females.* Wale ambao wanahusika wameainishwa katika Sheria hiyo, kwa hiyo, endapo mtu yeyote atafanya mambo ya kimapenzi ambayo yameainishwa kwenye ile sheria anatenda kosa la jinai. Sababu za msingi ni kwamba, *actually* ni la kisayansi kwamba mnapokutana watu ambao mna damu moja inaweza kuathiri vile vizazi vitakavyofuata. Kwa hiyo, msingi wake ni huo hasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sikubaliani na Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami kuhusiana na jambo hilo nadhani ni vizuri Sheria iheshimiwe kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Aah! Lakini tupate uwazi hapa, hivi kweli Sheria kwa hivi sasa inakataza mtoto wa kaka na mtoto wa mdogo wake huyo au mabinamu, inakataza au ni wale tu ambao ni wa…

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kutazama kwenye Sheria yangu hapa lakini naona haipo hapa. Lakini ukweli ni kwamba ni wale ambao kwa mfano dada na kaka kuoana au babu kumuoa mjukuuu wake au mtoto kumuona mama yake, vitu kama hivyo.

**MWENYEKITI:** Kama ni hivyo nadhani ni sahihi kabisa. Hivi wewe Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami umeng’ang’ania hivi unataka kumuoa nani tena na wewe? (*Kicheko*)

Hata baada ya ufafanuzi huo kwamba ni mtu na dada yake, mtu na mama yake, nyanya na mjukuu na hali hiyo, wewe unasemaje sasa?

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nakubali hiyo sina tatizo, lakini lile alilolisema Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto siyo kweli, ndivyo taratibu za Kiislam zilivyo. Naweka *Hansard* sawa, nadhani watanisaidia Waheshimiwa ambao ni Waislam hapa. Nilichokitamka ndicho hicho.

**MWENYEKITI:** Hiyo ni hatari! Mambo ya imani haya ukijaribu kutafsiri imani za wenzako mara nyingine wanapata taabu.

Kwa hiyo, baada ya ufafanuzi wa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba wanaohusika ni wale damu moja, nadhani sasa limekaa vizuri.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 42

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula na Mheshimiwa John A. Chenge.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Bunge lako lisahihishe *Hansard* kwamba sijasema kifungu chote bali nimesema Kifungu 27(A) kwa hiyo, iwekwe sawasawa hiyo.

Halafu kifungu 25 tumekipitisha ambacho ndiyo Madiwani wanaingizwa, kwa hiyo kwa kuwa watu wengi wananisikiliza wasifikiri sijui kusoma, najua kusoma na nataka hii ieleweke *very clearly*, kifungu cha 25 kinawaingiza Madiwani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 27 tofauti A inatoa sharti la kukoma, hicho ndicho nilichokuwa naseme huo ukomo uondolewe lakini mmeshaamua. Kwa hiyo,

*Hansard* isahihishwe hivyo ili watu wasije wakasoma wakafikiri kwamba Mzee Cheyo hakuelewa, nimeelewa lakini mmeamua vingine ni uamuzi wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Kwenye hilo nikutoe wasiwasi, ni kwamba Watanzania wengi wanakufahamu kwamba ni msomi, ni mtu mzuri na mzalendo. Lakini kwenye hili kwamba uweke mtu akishaonja Udiwani hata siku moja ahudumiwe kiafya mpaka kufa kidogo bado wakati wake, hivyo ndivyo tulivyoamua kama Bunge. Kwa hiyo, tuendelee kwa hii ya sasa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 42 nimesema iongezwe baiskeli na sababu tumesema kwamba kuna haja ya kuendelea na majadiliano makubwa lakini wote ambao wanatusikiliza na wanatutazama wanajua kwamba baiskeli inatumika kubeba nyanya, watu na kadhalika. Nina hakika kuna Walimu wengi sana ambao wasingeweza kufika kwenye vituo vyao kama pasingekuwa na daladala za baiskeli. Sasa unaposema kwamba eti hawa ni watu maskini hawataweza kupata *insurance* jambo hili silielewi kwa sababu gari yenyewe *third part insurance* ni shilingi 13,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashangaa sana kama kutakuwa na kampuni ya *insurance* ambayo kwa baiskeli itaweka shilingi 30,000= na kama ni 30,000/= ndiyo wakati huo wa sisi kusema kuwa hii siyo haki. Pia kama mtu anapata ajali kwa baiskeli ni rahisi sana kutokufa kama vile akipata ajali kwa gari. Sasa tunazungumzia vitu gani na watu hawa wataendelea na mtindo wa namna hiyo ya kuvunja Sheria na Bunge ni ambalo limeletwa na hao wapanda baiskeli. Kwa hiyo, naona hili jambo lingekubaliwa na Bunge lako, Serikali imeleta Muswada lakini sisi pia Kanuni inatukubalia kutunga Sheria tunavyoona ina *fit* mazingira ya hali halisi ya nchi yetu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la baiskeli nadhani nimeshalielezea, siyo kwamba tunakataza baiskeli zisitumike kibiashara, tunachosema ni kwamba zisitumike mijini bali zitumike vijijini. Halmashauri wanaelewa vizuri uwezo wa watu wao kule walipo vijijini, kwa hiyo hata leseni itabidi watoze kiasi gani wanajua. Lakini ukiachia kwenye matumizi ya Sheria hii *then* watakuwa wanatozwa na watu wengine ambao hawawafahamu hawa waendesha baiskeli.

Lingine ni kwamba sasa hivi tuwe tunaanza na huu ni mwanzo tu wa kuingiza pikipiki na hizi za magurudumu matatu ili tuone hali itakavyokuwa, kama hali itakuwa nzuri baadaye tunaweza kuja kuingiza na baiskeli, lakini tuwe na mwanzo, hatusemi kwamba baiskeli haziwezi kuingizwa katika Sheria, tuangalie kwanza hizi pikipiki na hizi Bajaji kwamba tutapata uzoefu gani katika kuzitumia hizi katika Miji Midogo na Dar es Salaam.

La pili, tatizo lingine ni kwamba, tukiziruhusu hizi baiskeli mijini ajali zitakazotokea zitakuwa nyingi sana, sasa tunataka pia tuwalinde Watanzania wasije wakaathirika na ajali ambazo zinaweza kutokana na hizi baiskeli zikiruhusiwa kufanya kazi mijini na kwenye majiji.

Pia lingine ni kwamba tukiruhusu baiskeli tunaongezea uwezo Halmashauri zetu kwa sababu fedha zitakazotozwa kwa hawa waendesha baiskeli zitaingia kwenye Mfuko wa Halmashauri. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba na kwa maoni yangu siyo vizuri kuingiza baskeli sasa hivi katika sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Sasa kwa ufafanuzi wako kinachoruhusiwa vijiji kinaruhusiwa kwa Sheria ipi sasa? Yaani kwa ufafanuzi huo uliotenganisha mambo ya vijijini ambayo ni *perfectly reasonable* kwa kweli hakuna *coalition* za baiskeli vijijini wala hawagongani na magari kwa sababu si mengi, lakini wanaruhusiwaje sasa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, wenzetu wa Shinyanga na Tanga wameshalishughulikia suala hili, wameweka *by-laws* au Kanuni kwenye Halmashauri zao ambazo zinaruhusu matumizi ya baiskeli kwa biashara ya kubeba abiria na tunaomba Halmashauri nyingine pia na zenyewe zifuate hilo ambalo limeshaonyeshwa na wenzetu wa Shinyanga na Tanga.

**MWENYEKITI:** Aah! *Point* ya kisheria hapa ni kwamba *there must be enabling Legislation,* huendi tu Halmashauri ukajitungia tu mambo yanayohusu *traffic* kwa kuwa yanahusu baiskeli basi ukatunga tu mwenyewe. Nadhani hata hao Tanga na Shinyanga pengine wamekosea tu kwa sababu ni Bunge hili hili ambalo lazima li-*enable* hiyo ili Halmashauri zifanye kazi. Kwa nini msiweke *enabling clause* basi tukamaliza hili suala kwamba, *for purposes of bicycles, Local Government Authorities can make necessary Legislation.*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelazimika kusimama kwa sababu mapendekezo yake kiuandishi wa sheria kwanza yana matatizo makubwa.

La kwanza, mimi ninafahamu Serikali imeleta *schedule of amendment,* yeye amejielekeza kuleta marekebisho kwenye sehemu ya Muswada ambayo haisomeki kama ilivyo sasa. Kwa hiyo, Kamati yako tutakuwa tunaipotosha sana kama tunakwenda kwa namna hiyo, lazima ajielekeza katika marekebisho ya ziada ambayo yameletwa na Serikali, yeye ameturudisha kwenye Muswada kama ulivyochapishwa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ukilishughulikia hilo la kwanza, maana Kamati inaweza ikasema kabisa kwamba hatuna mapendekezo yoyote ya kurekebisha kifungu hicho kwa sababu ametupeleka mahali ambapo sipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujielekeze kwa upande wa Serikali, kuna hoja hapa imetolewa kwa suala nzima la baiskeli ambalo kusema kweli hoja hiyo imeiva na hakuna anayeipinga ila ni namna ya kwenda nayo. Sasa kwa vile Serikali imepitia mlango wa sheria ya *Transport Licensing Act,* Sura 317 ya Sheria za Tanzania. Kifungu ambacho lazima tuanze nacho ni tafsiri ya neno *Motor vehicle.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Mwanasheria na Waheshimiwa Wabunge wengi wanaelewa ni kitu kinachoendeshwa na *motor engine* na ndiyo vinafanana pale wanapotaka kuingiza pikipiki ya magurudumu mawili na magurudumu matatu maana zote zinawashwa kwa *motor*. Ukiingiza baiskeli hapo inakuwa ni kituko katika uandishi wa sheria. Tafuta kifungu pekee kama unataka kutambua usafiri wa baiskeli kwa madhumuni haya ambayo tunataka tuyafanye.

Sasa ndiyo maana nilikuwa na wasiwasi mkubwa sana kwa mapendekezo yake yalivyokaa na pili yalivyoandikwa kwa sababu Serikali inatumia uandishi wa "*a motorcycle* or *tricycle"*. Halafu yeye anavyopendekeza anakuja kutumbukiza *plural* hatuandiki sheria kwa namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, hata mimi naungana na Mheshimiwa John Cheyo, kwa dhana, tukisema dhana ya Bima ndiyo iwe sababu ya kukataa baiskeli siziingie, *then* tunakuwa tuna-*defeat all purposes* ya *reality on the ground*. Nadhani hilo tungeliacha, tuziache Kampuni za Bima wataona wenyewe kama *third party* ilivyo sasa hivi kuna haja ya kuongeza premium kwa sababu *accidents* zinakuwa nyingi, hilo ni la kwao. Lakini nadhani tutafute njia ambayo ni nzuri ambayo itatuvusha hapa, tujielekeze kwa marekebisho hasa yaliyopendekezwa na Serikali lakini tu-*deal* kwa ushauri wake hayo aliyosema kuhusiana na baiskeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Andrew Chenge ahsante sana. Tunaendelea kupata tija kutokana na uzoefu wako na utaalam katika Sheria. Nadhani hilo ni sahihi alilolisema kwamba isingefaa kuweka badiliko hapa 42 kunakohusika na vyombo vya moto yaani vina *engine*.

Kwa maana hiyo basi na kwa sababu tumekubaliana kwamba baiskeli zishughulikiwe na Halmashauri, yaani zile leseni za baiskeli na taratibu zinazotawala baiskeli zisimamiwe na Serikali za Mitaa, basi kuna wajibu hapo kwa Serikali kuweka hiyo *enabling clause* mahali ambapo panastahili ili Halmashauri chini ya Sheria Kuu waweze kuwa na uhalali wa kutunga hizo sheria ndogo zitakazoziwezesha baiskeli kuwa kama vyombo vya biashara. Tukishalipokea hivyo, basi nadhani *CPD* kwa taratibu zile za Kikatiba alizopewa hata kama hatuwezi kulipata mara moja sasa hivi. Nia njema hiyo ya Bunge iweze kuonekana kabla Muswada haujafikishwa kwa Mheshimiwa Rais. Ahsante. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea ushauri huo tutaufanyia kazi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2008 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill,* 2008)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria Mbalimbali wa mwaka 2008 *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill,* 2008 na imeukubali pamoja na mabadiliko yake. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na kupitishwa)*

**Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania wa Mwaka 2008**
**(*The Tanzania Trade Development Authority Bill,* 2008)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*Tanzania Trade Development Authority Act, 2008)* sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mbunge wa Jimbo la Makunduchi CCM, kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekuwa unasubiri sana kwa ajili ya kuanzisha chombo kimoja cha kusimamia na kuendeleza biashara nchini ikiwa ni njia madhubuti ya kuwezesha ufanisi katika uzalishaji wa bidhaa na huduma humu nchini na hatimaye kuunganisha uzalishaji huu na utumiaji katika masoko ya Kitaifa, Kikanda, Kimataifa kwa misingi ya nguvu ya ushindani katika soko huru.

Mheshimiwa Spika, biashara ni *engine* ya uchumi wa nchi yoyote. Hivyo, uimarishaji wa biashara kupitia mamlaka mpya ikiwa Muswada utapita ni njia ya uhakika ya kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lengo na madhumuni ya Muswada. Muswada unaowasilishwa unalenga kwa kutungwa kwa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania au *The* Tanzania *Trade Development Authority* badala ya Halmashauri ya Biashara ya Nje ambayo inakusudia kuipa mamlaka uwezo wa kuratibu na kukuza biashara ya bidhaa na huduma ndani na nje ya nchi.

Mheshimia Spika, madhumuni ni kuwa, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania iwe na uwezo wa kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Biashara. Mkakati wa kukuza mauzo nje, sera ya masoko ya Mazao na bidhaa za kilimo na mpango unganishi wa biashara ili kukuza na kuendeleza biashara ya bidhaa na huduma katika soko la ndani Kikanda na Kimataifa. Aidha, inategemewa kuwa mamlaka itakuza ufanisi wa utendaji na kupunguza gharama za uratibu na uendeshaji wa biashara na hivyo kuleta ufanisi kwa madhumuni ya kukuza biashara ya ndani na nje. Mamlaka itaanzisha vituo vya biashara ndani na nje ya nchi, itashirikiana ipasavyo na waambata wa biashara katika Balozi za Tanzania zilizopo nchi za nje. Hivyo, Muswada unaopendekeza kufuta Halmashauri ya Biashara ya Ndani, Sura 103 na Sheria ya Halmashauri Biashara ya Nje, Sura 155 ili kuwa na sheria moja kuu itakayosimamia na kuendeleza biashara.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni haya yafuatayo:-

Kwanza, wajibu na majukumu ya kiutendaji ya mamlaka yameainishwa kulingana na sera ya biashara ya Taifa, mkakati wa kukuza mauzo nje, sera ya masoko ya mazao na bidhaa za kilimo na mpango unganishi wa biashara.

Pili, kuanzisha na kuendeleza vituo vya biashara ndani na nje na kufanya tafiti mbalimbali kwa lengo la kuboresha uzalishaji na ushauri, nyenzo au taaluma za kukuza na kuendeleza maeneo huru ya uzalishaji kwa mauzo nje na bandari huru.

Tatu, kutambua uwepo wa sheria nyingine na Taasisi za ndani, Kikanda na Kimataifa zinazohusika katika kuendeleza biashara. Sheria hizo ni pamoja na zile zilizoanzisha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zenye umuhimu katika kusimamia na kuendeleza biashara ya ndani na nje na kuendana na dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi au kwa lugha ya kiingereza *Decentralization by Devolution*.

Nne, inaweka misingi ya ushirikiano kati ya Taasisi na vyombo vingine vya sekta ya umma na sekta binafsi vya ndani na nje ya nchi katika kukuza, kuendeleza na kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa bidhaa na huduma na hivyo kuweza kuhimili ushindani katika masoko ya bidhaa na huduma hizo.

Tano, kuiwezesha Mamlaka kukusanya, kuhifadhi na kusambaza taarifa za mauzo na ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani na nje.

Sita, kushiriki katika majadiliano ya biashara na uwekezaji ya Kikanda kama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na ya Kimataifa hususan Shirika la Biashara la Dunia (*WTO*).

Saba, Muswada unaongeza na kuainisha makosa mbalimbali ya biashara kwa kuzingatia misingi ya sheria, kanuni za utawala bora na mwenendo unaokubalika Kimataifa na adhabu zitakazotolewa kwa ukiukwaji wa sheria hii.

Nane, kuipa mamlaka, uwezo wa kuratibu na kukuza biashara ya ndani na nje ili kuleta ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara.

Tisa, kumpa Waziri mwenye dhamana uwezo wa kutengeneza kanuni pale itakapofaa ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Muswada umegawanyika katika sehemu kuu nne zifuatazo:-

Sehemu ya kwanza ya Muswada yenye Ibara ya (1) mpaka ya (3), inapendekeza maelezo ya awali yaani jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika na walengwa wa sheria hii.

Sehemu ya pili ya Muswada yenye Ibara ya (4) mpaka 11 inapendekeza kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania itakayokuwa na watumishi kuanzia Mkurugenzi Mkuu, Wakurugenzi na watumishi wengine kama watakavyoteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi ili kumsaidia Mkurugenzi Mkuu katika utekelezaji wa majukumu wa Mamlaka. Pia inaainisha majukumu ya mamlaka, uanzishwaji wa Bodi ya Wakurugenzi na majukumu na mamlaka ya Bodi ya Wakurugenzi, uteuzi na majukumu ya Mkurugenzi Mkuu. Mamlaka inayoanzishwa itakuwa chombo huru katika kutekeleza majukumu yake kwa maana ya kutoingiliwa kiutendaji na chombo kingine au mamlaka yoyote wakati inatekeleza jukumu la kukuza uzalishaji na kuendeleza biashara.

Sehemu ya tatu, ambayo ni ya Ibara ya 12 mpaka 20 inaainisha vyanzo mbalimbali vya mapato ya mamlaka, mwaka wa fedha pamoja na utaratibu wa mamlaka kukopa. Aidha, wajibu wa mamlaka wa kutengeneza na kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi na kuwasilisha hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kulingana na Sheria inayosimamia fedha za umma kwa Waziri mwenye dhamana. Ni muhimu katika sehemu hii na ni jukumu la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa utendaji kazi wa Mamlaka.

Vilevile inaipa Bodi ya Wakurugenzi uwezo wa kuwapa watumishi wanaostaafu na waliopo kazini marupurupu mbalimbali ikiwemo Bima ya Afya na inatamka mali na madeni ya Mamlaka kulingana na Sheria hii.

Sehemu ya nne, ambayo ni Ibara ya 21 mpaka 29 inapendekeza masuala ya jumla ikiwa ni pamoja na uwezo wa Waziri wa kutoa maelekezo kwa maandishi yanayohusu utendaji kazi wa Mamlaka na kutengeneza na kurekebisha kanuni na kurekebisha jedwali la sheria na kukataza utoaji wa taarifa za Mamlaka kwa mtu au chombo kingine.

Pia Halmashauri za Wilaya na Mamlaka nyingine za Serikali za Mitaa zipewe uwezo wa kutengeneza sheria ndogo ndogo kwa ajili ya utekelezaji kamilifu wa sheria hii. Aidha, masuala mengine ni kinga dhidi ya mashtaka kwa Waziri mwenye dhamana, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi na watumishi wa Mamlaka wakati wa utekelezaji halali wa sheria hii. Utaratibu wa malipo ya posho kwa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi na matangazo ya amri, maelekezo na mashauri mengine. Aidha, umuhimu wa sehemu hii upo kwenye mapendekezo ya kufutwa kwa Sheria ya Halmashauri ya Biashara ya Ndani, Sura 103 na Sheria ya Halmashauri ya Biashara ya Nje, Sura 155 na masuala ya mpito.

Utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa utasaidia kukuza uzalishaji wa bidhaa na huduma hivyo kuwa kichocheo cha biashara katika soko la ndani ambao utasimamiwa, kuendelezwa na kuratibiwa ipasavyo kinyume na hali ilivyo sasa na hivyo kuwa kiungo cha biashara katika masoko ya nje Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko ahsante sana. Sasa nitamwita Mwenyekiti au mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, anakuja Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007 ili niweze kutoa maoni kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania wa mwaka 2008 "*The Tanzania Trade Development Authority Bill*, 2008" (*TANTRADE*).

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya hivyo, naomba unipe fursa hii nitoe salamu zangu za kheri kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupita salama mwaka 2008 na kuendelea salama.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wengine kwa misiba mbalimbali iliyotokea. Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira kwa misiba hiyo na awajalie marehemu wakae mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, tatu, ningependa kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mkinga kwa Mbunge wetu aliyechaguliwa wa Mbeya Vijijini pamoja na CCM kwa ushindi wa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijadili Muswada huu katika Ukumbi wa Ofisi ndogo ya Bunge iliyopo Dar-es-Salaam tarehe 19-20 Januari 2009. Katika vikao vyake, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu mapendekezo yaliyokusudiwa katika Muswada huu yaliyowasilishwa na Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, wakiwepo pia wawakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kuupitia Muswada huu, Kamati iliwaalika wadau mbalimbali na hivyo kuwapa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao kwa nia ya kuuboresha. Majadiliano hayo yalisaidia sana kuibua mawazo mapya, maoni na kufikia muafaka. Maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu ni matokeo ya mchakato huo wa kubadilishana mawazo na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao waliitikia mwaliko wa Kamati wa kuja kutoa maoni yao kwa lengo la kuboresha Muswada ulio mbele yetu hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Muswada huu kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Abdisalaam I. Khatib, Mwenyekiti; Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Mohammed A. Chomboh, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Ame P. Ame, Mheshimiwa Rostam Azizi, Mheshimiwa Vuai A. Khamis, Mheshimiwa Parmukh S. Hoogan, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Haji J. Sereweji, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Abdallah S. Sumry.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Naibu Waziri Dkt. Cyril Chami na Katibu Mkuu wa Wizara Bibi Joyce Mapunjo, kwa maandalizi na uwasilishaji mzuri wa Muswada kwa Kamati ikiwa ni pamoja na ushirikiano mzuri waliouonesha. Matokeo yake ni Muswada ulioboreshwa kwa mawazo ya wengi, hivyo ubora wake unajionyesha wenyewe bayana.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu una madhumuni ya kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara badala ya Halmashauri ya Biashara ya Nje. Madhumuni ya Muswada huu pia ni kuipa Mamlaka itakayoanzishwa kwa mujibu wa sheria hii uwezo

wa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Biashara na Mkakati wa Kukuza Mauzo nje pamoja na Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo ili kukuza na kuendeleza Biashara ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu, hasa baada ya iliyokuwa Halmashauri ya Biashara ya Ndani kuvunjwa; hakukuwa na Taasisi inayosimamia na kushughulikia biashara ya ndani. Hata kwa Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*), ilikuwa ni vigumu kuingilia eneo hili kwani kisheria yenyewe ilikuwa inahusika na usimamizi wa biashara ya nje. Kutokana na hali hii na ili kuinua viwango vya biashara ya ndani na nje, Kamati yangu inaunga mkono uletwaji wa Muswada huu kwa lengo la kufanya mabadiliko yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati imeridhika kuwa Muswada huu ukipitishwa, utasaidia sana kukuza na kuratibu biashara ya ndani na nje ya nchi na hivyo kuwanufaisha wafanyabiashara wa ndani na wa nje kwa njia ya kuwapatia taarifa za masoko na pia kuwasimamia katika kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua umuhimu wa kuanzishwa kwa Mamlaka hii ya Maendeleo ya Biashara, Kamati yangu ilikuwa inashauri kwamba, liwepo Bazara huru litakalokuwa na uwakilishi mpana zaidi kutoka sekta mbalimbali kwa mfano, Biashara, Viwanda, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Taasisi za viwango, Taasisi za Utafiti na kadhalika ili Baraza hili liweze kutoa ushauri kwa Mamlaka hii ipasavyo na ikiwezekana Baraza hili litambuliwe katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika pamoja na malengo mazuri ya Muswada huu, bado haujakidhi namna wajasiriamali watakavyosaidiwa. Kamati ina wasiwasi kwamba pengine mafanikio yake hayataonekana kama wadau ikiwa ni pamoja na namna wajasiriamali na wenye viwanda vidogo vidogo hawataelimishwa vizuri na kusaidiwa kuhusu masuala yahusuyo biashara ya ndani na nje kwani kuna vigezo vinavyotumika hivi sasa ili uweze kuuza nje ya nchi. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kuwaelimisha na kuwasaidia wajasiriamali na wananchi wenye viwanda vidogovidogo ili nao hatimaye waweze kufikia vigezo stahiki na hivyo kuuza bidhaa zao nje ya nchi na kwa maana hiyo kuliongezea Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuushukuru uongozi wa Wizara kwa kukubali baadhi ya ushauri wa Kamati moja kwa moja wakati wa mchakato wa kuchambua na kujadili Muswada huu kwenye Kamati. Hata hivyo, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo kwa baadhi ya vifungu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5(e) kinamtaka mfanyabiashara yeyote au Taasisi kupata kibali kwa Mamlaka hii kabla ya kupeleka bidhaa zake kwa ajili ya maonesho nje ya nchi, lakini Muswada huu haujaweka wazi adhabu atakayopewa mtu au taasisi itakayokaidi kifungu hiki. Aidha, Muswada huu haujabainisha iwapo mtu huyo au taasisi itakayofanyiwa hila na Mamlaka ishtaki wapi na kwa muda gani (*appealing)*. Hivyo, Kamati inashauri kwamba mambo haya yawe wazi katika sheria hii inayokusudiwa

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5 kinazungumzia kazi za Mamlaka hii, na kifungu cha 5(h), kinasomeka "*establish and maintain databases*" kama moja ya kazi hizo. Kamati inapendekeza kwamba, liongezwe neno "*trade"* yaani iwe *trade bases* baina ya neno "*maintain*" na "*databases*" ili kukipa kifungu hiki maana sahihi. Aidha,

Kamati imebaini kwamba kazi za ufuatiliaji (*Monitoring and Evaluation)* maendeleo ya biashara (*Trade Performance*) na pia tafiti za masoko (*Marketing Research*) hazijaorodheshwa katika kifungu cha 5 kama moja ya kazi za mamlaka; hivyo Kamati inashauri kazi hizi zijitokeze kwa kuongezwa kifungu "p" au kuingizwa kazi hizo kwenye vifungu muafaka.

Mheshimiwa Spika, kifungu 10(3) kinatamka kuwa Bodi ya Mamlaka yaweza kukasimu na/au kumuondolea mtumishi madaraka hayo kutokana na nguvu ilizopewa Mamlaka. Kwa kuwa aliyekasimiwa madaraka (*delegated)* huenda akawa ameshaingia gharama, Kamati inashauri kwamba, ni vyema kifungu hiki pia kitamke gharama hizo zitafidiwa namna gani.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21 kinatamka kuwa Waziri anaweza kutoa maelekezo *(directives*) kwa Bodi. Lakini kifungu hiki hakiweki wazi kama maelekezo hayo yatakuwa kwa njia ya mdomo au maandishi. Kamati yangu inapendekeza kwamba, liwepo neno "*in writing*" baada ya neno "*directions*" ili maelekezo hayo yaweze kutolewa kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24 kinazungumzia sheria ndogo baada ya kuwasiliana na Mawaziri wa pande mbili za Muungano. Kamati inashauri kwamba, kifungu hiki kirekebishwe badala ya mawasiliano …"*subject to consultation with the Minister"* ... maamuzi yafanyike katika vikao vyao vya pamoja. Hii itasaidia kuokoa muda kwa kutungwa kwa sheria hizo ndogo kuakisi sheria hii ya Mamlaka inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Jedwali (*Schedule)* inayozungumzia Wajumbe wa Bodi, Kamati inapendekeza aongezwe mwakilishi mwenye sifa zinazostahili kutoka Viwanda Vidogovidogo (SMEs). Aidha, Kamati ilionelea ni vema Wajumbe wote watakaoteuliwa katika Bodi wawe na sifa zinazoendana na majukumu ya Mamlaka hii ya Maendeleo ya Biashara ili kuleta ufanisi. Hii itasaidia kuzuia uteuzi wa wajumbe kiholela bila kufuata misingi bora ya kiutendaji. Kamati inashauri Mwenyekiti wa Bodi afahamu au aelimishwe majukumu yake ili kuepuka migongano na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka kama ilivyokwisha tokea kwa baadhi ya Bodi na pia ni vyema Mwenyekiti akawa na mawasiliano ya mara kwa mara na Katibu wake ili kuepusha migongano hiyo. Aidha, katika uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka, Kamati inashauri jinsia izingatiwe na kifungu kitamke hivyo bayana.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine niwashukuru tena Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Katibu Mkuu wa Wizara, Bibi Joyce Mapunjo pamoja na watendaji wote wa Wizara walioshiriki kuandaa na kuuboresha Muswada huu ikiwa ni pamoja na ushirikiano waliouonyesha kwa Kamati wakati wote wa kuujadili.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nirudie kuwashukuru na kuwapongeza wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao ambayo yametusaidia sana. Aidha, naomba kuwapongeza Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Viwanda na Biashara kwa michango yao mizuri na makini ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia sana kuboresha Muswada huu.

Nimalizie kwa kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashilillah kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo na Makatibu wa Kamati, Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Angelina Sanga kwa kuihudumia Kamati vizuri kwa wakati wote. Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwandoro. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko anatuwakilisha kule Uswiss Darvors kwenye Mkutano wa masuala ya fedha na uchumi na anatakiwa aondoke leo kuelekea huko. Ameniandikia barua nimeridhika na sababu hiyo. Kwa hiyo mtakapokuwa mnaona mtoa hoja hayupo ni kwa ridhaa ya Mheshimiwa Spika na nimearifiwa naye na kuhakikishiwa kwamba Naibu Waziri atashughulikia masuala yote kwa ukamilifu, tusiwe na wasi wasi wowote. Kwa hiyo sasa nitamwita Waziri Kivuli Mheshimiwa Lucy Owenya.

**MHE. LUCY F. OWENYA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na nguvu za kuweza kusimama hapa mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara wa Mwaka 2008 *(The Tanzania Trade Development Authority Act, 2008).* Kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 86(6) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri Dr. Cyril Chami (MB), Katibu Mkuu wa Wizara Bi Joyce Mapunjo pamoja na timu nzima ya watendaji kwa kazi waliyoifanya na kuleta Muswada huu muhimu. Ni matumaini ya Kambi ya Upinzani kuwa, Muswada huu unaweza ukaleta changamoto katika biashara za ndani na nje, jambo ambalo litaleta tija kwa Watanzania na Tanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5(2)(a) kinachosomeka kuwa, nanukuu: *"Give advice to the government, any person, organization or Institution…………."*

Kambi ya Upinzani inataka ufafanuzi kuhusiana na utolewaji wa ushauri wa uendeshaji mzuri wa biashara kama ni bure au kuna gharama zitakazokuwa zinaambatana na ushauri huo wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7(2)(d) kinasomeka kama ifuatavyo ninanukuu: "*On behalf of the Authority, receive gifts, fees, donations, grants or other moneys*", mwisho wa kunukuu. Mamlaka hii inayoundwa itakuwa inashughulika moja kwa moja na watu binafsi, Makampuni pamoja na biashara zao. Ni ukweli uliowazi kuwa pindi sheria inapoweka mwanya wa kupokea zawadi kwa chombo chenye maamuzi maana yake ni kukaribisha kutoa upendeleo kwa baadhi ya watu au makampuni. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuondoa maneno hayo ya "*receive gifts*" kwani yanaweza kupelekea rushwa katika utendaji wa Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7(2)(e) kinachoipa mamlaka Bodi kufanya uteuzi wa watumishi wa mamlaka kwa kadri itakavyoona inafaa. Kambi ya Upinzani inaona kifungu kinakandamiza uhuru wa utawala bora kwenye kipengele kinachotoa ushindani huru kwa wale wote wenye sifa zinazohitajika kwa kazi. Aidha kifungu hicho kinatoa mwanya wa upendeleo katika ajira na uchafu mwingine unaoweza kusababisha malalamiko toka katika jamii. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inashauri, kwa kuwa Mamlaka ni mojawapo ya asasi zitakazokuwa ni mali ya Serikali hivyo basi taratibu na kanuni za ajira kwa watumishi wa Serikali zifuatwe.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 8(1) kinachosema kuwa Rais ndiye atakayemteua Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka. Kambi ya Upinzani inatoa ushauri kama ule ambao imeutoa wakati tukiwasilisha maoni ya Muswada wa Sheria ya Viwango, kuwa nafasi hii itangazwe na ishindaniwe na wote wenye sifa na vigezo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9 kinachosema nanukuu "*The Board of Directors may appoint on such terms and conditions and upon such salaries as it may find appropriate, such officers and employee for proper and efficient conduct of the operations and activities of the Authority*". Kambi ya Upinzani inaona kuwa watumishi wote wanaotoa huduma kwa wananchi umuhimu wao ni sawa, hivyo basi kitendo cha kutoa upendeleo kimaslahi kwa baadhi ya watumishi kulingana na pahala wanapotolea huduma ni makosa na kunasababisha watumishi wa sehemu nyingine kuonekana hawathaminiwi na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kambi inashauri kuwa kinachotakiwa ni kurekebisha viwango vya mishahara (*salary scales*) kulingana na taaluma na uzoefu wa mtumishi ili kuongeza motisha ya utendaji wa watumishi na si kwa Bodi kutoa mishahara kulingana na wao wanavyoona. Tofauti na hapo hii inaleta dhana kuwa ajira katika Mamlaka ni maalum kwa kada fulani ya Watanzania na si kwa Watanzania wote wanaokidhi sifa na vigezo vinavyotangazwa kwenye magazeti kwa ajili ya ajira.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyatoa maoni hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha, ahsanteni kwa kunisikiliza. (*Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Owenya kwa maoni hayo kuhusu Muswada ulio mbele yetu. Waheshimiwa Wabunge katika orodha yangu nimekwishapokea sasa wachangiaji 4, Waheshimiwa Wabunge 4 walioomba kuchangia Muswada huu nitawatamka kwa mpangilio kama ifuatavyo: Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Herbert James Mntangi. Simuoni kwa sasa hivi Mheshimiwa Zitto kwa hiyo nadhani nitamtanguliza Mheshimiwa Kaboyonga kama yuko tayari, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Anna Lupembe. Kutarajia muda mara nyingi Miswada kama hii watu waongee kwa kirefu sana lakini kama muda utakuwa umekwisha tutaendelea jioni.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya mwanzo kuchangia Muswada ulio mbele yetu wa kuunda Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania. Kama ambavyo maudhui ya Muswada huu

yalivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri nianze kwa kuunga mkono hatua ya kuiunda Mamlaka hii. Hususan kwa sababu nchi yetu sasa hivi uchumi wake mkubwa tuseme sio sahihi siku zote Tanzania uchumi wake wa ndani unaungana na uchumi wa kidunia kwa maana ya kwamba tunachozalisha hapa nyumbani na hususan kile ambacho ni ziada ni vizuri kikauzwa nchi za nje.

Kutokana na ukweli huo ni kwamba kama nchi tunahitaji kuzalisha fedha za kigeni kwa kutumia ziada ya mazao yetu ya viwandani na mashambani kwa kuuza nje ili tuweze kupata fedha za kigeni za kununulia bidhaa mbalimbali kutoka nje ambazo hatuzitengenezi hapa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo uundwaji wa chombo hiki umekuja wakati muafaka hususan kwa sababu sasa tunaunganisha nguvu za biashara zote mbili kwa pamoja biashara ya ndani na biashara ya nje. Kwa hiyo, chombo hiki kitakuwa na mamlaka ya kuitazama biashara ya nchi kwa ujumla wake na hasa tukizingatia kwamba nchi nyingi zilizoendelea na zinazoendelea katika eneo la kukuza biashara ya nje zinafanya hivyo kwanza kwa kuhakikisha kwamba zinakuza biashara ya nje kutokana na uzalishaji wa biashara ya ndani. Kwa maneno mengine ni kwamba biashara ya nje inakuwa ni *extension* yaani upanuzi wa biashara ya ndani.

Mheshimiwa Spika, ili kuainisha mambo haya mawili tufike mahali tuweze kuona ni jinsi gani tutaiondoa nchi yetu katika hali ya sasa ambayo kwa kiasi kikubwa tunazalisha tusichotumia na tunatumia tusichozalisha. Kwa hiyo chombo hiki kiratibu sehemu hizi mbili za biashara yetu ya ndani na ya nje hususan kuhakikisha kwamba biashara ya nje iwe ni kiendelezo cha biashara ya ndani kutokana na uzalishaji wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa miongoni mwa mambo ambayo ningeshauri yapatiwe nafasi ya kipekee katika majukumu ya chombo hiki iwe ni pamoja na uzalishaji. Kwa sababu tatizo letu kama nchi sasa hivi si masoko peke yake, masoko ya nje kama tunavyofahamu kwa bidhaa nyingi yapo, nichukue mfano tu wa zao moja ambalo linatoka katika Jimbo na Mkoa ninaouwakilisha, Jimbo la Tabora na Wilaya zake kwa maana ya Urambo, Sikonge, Igunga, Nzega na kadhalika.

Kule tunazalisha zao moja la asali pamoja na mengine. Lakini asali hii haifahamiki sana katika masoko ya dunia na wananchi wanapata taabu ya kuelewa hii asali waipeleke wapi na kwa bei gani ambayo ni nzuri na kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiwa na chombo kama hiki matarajio yangu ni kwamba chombo hiki kitawasaidia hawa warina asali kuwaunganisha. Kwanza kuwaelekeza namna nzuri ya kufuga nyuki vizuri na kurina asali katika utaratibu mzuri unaolingana na mahitaji ya soko la kidunia. Jambo hili linaendana na bidhaa takriban zote ambazo nchi yetu inazizalisha na kwa maana hiyo kuziuza ndani na nje. Kwa hiyo tutakapokuwa na chombo kama hiki na kwa sababu chombo hiki kitaungana na vyombo vingine ambavyo vipo na vimeundwa kisheria kuangalia masuala mazima ya biashara kwa maana ya viwango, *quality* na *standards* chombo hiki kitaungana na vyombo hivyo ili

kuwaelimisha wananchi katika maeneo mbalimbali ya bidhaa zetu ambazo tumezizalisha. Kwa hiyo chombo kinakuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, vile vile ni kwamba chombo hiki kimepewa jukumu pamoja na mengine kuunganisha nguvu za wazalishaji wote na wauzaji wote wa bidhaa za nchi hii kupitia utaratibu wa Maonyesho ya Biashara. Sasa hapa linakuja suala la aina gani ya Maonyesho ya Biashara tunayafanya na tunayafanyia wapi? Mpaka sasa hivi nchi yetu ina Maonyesho makubwa ya Sabasaba ambayo yanafanyikia Dar es Salaam katika barabara ya Kilwa. Kama ambavyo wengi wetu tunavyofahamu uwanja ule uwakutanisha wafanyabiashara na wazalishaji kutoka sehemu mbalimbali za dunia ili kukutana na kubadilishana mawazo kuhusu nini wanaweza kununua kutoka Tanzania wale wanaotaka kuja kununua na nini Tanzania inaweza kuuza nje ya Tanzania kwa wale ambao wanaweza kuuza.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa ambalo nilitaka kulisisitiza hapa kwamba uwanja wetu wa Maonyesho wa Dar es Salaam unahitaji kuboreshwa sana kufikia ngazi za Kimataifa kwa maana ya Maonyesho ya Kitaifa. Bado Maonyesho yale huwa na vurugu zaidi na huwa kama ni mahali pa kukutana watu wanaokwenda kusikiliza muziki zaidi na pengine burudani hususan za masuala ya vinywaji vikali.

Sasa ukishapafanya mahali pa biashara kuwa ni mahali pa burudani hasa muziki na vinywaji vikali unafika mahali hali inakuwa ni ya vurugu zaidi kuliko hata kufanya biashara.

Kwa hiyo matarajio yangu ni kwamba chombo hiki kitatusaidia kurekebisha hali hiyo ya vurugu zaidi.

Mheshimiwa Spika, nisisitize kwamba suala zima la kukuza biashara ya Tanzania ni lazima liende sambamba na kukuza uzalishaji. Kwa hiyo, eneo la uzalishaji liwekewe mkazo wa kipekee na hiyo ni sehemu ya majukumu ya hii Mamlaka.

Nina *Bill Supplement* ya tarehe 17 Oktoba, 2008 sina uhakika kama ndiyo hiyo tunaendelea kuijadili au imeshabadilika, lakini kama hivyo ndivyo nikienda kwenye ukurasa wa 13 kwenye *schedule*. Katika *schedule* ile inasema "*made under section* 6 (2)". Pale inaelezwa utaratibu mzima wa kuipata *Board of Directors*.

Nikitazama hivyo ndivyo ilivyo kama haitobadilika basi Bodi hii itakuwa ni ya watumishi zaidi wa Serikali kutoka Wizara zinazoonyeshwa hapo kuliko wafanyabiashara na wazalishaji.

Kwa hiyo, nataka niungane na Kamati iliyochambua Muswada huu kwa kusema kwamba kama hii *schedule* bado ipo kama ilivyo na kwa kuwa itakuwa ni sehemu ya sheria ambayo tunaipitisha leo nilikuwa naomba ifanyiwe mabadiliko kwa kuondoa Watumishi wa Serikali zaidi kama inavyoonekana hapa na badala yake waingizwe watu au Watanzania ambao wana sifa za biashara, mambo ya fedha, mambo ya sheria, mambo ya viwanda kuliko mfumo huu kama ulivyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hakika itakuwa sikumtendea haki mchangiaji anayefuata kwa sababu siwezi kumkadiria ila haki yake ni dakika 15. Sasa nikisema ajaribu au tumkatize halafu arejee tena saa 11.00 bora hilo tuliweke kiporo hadi saa 11.00 jioni. Kwa hiyo nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.52 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na awamu ya uchangiaji wa Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania wa Mwaka 2008 *(The Tanzania Trade Development Authority Bill, 2008*). Wachangiaji nilionao ni wanne; Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Herbert Mntangi na Mheshimiwa Basil Mramba. Moja kwa moja tuanze na Mheshimiwa Kabwe Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Muswada huu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara na ni Muswada muhimu sana. Kabla sijaanza kuchangia mchango wangu mfupi, nami pia ningependa kutoa salamu za mwaka mpya, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia kwa mwaka huu wa 2009. Vilevile napenda kutoa pole kwa watu wote ambao walifiwa, ikiwemo familia ya Marehemu Nyaulawa.

Napenda kutambua uamuzi wa Wananchi wa Mbeya Vijijini wa kumchagua Mchungaji Mwanjale, ingawa watu waliomchagua ni wachache sana, 33% tu ya wapiga kura waliojitokeza kati ya 35% waliojitokeza. Kwa hiyo, nadhani ni vitu vya kuangalia sana katika chaguzi na tume inapofanya maamuzi kuhusiana na wagombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, Muswada huu ni muhimu sana na nadhani ni Muswada ambao umechelewa, kwa sababu kwa muda mrefu sana Mamlaka ya Biashara ya Ndani ilikuwa ni kama haipo, kwa sababu mashirika yote yanahusiana na Mamlaka ya Biashara ya Ndani kama RTC, BHESCO na kadhalika, yalibinafsishwa, mengine yalifilisiwa na mengine yalikufa tu yenyewe. Kwa hiyo, mfumo wa biashara ya ndani haukuwa unaratibiwa. Sasa Muswada huu unajaribu kuhakikisha kwamba, yale ambayo yalikuwa yanafanywa na *Board of Internal Trade,* ambayo ilikuwa imekufa, sasa yatafanywa na Mamlaka na itaweza kusaidia kuweza kufanya wanachokiita *integration* ya *markets* za ndani.

Tuna tatizo kubwa sana katika uchumi wetu, bado uchumi haujawa *well integrated;* ndiyo maana ni rahisi sana kusikia kuna mahindi yanaoza Rukwa wakati kuna njaa Mwanza au kuna maharage ambayo hayana soko Kasulu lakini kuna njaa Dodoma au Morogoro na kadhalika. Hii ni kwa sababu ya kutokuwepo kwa mfumo mzima wa habari, kuhusiana na masoko ya ndani. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba, kwa mujibu wa zile kazi ambazo nimeziona kwenye Mamlaka, kazi hii itaweza kufanywa kwa ufanisi.

Jambo moja tu ambalo ningependa kupata maelezo ya ziada *(clarification),* kutoka kwa Waziri wa Wizara hii ni kuhusiana na Muswada huu kutumika pande zote mbili za Muungano; Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Suala la biashara ya nje ambayo ni sehemu ya mamlaka ni suala la Muungano, halina tatizo lipo kwenye Katiba na Sheria inasema kwamba, itatumika Zanzibar katika hili. Kwa suala la biashara ya ndani, hili ni suala la ndani kila sehemu ya Muungano.

Muswada umetamka kwamba, unatumika pande zote mbili na hata uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka unaonyesha kwamba, kutakuwa na *consultation* kati ya Waziri anayehusika na biashara kwa Zanzibar na Waziri anayehusika na biashara wa Muungano. Sasa hili naona ni tatizo, inabidi kuliangalia kwa sababu biashara ya ndani sio jambo la Muungano; Muswada unatambua kutumika pande zote mbili kwenye *application* ya Muswada. Kwa hiyo, ningependa kupata maelezo; ni jinsi gani ambavyo hatutaweza kuvunja Katiba kuhusiana na eneo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa sana la biashara ya nje. Hivi sasa tafiti mbalimbali zinaonyesha kwamba, tuna tatizo kubwa sana la *balance of trade,* kwa sababu tunaagiza zaidi bidhaa kuliko tunavyouza. Vilevile tuna tatizo kubwa sana la kwamba, tunayoyauza yapo *dominated* na *primary products* kwa upande wa *traditional export.* Vilevile tuna tatizo kwamba, tuna *import* sana bidhaa za viwandani kutoka nje. Hii inaonyesha kwamba, tunauza *primary products*, tuna *import machineries,* kitu ambacho utaratibu wetu wa viwanda vya ndani kwa ajili ya uzalishaji wa ndani bado ni mdogo kuweza kuzuia hizo *imports*.

Mchana huu nilikuwa najaribu kuangalia Taarifa ya Benki Kuu, kuhusiana na urari wetu wa biashara, inayoishia mwezi Disemba, 2009 inaonekana kwamba, urari wa biashara umeongezeka sana. Ingawa kuna *improvement* katika eneo la uuzaji nje *manufactured goods, especially plastic items,* ngano, chuma na *steel items*. Sasa kwa ngano, tunaona juhudi ambazo zinafanywa na kampuni binafsi kama Kampuni ya Bakhresa na kadhalika, kwenye kuuza ngano katika nchi za Congo, Rwanda na kadhalika, kitu ambacho itabidi Mamlaka itoe *support* ya kutosha sana kwa Watanzania kama hawa.

Kwa upande wa *iron and steel items,* inawezekana kabisa ni tatizo ambalo linalalamikiwa kila siku kuhusiana na uuzaji wa chuma chakavu. Sababu tume-*double* uuzaji wa bidhaa nje, lakini imechangiwa kwa kiasi kikubwa na uuzaji wa vitu kama hivi, lazima ziangaliwe. Kitu ambacho kinanifanya nimwombe Waziri akiangalie na hasa mamlaka itakapokuwa imeanzishwa iweze kukiangalia, inaonyesha sasa hivi juhudi za nchi kuuza nchi jirani kama Burundi, Rwanda, Congo, Kenya na Uganda zimeongezeka.

Juhudi hizi zinapaswa kuongezeka sana, kwa sababu uuzaji katika nchi hizi za jirani za kiafrika, hauna vikwazo vingi kama uuzaji kwenye nchi za mbali kama Ulaya na Marekani. Kwa hiyo, naomba Mamlaka itakayoanzishwa itoe kipaumbele kikubwa kwenye *Regional Trade*, kwa sababu inaonyesha kwamba, *Regional Trade* inaweza ikatuongezea sana na kupunguza urari hasa uliopo wa biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine.

Suala zima la tunauza nini nje ni tatizo ambalo inabidi liangaliwe kwa undani sana. Sasa hivi kwa kiasi kikubwa, mauzo yetu ya nje zaidi ya asilimia 39 yanachangiwa sana na dhahabu peke yake, ukichanganya na madini mengine yanafikia kama asilimia 44. Mwaka 2008 tuna rekodi mbaya sana ya uuzaji nje korosho; pamba imeongezeka sana na kahawa imeshuka kidogo. Nadhani mamlaka itabidi ifanye kazi ya ziada ya kuhakikisha kwamba, utekelezaji wa Sera yetu ya Biashara, unaangalia sana mauzo nje ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunapunguza urari wa biashara na tunapata fedha za kigeni za kutosha, ziweze kusaidia katika maendeleo ya uchumi wa taifa letu.

Katika hili pia, nizungumzie nini jukumu hasa la Mamlaka. Mwaka 2003, Serikali ilitunga Sera ya Biashara; nilipokuwa naangalia kazi za Mamlaka ambayo tunaiunda leo, sijaona kitu ambacho kimetamkwa wazi wazi kuhusiana na utekelezaji wa sera hii, ambapo mimi nilikuwa nadhani kwamba, Mamlaka ingekuwa wazi kabisa bila kufinyangwa na maneno mengine. Mamlaka iwe ndio chombo cha utekelezaji wa Sera ya Biashara. Hii itasaidia sana kuipa Mamlaka uwezo ku-*implement* ile *Trade Policy* yetu, kwa maana ya *Internal Trade* na *External Trade*.

La pili, Tanzania tuna tatizo kubwa sana la *marketing intelligence,* hatujui ni bidhaa zipi na wakati gani zinatakiwa wapi. Tulikuwa na *Board of External Trade*, imejitahidi kufanya jinsi ambavyo imeweza kufanya, lakini tunahitaji sana hivi vinavyoitwa Vituo vya Biashara Nje, ambavyo Mamlaka imepewa kazi ya kuvianzisha na kuviendeleza. Kimsingi, tunapaswa kuwa na *unit* fulani ya *marketing intelligence* ili iweze kuelezea *South Africa* kuna nini, wanataka nini kutoka Tanzania; Congo kuna nini wanataka nini kutoka Tanzania; Burundi kuna nini wanataka nini kutoka Tanzania. Sasa hii sijaiona vizuri kwenye zile kazi za Mamlaka ambayo tunaianzisha.

Kazi nyingi sana zimeorodheshwa, lakini kuna kazi ambazo zinapaswa kuonekana wazi. Lingine ambalo ningependa kuliona wazi ni kuhusiana na suala la nani sasa anakuwa na mamlaka ya kuongoza mazungumzo ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi nyingine, kama ni *multilateral* kati ya Tanzania na nchi nyingine, kama ni *multilateral trade negotiation.*

Sasa hivi tunaenda kwenye negotiation nyingi sana; tuna *negotiate Common Market* Afrika Mashariki, tuna-*negotiate Free Trade Area* imeshakuwa *negotiated*, lakini tunaenda katika *Custom Union* ya *SADC*. Tunajadiliana *EPA*, tupo kwenye mazungumzo yasiyoisha ya *WTO* na DOHA round, lakini Mamlaka haijaonyeshwa wazi kwamba, ndiyo itakayokuwa Wakala wa Serikali kuhusu majadiliano ya nje.

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba, hili nalo Mheshimiwa Waziri, ungeweza kuliangalia liweze ku-appear kwenye kazi za Mamlaka, kwa sababu itakuwa ni chombo ambacho kina uwezo wa kutosha wa kuweza ku-*implement Trade Policy* ya nchi, kwa maana ya *foreign* na *internal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimefurahishwa sana na *innovation* ya jinsi gani ambavyo Wajumbe wa Bodi watakuwa wanapatikana kwenye mamlaka hii. Kumekuwa na malalamiko mengi sana, kuhusiana na Mawaziri wanateua watu gani kwenye Bodi za Mashirika ya Umma na ni tatizo kubwa sana. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, tunakutana nalo, unashangaa Bodi hii inahitaji watu wenye uwezo fulani, lakini unakuta Waziri ameteua mtu ambaye wala hajui nini kinachoendelea. Uzuri wa Sheria hii, imeweza kuweka watu wanatoka wapi, kwa hiyo, inawabana Mawaziri juu ya aina ya watu ambao wanawateua.

Nilikuwa naomba Waziri atakapokuwa anafanya uteuzi, aangalie ni jinsi gani ambavyo anaendana na Sheria inavyopendekeza, lakini pia na Sheria nyingine zitakazokuja kwa ajli ya mabadiliko mbalimbali ya vitu ambavyo tunaviunda, ijaribu kuiga kutokana na hiki ambacho kimeonyeshwa katika Muswada huu wa kuanzisha TanTrade.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo ambayo nilikuwa nimepanga kuyazungumza na yale ambayo nitakuwa nahitaji maelezo, nadhani Mheshimiwa Waziri, ataweza kuyatolea maelezo kwenye majumuisho. Nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, niweze kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba nitoe heri ya mwaka mpya, kwa Wabunge wenzangu wote, pamoja na wewe mwenyewe Mwenyekiti.

Ninaomba nitoe pole kwa wote waliopata matatizo mbalimbali. Vilevile natoa pole kwa aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Nyaulawa.

Nachukua nafasi hii kumpongeza Mbunge aliyefika siku ya leo, kwa kupata kura nyingi sana kwenye uchaguzi uliofanyika Mbeya Vijijini. Nakipongeza sana Chama cha Mapinduzi, kwa kupata ushindi Mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Waziri, kwa uamuzi mzuri wa kutuletea Muswada mzuri, ambao utawaimarisha wajasiriamali wenzetu ambao wanajishughulisha na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba kusema kuwa, Muswada huu utawapa fursa wajasiriamali wadogo wadogo. Mpaka hivi sasa tuna Uwanja wa Sabasaba, ambao unachukua wajasiriamali wakubwa na wadogo wadogo. Ukiangalia kwa undani zaidi, uwanja huu unafanya kazi kwa mwaka mara moja, yaani wakati wa

Sikukuu ya Sabasaba tu.  Wajasiriamali wengi wanatamani kuja katika uwanja huu, ili waweze kuleta vitu vyao ambavyo wanavyovitengeneza na ukizingatia wajasiriamali wetu hata vijijini wanaweza kutengeneza *wine*, sabuni na vitu vingi tu vidogo vidogo. Wanakausha mboga za majani hawajui wapeleke wapi, lakini kwa Muswada huu Mamlaka hii inaweza ikawakomboa wajasiriamali mbalimbali.

TAMISEMI nayo vilevile ikiweka ushirikiano mkubwa, kwa kuwa ndiyo ina Halmashauri ambazo zipo katika Mawilaya yetu na Mikoa yetu na ndizo zinazojua wajasiriamali wengi; Halmashauri hizi zinaweza kuwasaidia wajasiriamali wadogo wadogo, ili kuwaweka katika mazingira mazuri kama kuwapa hamasa na mafunzo. Vilevile Halmashauri hizi zinaweza kuwaleta wajasiriamali wetu katika Uwanja wa Sabasaba.  Wajasiriamali wengi wanatamani kuja Uwanja wa Sabasaba, lakini wanashindwa kutokana na hali duni na ufinyu waliokuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka hii ambayo leo hii tunapitisha Muswada huu, ikipewa uwezo sasa hivi kwa kuwa inakuwa Mamlaka, iwe na kanda ili wale wajasiriamali wadogo wadogo, watakaoshindwa kuja Uwanja wa Sabasaba, waweze kuweka maamuzi au mipangilio mizuri ambayo inaweza kuweka maonesho katika Kanda ili kuwasaidia.  Vilevile kupanua wigo kwa ajili ya biashara ndogo ndogo za hawa wajasiriamali ili waweze kuwa na kiwango kikubwa, waweze kuwa na ushindani, ukizingatia ukienda sehemu mbalimbali kama vile Kenya, unakuta JUAKALI. JUAKALI kuna wajasiriamali wengi na wapo wanaotoka Tanzania wanakwenda JUAKALI, wanakwenda Rwanda, lakini ni wajasiriamali wachache ambao wanakaa mijini kama Arusha na Dar es Salaam.  Wajasiriamali wengi walioko kwenye Mikoa kama ya Rukwa na Ruvuma, hawajui namna ya kuweza kuvuka kwenda mahali huko.

Mamlaka hii ikishakuwa tayari na wakiweka maonesho ya kila Kanda; Kanda fulani inafanya maonesho wajasiriamali wake wanakuja wanaleta vitu vyao, kuna wajasiriamali wengi ambao watajitokeza.  Viwango vile ni vizuri, wanaweza nao wakaondoka wakaenda hata kuuza nchi za nje.  Tatizo kubwa ambalo linawagusa wajasiriamali wetu ni kukosekana kwa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uwezo, lakini tukiweka wigo kama nilivyosema, TAMISEMI ikitoa ushirikiano mkubwa, ikitoa mafunzo na hamasa kubwa kwa wajasiriamali wadogo wadogo, ambao wana uwezo na kuwafikisha kwenye maonesho ambayo yatakayokuwepo katika Kanda au Dar es Salaam, nafikiri tutaweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa.  Wajasiriamali wengi wataibuka kuwa wajasiriamali wakubwa, wataweza kuchukua vitu vyao na kupeleka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajasiriamali ambao wanapata fursa ya kwenda kwenye Sabasaba, wanajifunza mambo mengi sana; kwa sababu wakifika kule wanakutana na watu mbalimbali, wanakutana na watu wa Kenya, Rwanda na watu wa nchi mbalimbali, ambao wanaleta vitu mbalimbali vinavyowafungua macho, kusema ala kumbe hiki kitu kinatengenezwa hivi; wanakuwa ni wachache ambao wapo maeneo ya Mikoani na Mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai, ninaomba niupongeze sana Muswada ulioko mbele yetu; lakini Mamlaka haya na TAMISEMI itoe ushirikiano mkubwa sana kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wadogo kuweza kuwapa mafunzo na kuwapa hamasa kubwa waweze kusaidia wajasiriamali. Vilevile kuna hawa Maafisa Biashara, sasa hivi hawana kazi ya aina yoyote, mimi sioni kama wana kazi, hata leseni siku hizi katika Mawilaya hazitolewi wapo tu. Halafu vilevile hawa Maafisa Biashara, wengi walikuwa Wizara ya Viwanda na Biashara nafikiri wakatolewa wakapelekwa Wizara ya TAMISEMI, naomba natoa ushauri, warudishwe katika Wizara ya Viwanda na Biashara ili wawe ndio mtandao mkubwa kuweza kuhamasisha wajasiriamali katika vijiji waliko. Kwa kuwa katika kila Wilaya, unakuta Afisa Biashara yupo tu hana shughuli ya kufanya, lakini wao ndio itakuwa chachu kubwa kuwaibua wale wajasiriamali wadogo wadogo waweze kutambulika. Nilikuwa natoa hayo tu ili waweze kutusaidia kuibua vipaji vya wajasiriamali wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mazungumzo mengi ila naupongeza sana Muswada huu na Mamlaka. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu. Ndugu zangu wa Wilaya ya Muheza, siku hizi wana utaratibu mzuri wa kisayansi, wanajua namna ya kutuma na kupokea salamu za mwaka mpya. Kwa niaba yao, naomba niseme Kheri ya Mwaka Mpya kwa Waheshimiwa Wabunge wote na ndugu zetu. Pia nimpongeze sana mwenzetu huyu, ambaye amechukua nafasi maalum kutoka kule Mbeya Vijijini na tumemkaribisha kwa vigelele leo hapa Bungeni. Karibu sana na tutakusaidia tena pale utakapohitaji msaada wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninauzungumzia Muswada huu kwa maelekezo na kwa kuelewa kwamba, kwanza, tunapozungumza nje, kwangu mimi tafsiri ya nje ni pamoja na Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi; nchi zilizoko katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Licha ya kwamba tupo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mshariki, bado biashara yetu katika nchi hizi inahesabika kama biashara ya nje ya nchi. Lingine ni kwamba, madhumuni ya Muswada wenyewe yapo mengi, lakini najikita katika dhumuni moja kubwa ambalo nitalizungumzia kwa kina na hili ni dhumuni la kukuza mauzo ya biadhaa za kilimo na mifugo. Kwa hiyo, katika mazungumzo yangu leo nitajielekeza katika maeneo hayo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo bidhaa nyingine nyingi, lakini mifano nitaielekeza kwenye kilimo na mifugo. Nafurahi kwamba, sasa Mamlaka hii inaundwa. Kwa miaka zaidi ya minne iliyopita, nimekuwa nikizungumza sana kuhusu biashara ambayo nimekuwa nikiona haisaidii taifa hili la Tanzania. Haiendelezwi katika mipango ya kibiashara, kama biashara inayotoka nchini kwenda nchi nyingine. Nimekuwa nikisema katika mazao ya kilimo, kwa mfano, machungwa kutoka Muheza, lakini na mifugo kutoka katika Wilaya zilizoko jirani na nchi zinazopakana na Tanzania, wamekuwa wakiuza mifugo kwenda nje ya nchi. Machungwa yanayouzwa nje ya nchi na mifugo yetu yote, hayaisaidii Tanzania kupata fedha za kigeni hata senti tano. *(Makofi)*

Nimekuwa nilieleza hapa kwamba, wenzetu wafanyabiashara hawa wa kutoka nchi jirani, kabla hawajaja Tanzania, wamekuwa wakiingia katika Benki zao wanabadilisha fedha zao za kigeni huko huko.  Wakiingia ndani ya nchi, wanaingia na fedha za Tanzania na wananunua bidhaa katika nchi ya Tanzania kwa fedha za Tanzania. Biashara gani ya nje ya nchi, kati ya nchi na nchi, inayoendeshwa kwa mtindo huo?

Pamoja na jitihada nilizojitahidi kusema sana, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa.  Naamini kwa sababu ya matatizo yaliyokuwepo hapa nchini kwamba, Bodi iliyokuwepo ilikuwa inayumba, haikuwa inawezeshwa hata kuweza kufanya kazi yake kikamilifu, lakini hata hiyo Bodi haikuwa na meno ya kutosha kwa wakati ule kufanya kazi nilizokuwa nikizisema zinatakiwa zifanywe.  Leo Mamlaka hii nimeiona imepewa meno na uwezo mkubwa wa kufanya yale tunayoyakusudia kuyafanya ili biashara iweze kuwa kweli biashara inayoweza kufanyika kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wafanyabiashara hawa wa nje kuja Tanzania, walikuwa wanadiriki kwenda mpaka mashambani, wao wenyewe wananunua huko kwa wakulima, licha ya kwamba wapo wengine waliokuwa wakiwatumia madalali wa Tanzania.  Kwa hiyo, Mamlaka ifanye kazi kwa ufanisi wa hali ya juu ili Watanzania tuweze kufaidika na biashara hii ya kwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi moja kubwa kwangu mimi ni kwamba, Mamlaka ijitahidi sana.  Zipo taasisi katika Wizara yenyewe ya Biashara na Viwanda, kuna maeneo mengine katika Wizara ya Mambo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini na katika Balozi zetu mbalimbali, vipo Vitengo vinavyosimamia utekelezaji wa biashara kati ya Tanzania na Nchi za Nje huko aliko.  Moja kati ya kazi kubwa ni Mamlaka hii sasa kuunganisha nguvu ya Vitengo hivyo vilivyopo katika maeneo mbalimbali, katika Balozi mbalimbali ili viweze kushirikiana na kukuza biashara ya nje kutoka Tanzania kwenda nchi za nje na kutoka nchi za nje kwenda Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tumezungumza sana kuhusu kuthibiti ubora wa bidhaa; hata hatukumaliza muda nimekwishasikia kuna bidhaa feki zilizokamatwa na inawezekana leo hii tunapozungumza zikateketezwa. Kwa Watanzania kuteketezwa kwa bidhaa ambazo zimeagizwa kutoka nje kuja Tanzania, lazima tuelewe kwamba, kuna fedha za kigeni zilizotoka katika mabenki yetu kununua bidhaa hizo. Hata kama ni kiasi kidogo, lakini ni fedha ambazo ni za nje na dhamana ya Watanzania.  Leo kununua bidhaa feki zinakuja zinateketezwa, maana yake fedha zetu za nje kwa kiasi fulani, tumeziteketeza sisi wenyewe.  Bodi ya Biashara ya Nje lazima ielewe na itoe elimu ili wanaoagiza bidhaa hizo na kufikia hatua ya bidhaa kuteketezwa na fedha zetu zimeteketea, waache kabisa mtindo huo ambao unaliteketeza taifa letu.  (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka inakusudia kuwa na matawi au vituo vya biashara ndani ya nchi. Mimi mapendekezo yangu ni kwamba, vituo hivi ambavyo mamlaka itafungua kwanza tuvielekeze katika maeneo ambayo yapo katika mipaka ya Tanzania, ambapo kuna biashara, kwa mfano, hizo za kilimo nilizozitaja na zile za mifugo ambazo nimezielezea.  Tuanze kuzisimamia ili tuone tutanufaika kwa kiasi gani na bidhaa hizo; ng’ombe wanaokwenda huko na machungwa yanayokwenda huko.

Kwa maana hiyo, nilikuwa na pendekezo langu pia, pamoja na sehemu nyingine na pale Muheza tuwe na kituo, tuuze machungwa tani nyingi kwa mwaka kwa fedha nyingi, lakini hatunufaiki na fedha za kigeni zozote. Tunaipenda sana biashara ile na hatutaki kuwepo na utaratibu mwingine wowote utakaowazuia wakulima wa Wilaya ya Muheza kupata fedha kutokana na mauzo yao ya machungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeshauri ni kutambuliwa kuwepo kwa madalali. Biashara hizo tunazozifanya za mifugo, za machungwa, wapo madalali, kwa hiyo, sheria iwatambue kwa sababu ni muhimu. Watu wa kutoka nje, hatutaki waende mashambani kununua machungwa moja kwa moja kwa wakulima, maana yake lazima awepo Mtanzania atakayefanya kazi hiyo ya udalali. Kwa hiyo, tutakapotengeneza kanuni zetu, basi ziwepo kanuni za kutambua madalali; waandikishwe rasmi, wawe na ofisi watambuliwe, ili wageni wanaotoka nchi za nje kuja kufanya biashara hizo wawe na uhakika wa usalama wa fedha zao na utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema sasa hivi kuna biashara kubwa ya mifugo imeibuka hapa nchini; ngombe, mbuzi, wanasafirishwa kutoka katika mkoa wa Tanga. Nina uhakika hilo litakwenda katika mikoa mingine, kwenda katika nchi ya Comoro; ng'ombe hao na mbuzi hao wanapitia Zanzibar. Nani anafanya biashara hiyo? Wanafanya biashara hiyo watu ambao hatuwafahamu, lakini wanafanya kwa mtindo ule ule wa kununua kwa fedha za Tanzania na kupeleka na kuuza nje ya nchi ya Comoro kwa fedha za kigeni. Hawana leseni, wala hakuna mtu yeyote anayewafuatilia wananchi hawa. Kweli bei wanayonunulia ng'ombe mmoja ni nzuri kwa mfugaji wa Muheza. Mimi nashukuru kama ng'ombe alikuwa ananunuliwa kwa shilingi 350,000, sasa watapata shilingi 500,000 hadi shilingi 600,000, lakini tutaendelea na biashara za namna hiyo mpaka lini? Tufanye kazi kisayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia sana Uwanja wa Maonesho, sitahitaji kusema sana lakini nataka niseme, tulipata adha mwaka uliopita wakati wa kufungua sherehe zile za Saba Saba pale; harufu kubwa ilikuwa inatoka kwenye dampo lililopo karibu na Uwanja ule wa Biashara wa Kimataifa mpaka tuliona aibu kwa wageni. Naomba jambo hili tulitazame vizuri. Vilevile tuangalie na yale magereji yaliyoko pale, yanayoleta adha kubwa na kufanya uwanja ule ukose nafasi ya kutosha. Jamani, tufanye jitihada ili kweli pale paonekane ni Uwanja wa Maonesho ya Biashara wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hizi nilizosema ziandaliwe za kuweza kuwatambua madalali, zitasaidia sana kujenga motisha kwa wanunuzi kutoka nje, kujenga imani kwa Watanzania na biashara za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu unakaribia kwisha, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Hebert Mntangi. Kama nilivyosema mwanzo, atafuatiwa na Mheshimiwa Basil Mramba na baadae tutamsikiliza

Mheshimiwa Jenista Mhagama, wakati Mheshimiwa Waziri anajiandaa kuja kuhitimisha hoja yake. Moja kwa moja nimkaribishe Mheshimiwa Senator Basil Mramba.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami niungane na wenzangu kutoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Luckson Mwanjale, Mbunge Mpya wa Mbeya Vijijini kwa kuchaguliwa. Mimi nimefarijika sana, kwa sababu niliwahi kuishi Mbeya na nikiona mtu yeyote wa Mbeya anaendelea, nafurahi sana. Karibu sana ndugu yangu Mwanjale, nipo tayari kuwa mwalimu pale utakaponihitaji.

Nichukue nafasi hii kwa mara ya pili, kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Nyaulawa, ambaye nafasi yake sasa imechukuliwa na Mheshimiwa Mwanjale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kupeana kila la kheri kwa mwaka huu mpya wa 2009, hasa kuwashukuru wale ambao wamenipa salamu za heri mahususi kutokana na hali halisi. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonisumbua sana mimi ni biashara yetu ya ndani, baada ya kufutwa kwa *Board of Internal Trade,* unaweza ukasema biashara ya ndani ya Tanzania haina mwenyewe. Mimi nilikuwa kwenye Wizara hii hadi mwaka mmoja uliopita na naelewa kwamba, biashara ya ndani ya Tanzania ni kama inaenda kwa kudra za Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, nimefurahi sana kwamba, kwanza, Mheshimiwa Rais alipounda Wizara hii upya, alisisitiza umuhimu wa kushughulikia biashara ya ndani. Ninawapongeza walionifuata kwenye Wizara hiyo kwamba, jambo hili sasa wamelihitimisha kwa kuleta Muswada hapa. Nawapongeza sana.

Niseme kwamba, pamoja na kuwepo kwa biashara holela holela, kuna maeneo Tanzania ambayo pengine Wizara ingependa kuyaiga au kujifunza kwao, namna wanavyoendesha biashara ya ndani. Eneo moja ninalolifahamu ni Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Iringa, una Programu Maalum ya Kuanzisha Maeneo ya Biashara Vijijini, nadhani wanafadhiliwa na Serikali ya Denmark, ambayo kwa namna nilivyojifunza ni mfano ambao ungeweza ukaigwa sana. Nasema hivyo kwa sababu maeneo mengi ya Tanzania, hayana maduka yanayoeleweka, hayana hata masoko ya kimila yanayoeleweka, sana sana tuna magulio ambayo kwa namna fulani inaweza ikawa ni kama ngoma ya mdundiko hivi; leo yako hapa, kesho yanahamia kule, kesho kutwa wanahamia kule, hayana utaratibu maalum unaoeleweka wa kisayansi. Kwa hiyo, ningetoa ushauri kwa Wizara kujifunza kinachoendelea pale Iringa, inawezekana wakaiga Mikoa mingine na Wizara kupitia sheria hii sasa, kupitia mamlaka hii na sheria yenyewe, wakaweza kueneza dhana hiyo nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wa pili ni Mkoa wa Kilimanjaro, ambao kwa muda mrefu sana, kabla hata sijazaliwa, tumekuwa na masoko ya kimila; masoko yale hata leo ukienda yapo. Hili ni eneo ambalo limetengwa maalum ngazi ya kata au kata mbili zinachangia eneo moja, kuna maduka yamejengwa kule yenye bidhaa mbalimbali; mengine ni *sub-whole salers,* mengine ni *whole salers* na mengine yana bidhaa ambazo

zimetoka mijini. Kwa hiyo, siku yoyote na wakati wowote, unaweza kwenda madukani huko ukapata bidhaa. Kubwa zaidi, wakulima wanaweza kwenda kwenye masoko hayo, wakichukua bidhaa pengine ni ndizi, maziwa, mboga, matunda na hata mifugo; mbuzi na ndafu zinauzwa kule. Kwa hiyo, wakati wowote ukihitaji aina fulani ya chakula kwa mfano au aina fulani ya bidhaa, ukienda pale sokoni utajipatia kila kitu; utanunua sabuni, utanunua nguo, utanunua viatu, utanunua ndizi, utanunua viazi, utanunua chochote kile unachohitaji hata mayai, hata mbuzi ukachinje.

Kwa hiyo, nilidhani, ingawa mfano huo haukuanzishwa na Serikali, lakini ni mfano ambao katika Mikoa mingine wenyeji wangeiga. Vilevile ingeweza ikasaidia na ikatoa sura nzuri sana ya bidhaa kupatikana mahali pamoja panapoeleweka wakati wote na wananchi wakaweza kuzinunua kwa ushindani, kwa bei nzuri na kwa upatikanaji ambao ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa tatu tayari unatekelezwa, nadhani Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza ule Mradi unaoitwa Mradi wa Masoko Vijijini. Nadhani Kibaigwa ni mojawapo ya eneo hilo na najua kuna maeneo mengine, ambayo yamekuwa yakiandaliwa na yanaandaliwa. Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, kuna mifano kadhaa. Maeneo haya ambayo ni *Trade Centers* ambazo zimetajwa kwenye sheria hii, nadhani kifungu cha 5(1), maeneo haya kwa kweli nafikiri ni muhimu na kama tungeyapanua yakawa mengi, yangeweza yakasaidia sana. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, pengine tungekuwa na maeneo ya namna hii kwa kila Kata na pengine Halmashauri za Wilaya zingeshawishiwa kujenga *infrastructure* inayotakiwa kama maji na umeme. Kwanza, kutenga eneo halafu kuvuta maji pale, kuvuta umeme, simu na vile vile wangeweza hata wakatenga eneo la viwanda vidogo vidogo. Watu wanatengeneza vitu, wanauza hapo hapo sokoni, eneo la maghala, vyakula vya ziada vikawekwa pale, wakaja watu hata kutoka maeneo mengine ya mbali wakanunua, wakapeleka mbele ya safari, wakaenda kuuza na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kwamba, kwenye eneo hili kifungu hicho nilichokitaja; *Trade Centers*, tuangalie utaratibu huo na tuufanye kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo nashauri, tulilizungumza sana kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara, ambayo mimi ni Mjumbe; ni kwamba, kwa sababu Serikali imejitoa kwenye biashara, Serikali hainunui wala haiuzi ni lazima Mamlaka hii iwe karibu sana na wafanyabiashara, wanaouza nje na wazalishaji wa bidhaa zenyewe. Hatuoni mahali popote kwenye Muswada huu, ambapo jambo hili limetamkwa waziwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kitu ambacho labda kwa kukosa maneno mazuri zaidi ninachoweza kukiita, *Stake holders Forum,* mara tatu kila baada ya miezi mitatu na kila baada ya miezi minne kuwepo kikao cha mamlaka hii na *stakeholders* kuzungumzia hali ya biashara ikoje na matatizo yakoje. Kwa hiyo, ningedhani kwamba, Mamlaka za Mazao shirika kama CTI, wale Wanachama wa Chama cha Wenye Viwanda, Chama cha Wenye Biashara, Viwanda, Kilimo na watu wengine mbalimbali, wanaofanya biashara wangeweza kuwa na kikao kimoja kila baada ya miezi mine,

kuzungumzia hali ya biashara ikoje. Ya pili, kama ninavyosema hapa, hata kupeana habari hivi ni kweli biashara hii inauzika; na kama inauzika ni wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, kuna wakati nadhani hata sasa lipo soko kubwa sana la soya, lakini ukienda kwenye maeneo ambayo yanastawi, bado wanang'ang'ania yale maharage tena ya kizamani, ambayo kwenye soko hayatakiwi. Soko leo linataka soya au aina fulani za maharage. Watu wa kawaida wangeweza kuzalisha bidhaa hizi, lakini nani awaambie; na huyo wa kuwaambia nae amelitoa wapi na nani atakayepeleka vitu hivyo kwenye soko?

Kwa hiyo, tunabaki katika hali ambayo siku nenda rudi, watu wanazalisha bidhaa zile zile hata kama hazina soko. Watu wa kuweza kutuambia kinachoendelea kwenye soko, kama alivyosema Mheshimiwa Zitto, kama ni kwenye ukanda Kenya wanahitaji nini sasa hivi, Malawi wanahitaji nini sasa hivi; vikao kama hivi vya *Stakeholders* vinaweza kutoa habari kwa wazalishaji na wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, wale *Stakeholders* wenyewe wataweza kuzungumzia matatizo mengine yanayoweza kukwamisha biashara, kwa mfano, usafirishaji. Mfano mzuri sana ni usafirishaji wa ndege; inashindikana kabisa ndege kubwa kutua kwenye Uwanja wa Kilimanjaro, ili zichukue bidhaa na badala yake tunaendelea kuuza maua kupitia KLM na mboga kupitia ndege nyingine, kiasi kidogo kidogo kwa sababu ndege zile nazo hazichukui kwa wingi. Kungekuwa na *Forum* ya namna hii, wangeweza kwa pamoja wakafanya mpango labda tutafute ndege aina fulani kutoka mahali fulani, ikafikisha maua soko fulani kisha ikaendelea au ikafikisha mboga soko lingine huko n'gambo. Kwa hiyo, kwa njia zile kila mtu atafaidika; mzalishaji atafaidika, soko la nje tutaweza kuuza na biashara yetu ya ndani na uzalishaji wa ndani na uuzaji nje vyote vinakuwa vinafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kwa dhati kuingiza kifungu kwenye Muswada huu. Labda mara baada ya (a),(b), pale mahali kwenye *functions* za mamlaka hii, iwe kitu kama vile kusema *to organize quarterly* au *frequent stakeholders' forum to address and advise on general or specific trade matters for consideration by the Authority and the Government.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mamlaka ikae na hawa watu wapate habari, ndio sasa iweze kusema namna ya kuishauri Serikali. Mojawapo ya kazi za mamlaka hii, kama tunavyoona kwenye kifungu cha 5(1)(a) *is to advise the Government*. Wataishaulije Serikali kama hawapati habari? Huko kwenye *field*, ndio maana nasema mahali fulani pale tuweke hizi *Stakeholders Forum* ni kitu muhimu sana katika Muswada huu. Ninaungana na *point* aliyokuwa anaisema Mheshimiwa Zitto kwamba; ni vizuri tukasema vitu *specific* vya kufanya, moja ni hili la kuendeleza *trade centers* kama nilivyosema vijijini.

La pili ni hili la kuwa na *Stakeholders Forum*, ambazo zitatafakari masuala mara kwa mara na kushauri mamlaka yenyewe na serikali yenyewe. Kwa njia hiyo, labda biashara ya Tanzania itaanza kutembea badala ya sasa ambayo inasukumwa, inakwenda

bila kuwa na utaratibu mzuri ulioandaliwa na kuwa na utaratibu mzuri ambao unaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimalizie tu kwa kusema, mimi ni kati ya watu ambao wamefurahi sana kuona jambo hili linakuja sasa na litaunganisha viwanda vidogo ambavyo viko vijijini. Vilevile linaweza likatoa sura mpya kabisa kwenye biashara ya ndani na uzalishaji wa ndani wa bidhaa mbalimbali hapa Tanzania. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Basil Mramba, kwa mchango wako. Kama nilivyosema, mwanzo mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, wakati Mheshimiwa Waziri anajiandaa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji, ingawa nimekuwa mchangiaji wa mwisho lakini niseme tu kwamba, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, walioanza kuchangia mada hii wameweza kutoa maoni na ushauri wa kutosha kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa analiapisha Baraza Jipya la Mawaziri mwaka 2008, mwezi Februari, alitoa hotuba nzito sana na aliwaambia Watanzania anakusudia baada ya kuunda Baraza hilo Jipya, ataunda Chombo Maalum, kitakachoweza kusimamia suala zima la biashara katika nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu kile alichokitamka siku ile alipokuwa anaunda Baraza Jipya la Mawaziri, leo kimeweza kuja mbele ya Bunge lako Tukufu na kuweza kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka maneno ya Mheshimiwa Rais wakati anatamka tamko hilo, alitoa mfano alisema, inasikitisha sana kuona… Mheshimiwa Zitto Kabwe amerudia yale maneno kwa namna nyingine; nchi hii kuna wazalishaji wa mazao mbalimbali. Kwa mfano, Mkoa wa Ruvuma wanazalisha mahindi, lakini kule Mwanza wanaweza kuwa na njaa na hawana mahindi na kule Mwanza mahindi yanaweza yakawa yanauzwa kwa bei kubwa sana, lakini ukienda Ruvuma, utakuta mahindi hayo hayo yanauzwa kwa bei ndogo sana. Mfano huo ulimpelekea Mheshimiwa Rais, kwa makusudi mazima, kuona kwamba, sasa inatosha ni lazima aunde chombo maalum, kitakachoweza kusimamia mfumo mzima wa biashara ndani ya nchi na mahusiano yetu ya kibiashara nje ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujiulize; ninataka niongee kwa ujumla wake, naupongeza uanzishaji wa mamlaka hii, lakini ninataka kutambua kazi kubwa ya wataalam wetu na Wizara katika kutoa majukumu yatakayofanywa na mamlaka hii, kwa maana ya kazi zitakazofanywa na Mamlaka hii.

Nilipoziangalia nilipata nguvu ya kujiuliza hivi, Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya Tanzania nikianza na hapo, nchi yetu inasifika kwa bidhaa gani? Tukiulizwa swali hapa

la dharura tu Waheshimiwa Wabunge, labda ukawa ni mtihani wa uchaguzi wetu mwaka 2010 kwamba, anayetakiwa kurudi Bungeni mwaka 2010 aanze kujibu swali hili; hivi nje ya nchi ya Tanzania nchi yetu inatambulika kwa kuuza bidhaa zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndio tuanzie, ninachofahamu angalau tunatambulika kwa kuuza mazao ya kilimo kama kahawa, pamba, tumbaku, korosho na katani, kwa namna moja au nyingine. Mazao haya yote, yanauzwa kule yakiwa ghafi na ukiangalia biashara ya mazao haya, imekaa katika muundo wa kukuza uchumi wa nchi ama kuangusha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema mamlaka hii imefika wakati muafaka na kazi za mamlaka hii ni pamoja na kuishauri Serikali yetu, njia ambayo itasaidia kutengeneza mfumo wa biashara utakaowajenga Watanzania kuwa wafanyabiashara wazuri, ndani ya nchi yao. Vilevile kumiliki rasilimali za kibiashara tulizonazo ziwe za kilimo, ziwe za bidhaa katika kukuza uchumi wa nchi na uchumi wa Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio umuhimu ninaouona upewe kipaumbele, kwa mamlaka hii katika kusimamia zoezi zima hili la biashara ya ndani na biashara ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka hii leo tunaipa jukumu la kuishauri Serikali yetu, ingawa itatakiwa isimame kama chombo mahususi kitakachobeba dhamana kubwa ya mustakabali wa maisha ya Watanzania katika sekta hii ya biashara. Ninaomba sana Mamlaka hii ijiunganishe vya kutosha na Wizara nyingine, Mashirika mengine na Taasisi nyingine, ambazo zitasaidia kutufikisha kweli huko tunakofikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe tukubali kwamba, leo tunapozungumzia biashara ya nje, hatuwezi kuuza kitu chochote nje ya Tanzania, kama hakina ubora unaotakiwa. Mheshimiwa Mntangi amesema, tumepitisha Sheria ya Viwango jana, lakini hivi tumejiandaa namna gani kuhakikisha wafanyabiashara wetu katika nchi yetu ya Tanzania, watapeleka bidhaa katika masoko ya kilimwengu, bidhaa zenye kiwango kinachotakiwa lakini tukaacha hii tabia ya kuendelea sisi Watanzania kuwa ni soko la kupokea bidhaa zisizokuwa na hadhi, zisizokuwa na ubora na zinazoharibu uchumi wetu kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Mamlaka hii ni kuhakikisha inafufua viwanda vitakavyofanya kazi ya kusaidia uzalishaji ndani ya nchi yetu, kwa matumizi ya ndani ya nchi. Vilevile biashara ya nje ya nchi, inaenda kwa kasi kubwa kuliko kitu kingine chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kufika mahali popote kama mazao yetu yataendelea kuuzwa yakiwa ghafi, bila kuyabadilisha kuwa bidhaa ambazo zitaongezewa uwezo kupitia kwa wafanyabiashara na kuyauza katika suala zima la kuwa bidhaa ili kukuza uchumi wa nchi yetu na kuleta Pato la Taifa na vile vile kuwasaidia wafanyabiashara wetu kulingana na mfumo mzima wa soko la ndani na soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba mamlaka hii ishauri sana kwenye suala zima la kukuza viwanda vyetu, lakini vile vile kuongeza thamani ya mazao yetu yawe ni mazao ya biashara, mazao ya mboga mboga au ya chakula; kwa namna yoyote itakavyoonekana. Biashara hiyo tunayoitafuta nje ya nchi na ndani ya nchi, iwe ni ya viwango ambavyo vinatakiwa na heshima ya nchi yetu katika kufanya biashara ndani na nje ya nchi iweze kwenda sambamba na wenzetu wengine tutakaopambana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusione suala hili ni suala la mchezo, biashara sasa hivi kimataifa ina ushindani mkubwa sana, ikiwezekana tufanye makusudi mazima kupitia Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana tutoe ruzuku katika mazao ama maeneo yale tunayoona kwamba, biashara hizo zikifanyika zitaleta tija na vilevile zitaongeza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye maamuzi hayo lakini tukiendelea tu kusema, nchi yetu imekuwa ina sifa ya kuwa na mipango mizuri sana, lakini mipango ile haisimamiwi na kutekelezwa inavyotakiwa. Matokeo yake, tunaweza kuwa tunapitisha sheria nzuri, yenye mwelekeo mzuri, lakini utekelezaji wake ukawa si wa kusaidia kwenda mbele ni wa kutufanya tuendelee kuwa hapa hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mamlaka hii kwa namna moja ama nyingine, kwa kushirikiana na mamlaka nyingine katika nchi yetu ya Tanzania, zizingatie pia usimamiaji wa mipango ya bei katika nchi yetu ili kupunguza mifumko ya bei isiyokuwa na maana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka itashughulikia suala la biashara ya ndani na nimetoa mfano, wakati Mheshimiwa Rais, anatoa ahadi ya kuunda Mamlaka hii, ilikuwa ni kuona namna gani wakulima wa mahindi, kwa mfano, Mkoani Ruvuma, Jimbo la Peramiho, Wilaya ya Songea, wangeweza kuuza mahindi yao kwa bei nzuri kule Mwanza. Tumegundua kwamba, hapa katikati bei zimekuwa zikipanda na kushuka, kama homa ya vipindi; hakukuwa na mwelekeo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa Mamlaka hii itapata hadhi ya kusimamia suala zima la biashara, basi litoe mafunzo, liwezeshwe, lihusiane na vyombo vingine ndani ya nchi yetu ya Tanzania, pamoja na kwamba, mfumo wetu ni wa soko huru, lakini mamlaka isaidie.

Pamoja na kuwa na mfumo wa soko huru, udhibiti wa bidhaa na udhibiti wa bei, Mamlaka itusaidie sana ili kuwasaidia Watanzania kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali, wakati Waziri wa Viwanda na Biashara alipokuwa anapitisha bajeti yake ya mwaka 2008/2009 alisema, Serikali kupitia Wizara yake, inalenga kutekeleza Programu Maalumu ya Kuongeza Uzalishaji wa Bidhaa na kuuza ndani na nje ya nchi. Alisema pia kwamba ni lazima tufikie mahali,

tujenge mahusiano ya kibiashara kati yetu na nchi za Mashariki ya mbali kama China na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini Mamlaka hii itatupeleka huko, lakini ni lazima tuendelee kuwa waangalifu. Mamlaka hii itusaidie kuyapambanua hayo mahusiano na hao marafiki tutakaofanya nao biashara, iangalie ni namna gani Watanzania wataweza kupata nafasi ya kufanya biashara katika nchi yao na nje ya nchi, kabla ya kukaribisha wawekezaji ambao wamekuwa wakichukua biashara hata za Watanzania. Ukienda Kariakoo, utapata ushahidi wa haya ninayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara za Watanzania zimechukuliwa na watu wengine, sasa Mamlaka hii nitaomba sana itusaidie. Tunao vijana wengi, ambao wangeweza kufanya biashara, lakini maeneo ambayo yanafanyiwa biashara na watu waliokuja badala ya vijana wetu wa Tanzania, yameweza kupoteza ajira nyingi za kujitegemea kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hoja ya kuunda Mamlaka ya kushughulikia na kusimamia suala zima la biashara ya ndani na nje. Naendelea kusisitiza kwamba, tuwe na mwelekeo wa kuhakikisha muundo huo wa biashara uwe ni muundo utakaoleta mageuzi ya kiuchumi kwa nchi yetu na kwa Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile muundo huo wa biashara, ubadilishe dhana nzima ya uzalishaji kwenye nchi yetu kutoka uzalishaji holela kwenda katika uzalishaji wenye tija na hasa tukianzia na mazao ya kilimo ambayo ndiyo yamekuwa ni ghafi kubwa ya kutengeneza biashara katika dunia kupitia nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaiunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo juu ya Muswada huu wa Mamlaka ya Biashara katika nchi yetu. Nami pia nawatakieni kheri ya mwaka mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono, kwa sababu mimi ni mmoja kati ya watu ambao nimekuwa nikizungumzia sana, juu ya kuboresha biashara zetu ama kuwahamasisha Watanzania kushiriki kikamilifu katika biashara ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeshafika milioni arobaini, lakini kama unataka kutafuta idadi ya Watanzania wanaochangia katika uchumi wa nchi yetu kwa maana ya kuchangia, acha wale ndugu zangu Wamachinga wanaotembea kutwa nzima wakitafuta riziki yao, sidhani kama tunazidi ama watazidi asilimia 15.

Mimi si mchumi, lakini katika hali ya kawaida na katika mahesabu ya kawaida, milioni 40; asilimia kumi na tano, kwa vyovyote vile itakavyokuwa uchumi wetu hautakwenda kwa kasi kiasi hicho, kwa sababu wanaochangia ni wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilianza kuunga mkono Muswada huu, kwa matarajio kwamba, Mamlaka haya na siyo Mamlaka hii, yatafanya kazi kubwa ya kuhamasisha na kusaidia Watanzania kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi yetu. Ninataka niungane na wale ambao wamesema hivi, maana hili linaweza kuwa ni donda ndugu, tunapopitisha sheria hizi tunalenga wakazi wa Mijini na tunasahau kwamba, vijijini ndiko waliko Watanzania wengi na ndiko mazao mengi yaliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mfano, kule kwangu Chiwata, wanalima nyanya kwa wingi tu na ni hodari kweli kweli, lakini nenda kaitazame ile barabara ambayo wanaitumia kupitisha nyanya zao kupeleka sokoni si nzuri hata kidogo. Nataka kusema kwamba, Mamlaka haya kwa kushirikiana na maeneo mengine na Mamlaka nyingine katika nchi yetu, lazima kuhakikisha kwamba, barabara zetu vijijini zinatengenezwa katika kiwango ambacho mkulima wa kawaida atapata urahisi wa kusafirisha bidhaa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika eneo la *Establishment of the Authority; there is established the Tanzania Trade Development Authority*. Ukisoma neno hili, linakupa matumaini makubwa kwamba, sasa kazi imeiva na ukisoma kipengele cha 5(b); *integrate the domestic market development*, bado inakupa matumaini makubwa lakini wasiwasi wangu inawezekana Muswada huu ukashindwa kufanya kazi vizuri, kwa sababu ya kuwawezesha wafanyabiashara hawa waweze kuyafanya haya ambayo yamo ndani ya Muswada huu. Kwa mfano, wafanyabiashara wengi, pamoja na wakulima, uwezekano wa wao kupata mikopo ni mdogo sana. Kwa hiyo, haya yanaweza yakaishia katika makaratasi tu, kwa sababu hawana fedha za kuanzia. Naomba Mamlaka haya, watakapokuwa wanatekeleza majukumu yao na eneo hili la fedha za kuanzia vijijini na mijini walizingatie sana ama sivyo mamlaka itasua sua kuendesha shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kama wenzangu walivyosema, Tanzania hii tuna mazao mengi sana na tuna matunda mengi sana, lakini kwa sababu hatuna utaratibu mzuri wa kuyafanya matunda haya yawe na thamani au yafike sokoni kirahisi, matunda haya yanaoza kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu kuna embe nyingi, ukifika Kilwa pale pana machungwa mengi, ukienda Muheza kama alivyosema Mheshimiwa Mntangi pale, machungwa unayasukuma kwa mguu. Wanakuja wenzetu majirani wanayachukua kirahisi rahisi tu, wanakwenda kutajirika. Muswada huu sasa uje kutoa majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka kukubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Basil Mramba, kuwe na tathmini baada ya muda Fulani, ili tujiridhishe kama kweli huu Muswada unafanya kazi kwa Watanzania.

Mimi nasema tumeuchoka umaskini, Watanzania wana uwezo mkubwa, wanachokosa ni msukumo tu. Tukiwezeshwa tunaweza na Mamlaka haya yatafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuahidi kwamba, nitazungumza kidogo sana, lakini mazungumzo yangu yatakuwa mazito na hivyo ndivyo nilivyofanya. Ninaunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Suleiman Kumchaya.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naipongeza Wizara nzima kwa mashirikiano mazuri sana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara na pia kwa kuwasilisha Muswada huu kwa faida ya Tanzania. Nawapongeza sana hasa chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mary Nagu (Mb) na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Cyril Chami (Mb), Mungu awabariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mipango hii iliyowasilishwa, sina shaka isipokuwa juhudi ziendelee na ukipita Muswada huu basi elimu za biashara zizidi kutolewa na tuwe na mikakati ya kukuza zaidi biashara nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Biashara na Sekta zake, ipewe uwezo mkubwa kuweza kuwezeshwa na watoa semina katika ngazi mbalimbali za ndani na nje, kwa mambo haya ya biashara. Mabenki yafanye kazi na kuijali nchi ya Tanzania, lakini tuwe na miundombinu ya biashara na tahadhari ili tufaidike.

Kwa niaba ya Wananchi wa Magogoni, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kuunda Mamlaka mpya ya Maendeleo ya Biashara Nchini, ambayo inapewa nguvu mpya za kusimamia, kuendeleza na kulinda maslahi ya biashara za ndani na nje ya nchi, kwa lengo la kuinua uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza sana kuwa Mamlaka hii ijikite sana, katika kuzilinda biashara zinazotokana na uzalishaji wa mazao yanayozalishwa hapa nchini, licha ya kuwepo kwa utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mdau ninayetoka katika eneo linalozalisha sukari kwa wingi nchini, ingawa ni kweli kwamba, uzalishaji wa sukari nchini hautoshelezi mahitaji na Serikali inaruhusu kuingizwa kiasi cha sukari kutoka nje ya nchi, tatizo lililoachwa bila uthibiti ni kuwaacha wafanyabiashara wasio waaminifu, kuingiza nchini kwa wingi mno sukari ambayo ni *sub-standard* na ambayo ni zaidi ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtindo huu unaharibu soko la sukari ndani ya nchi, kwa kushusha sana bei halisi ya sukari inayolingana na gharama za uzalishaji.

Matokeo ya vitendo hivi ni kushusha ufanisi wa uzalishaji nchini na pia kushusha bei ya miwa wanayolima wakulima wadogo, ambao bei yao iko *pegged* kwenye bei ya kuuza sukari inayozalishwa nchini. Hali hii inawakatisha tamaa wazalisha miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iisimamie Mamlaka hii, idhibiti hali niliyoieleza hapa.

Kwa maelezo haya, naunga mkono hoja.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *page 4* kwenye *interpretation* ya *Local Government Authority*, iongezwe namba na mwaka wa *Local Government Act.* Mwaka 1982, Namba …

Mheshimiwa Mwenyekiti, *page* 11, *Section* 22(4), kwenye *penalty;* "*not less than ten million shillings and not exceeding twenty million shillings.*" Ushauri wangu, *ten million* ni kubwa mno kwa Mtanzania, iwekwe *maximum, minimum; Judge* anangalie mwenyewe. Pia kifungo iwekwe *maximum, minimum; Judge* aangalie mwenyewe isiwe *imprisonment for a term of 12 months*. Section 23(4), maoni yangu yanafanana na Section 22(4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ulioandaliwa na Wataalam wa Wizara ya Viwanda na Biashara, chini ya uongozi thabiti wa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na timu yake; Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi ni hatua muhimu kimapinduzi. Naunga mkono Muswada.

Kama ilivyoelezwa kuwa, madhumuni ya huu ni kutunga sharia mbalimbali, zenye malengo ya kuboresha, kwa kutekeleza Sera ya Taifa ya Biashara na mkakati wa kukuza mazao na bidhaa zetu kwa lengo la kuendeleza biashara ya ndani na nje ya nchi.

Katika kutoa michango yangu, kwa lengo kuboresha Muswada, napenda kutoa ushauri au mapendekezo yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa sheria itakayotungwa itakusudia kufuta Sheria ya Halmashauri ya Biashara ya Ndani na Sheria ya Halmashauri ya Biashara ya Nje; nashauri Mamlaka ihakikishe kuwa, urasimu wa kutoa leseni ya biashara urahisishwe kwa kuwa na kituo kimoja *(one shop centre)* katika Mikoa. Vilevile sheria izingatie ada ya leseni, kwa lengo la kuwavutia wafanyabiashara wadogo hasa wanawake waishio vijijini.

(ii) Kuhusu majukumu ya Mamlaka, ibara ya 5(1)(m) ni kuandaa Maonesho ya Biashara ndani na nje ya nchi. Asilimia 90 ya Watanzania ni wakulima na wafugaji; nashauri Mamlaka ihakikishe Maonesho ya Biashara ya Kilimo na Mifugo yanaadaliwa kimkoa na kiwilaya, kwa kuwahamasisha wakulima kuonyesha bidhaa zao na

kuwashindanisha kwa kutoa zawadi.  Utaratibu huu hutoa nafasi kubwa na pana kwa wakulima na wafugaji vijijini, badala ya hali ilivyo sasa ya kuandaa maonesho kikanda.

Napenda kumalizia kwa kumshukukru Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa kutuletea Muswada huu.  Naomba ushauri nilioutoa uzingatiwe.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maendeleo ya Biadhara Tanzania, itasimamia moja ya eneo muhimu katika uchumi wa nchi; lile la biashara ya ndani na nje.

*Clarification* inayohitajika ni uwezo wa Mamlaka husika, uliopewa katika kuendesha shughuli zake.  Madhumuni kama yalivyobainishwa, inaonekana kama vile Mamlaka itakayoundwa inapachikwa tu (*inserted)*.  Sera na sheria zipo zinazotawala eneo la biashara tayari zipo.

Mamlaka itawajibikaje kutokana na sera zilizopo pamoja na ku-*enforce* madaraka ya mamlaka?

Je, Mamlaka iatafanyaje kazi yake kuteleza baadhi ya vipengele muhimu kama kila cha kupunguza "*cost of doing business*"?

Je, Mamlaka ita-*intervene* vipi pale maamuzi yanapocheleweshwa au pale ambapo urasimu umezagaa?

Ni vyema tuige mamlaka kama hii ya Marekani *(Competitiveness Council of USA)*, ambayo inalinda *standards* za bidhaa, zinanyang'anya leseni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kutoa pole kwa familia ya Marehemu Richard Nyaulawa. Halikadhalika, nampongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, ambaye sasa amechukua nafasi ya Marehemu Nyaulawa.

Ninawapongeza sana Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Kuleta Muswada huu Bungeni, unaleta ufufuaji mkubwa wa biashara ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna aina nyingi za masoko, lakini hili linaloendeshwa na TAMISEMI la kuendesha masoko ya vijijini kama lile la Kibaigwa; Wananchi wapewe fursa ya biashara za aina mbalimbali ili waweze kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu muhimu cha kukuza biashara ya ndani na nje ni taarifa juu ya masoko ya aina mbalimbali. Wadau wakipewa nafasi ya kukutana mara kwa mara, watabadilishana mawazo na taarifa ya masoko ya bidhaa mbalimbali.

Muswada huu unatoa nafasi kubwa, kwa biashara zetu vijijini kukua na kutoka nje ya nchi. Hii ni fursa pekee ya kuzalisha bidhaa zinazotakiwa na sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Waziri mwenye Dhamana na Wizara hii, pamoja na Naibu wake na Watendaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la majukumu ya taasisi na mamlaka mbalimbali zinazojihusisha na ubora wa bidhaa mbalimbali, kutoka nje ya nchi na kutoka viwanda vyetu hapa nchini, taasisi ni kama *TBS, TFDA* na kadhalika, mimi naomba nijikite kwenye madawa na vipodozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa yapo madawa na vipodozi ambayo hayapo kwenye viwango, kwa mfano; vipodozi vingi hivi sasa vinaleta athari nyingi kwa watumiaji. Akina mama wengi hivi sasa wanaota ndevu nyingi kama wanaume, wengine mpaka na sharubu. Kama hiyo haitoshi, watu wengi hivi sasa wanasumbuliwa na matatizo ya figo, lakini pia akina mama wengi ngozi zao zinaungua na hata baadaye kupata saratani ya ngozi. Hivyo basi, ningeomba hizi taasisi zilizopewa dhamana, zifanye kazi kwa makini na kwa uaminifu ili kuokoa maisha ya Watanzania.

Kuhusu madawa, yapo ambayo muda wake umepita lakini bado yapo kwenye soko na watu wanayatumia, hii ni hatari sana; madawa haya husababisha wagonjwa kutokupona kwa vile ni *PLACEBO*, lakini pia husababisha usugu wa maradhi katika mwili wa mtumiaji. Wakati mwingine madawa yanaonyesha bado muda wake wa matumizi, lakini yanakuwa yameisha nguvu kutokana na utunzaji mbaya wakati wa kuyasafirisha au kuyatunza. Naomba wawe makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawatakia kheri sana na maisha marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri, ahitimishe hoja yake.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipataia nafasi hii ili niweze kutoa maelezo kutokana na hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na kuchangia Muswada huu wa kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Miashara Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitoe shukurani kwa Kamati ya Kudumu ya Viwanda na Biashara, kwa ushirikiano mkubwa waliouonyesha katika kutusaidia kuuboresha Muswada ambao tunaujadili leo. Kamati hii ina Wajumbe

waliobobea katika biashara na wengi wamefanya kazi katika Sekta hii ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu itaendelea kutumia maelekezo, ushauri na busara za Kamati hii, ili kuzidi kuiimarisha Sekta hii hasa hii ya Biashara ambayo ni muhimu sana katika kuondoa umaskini na kuongeza kipato cha wananchi wetu na kuwa maisha bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niishukuru Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia Muswada huu kwa nia ya kuuboresha. Waliochangia kwa kuongea hapa Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Herbert Mtangi, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Clemence Lyamba, na Mheshimiwa Pindi Chana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijaribu kupitia hoja moja baada ya nyingine, kwa zile ambazo nimezikamata na zile ambazo hatukuzikamata, tutazijibu kwenye majibu ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ambayo imetolewa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, ilikuwa ni umuhimu wa kuwasaidia wajasiriamali wadogowadogo. Alisisitiza sana katika hotuba yake kwamba, Mamlaka hii ihakikishe kwamba, haimnufaishi mfanyabiashara mkubwa tu, lakini hata mfanyabiashara mdogo ananufaika. Majibu ni kwamba, kifungu cha 5(1)(f) na (g) na kifungu cha 5(2)(g), vinaeleza ni kwa namna gani Mamlaka itakavyoshirikiana na wajasiriamali wadogowadogo, pamoja na taasisi nyingine katika kukuza biashara. Kwa kutumia vifungu hivi, utaratibu wa kuwasaidia wajasiriamali wadogowadogo, utaainishwa kwenye mikakati ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo Mwenyekiti ameisema ni Bodi ya Mamlaka kuwa na Mwakilishi wa Viwanda Vidogovidogo, hapa alikuwa anatia msisitizo kuhusu umuhimu wa kuinua Sekta ya Viwanda Vidogovidogo. Ushauri huu umepokelewa na utatekelezwa ipasavyo, kwani lengo ni kuhakikisha wajasiriamali wadogo wanaendelezwa na kuweza kubadilika na kuwa wajasiriamali wa kati na wakubwa, wenye uwezo wa kukabili ushindani na kuchangia zaidi kwenye uchumi. Kifungu cha 27 kinamruhusu Mheshimiwa Waziri anayehusika na biashara, kufanya marekebisho katika jedwali na hivyo kuwezesha kuwepo kwa Mjumbe kutoka *Small and Medium Enterprises.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu imeulizwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Lucy Owenya, ambaye alipenda kupata ufafanuzi kuhusu utolewaji wa ushauri wa uendeshaji mzuri wa biashara kama ni bure au kuna gharama zitakazokuwa zinaambatana na ushauri huo. Kifungu cha 5(2)(a) kinasema, ushauri utatolewa bure kwa yale makundi yanayotaka kutumia ushauri huo, kwa dhamira ya kujitengenezea fedha nyingi. Ipo haja ya wao kutozwa kiasi kidogo cha ada, hasa pale ambapo ushauri huo utaigharimu Mamlaka nayo kuingia mfukoni na kutumia fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ameitoa Mheshimiwa Lucy Owenya ni kifungu cha 5(e), ambacho kinamtaka mfanyabiashara kupata kibali kwa Mamlaka kabla ya kupeleka bidhaa zake kwa ajili ya maonesho nje ya nchi. Muswada haujaweka wazi, adhabu atakayopewa mtu au taasisi itakayokaidi kifungu hiki. Aidha, Muswada haujabainisha jinsi ya kukata rufaa kwa yeyote atakeyefanyiwa hila na Mamlaka.

Kwanza, tuseme hapo kwamba, adhabu imeainishwa katika kifungu cha tano na kifungu hicho kinasema; kama mtu ameomba kupeleka bidhaa zake nje na imetokea kwamba, labda amenyimwa kibali na Mamlaka husika, mtu huyo anao uwezo wa kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana ya biashara, kupinga uamuzi huo. Asiporidhika na maamuzi ya Waziri, baada ya Waziri kupitia rufaa yake, mtu huyo vilevile anao uwezo wa kukata rufaa katika Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara. Adhabu hii ambayo nimeisema ya ukiukwaji wa sheria, imebainishwa katika jedwali la marekebisho, kipengele (h), kuna adhabu ya mtu atakayekiuka maelekezo ya kupata kibali cha Mamlaka kabla ya kupeleka bidhaa zake nje kwa ajili ya maonesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni hoja ya kwamba, Serikali iondoe maneno *receive gifts,* kwani yanaweza kupelekea rushwa katika utendaji wa Mamlaka. Majibu ni kwamba, tunakubaliana na hoja ya mchangiaji kama ilivyo katika maoni ya Kambi ya Upinzani; ni kweli kwamba, mtu anaweza akatumia nafasi hiyo ya kupokea zawadi halafu baadaye akafanya maamuzi ambayo si sahihi kwa kushawishiwa na hiyo zawadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7(2)(e), nacho kina hoja kutoka kwa Mheshimiwa Lucy Owenya, ambaye anasema taratibu na kanuni za ajira za Asasi za Serikali zifuatwe badala ya kuipa Bodi mamlaka ya kufanya uteuzi wa watumishi wa Mamlaka kwa kadiri inavyoona inafaa. Utaratibu wa kuwapata watumishi, unafuata mfumo na utaratibu wa Serikali ulio wazi na wa haki kwa wote wenye sifa, ikiwa ni pamoja na atakayeajiriwa atakuwa na sifa za kumudu majukumu ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, kulingana na wakati huo.

Kwa hiyo, nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, hilo analolisemea lipo katika sheria na hata katika kanuni za utendaji wa Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kuhusu nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Biashara Tanzania. Mheshimiwa Lucy Owenya, anatoa hoja kwamba,

nafasi hiyo itangazwe na ishindaniwe na wote wenye sifa na vigezo, badala ya uteuzi kufanywa na Mheshimiwa Rais. Majibu ni kwamba, utaratibu uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka, utakuwa wa wazi na wa ushindani, kwa kutangaza nafasi hiyo kwenye vyombo vya habari na baada ya mchujo, majina matatu yatawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na Rais atafanya uteuzi baada ya kupokea majina hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine inahusu mambo ya ajira katika Mamlaka inayotarajiwa kuundwa, ambayo inahusu viwango vya mshahara. Mheshimiwa Owenya, anatoa hoja kwamba, viwango vya mshahara virekebishwe kutokana na taaluma na uzoefu wa watumishi ili kuongeza motisha ya watendaji na siyo kwa Bodi kutoa mishahara kulingana na wao wanavyoona. Jibu hapa ni kwamba, Bodi inapewa mamlaka ya kuajiri afisa yeyote, pale tu itakapoonekana kuna haja ya kufanya hivyo, kwa masharti na malipo itakavyoona inafaa. Kuajiri huku si kwa watumishi wote wa Bodi, bali ni pale tu itakapoonekana kuna haja ya kufanya hivyo; mfano, endapo itatokea kuna haja ya kuajiri Mtaalamu wa Utafiti wa Biashara au Mshauri Mwelekezi, kwa ajili ya kazi Fulani; ni wazi kwamba, masharti yake na malipo au mishahara yao, itakuwa tofauti kutokana na kazi yenyewe, kipindi cha kazi na muda wa tatizo lenyewe ambalo linahitaji mtalaamu huyo kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijibu hoja ya Mheshimiwa Siraju Kaboyonga; amesisitiza umuhimu wa kutoa kipaumbele kwa uzalishaji kwamba, mamlaka hii isiishie tu kwenye biashara, lakini vilevile ijaribu kuliangalia suala zima la uzalishaji ili kuwafanya Watanzania wazalishe bidhaa ambazo zitaendana na masoko ya kimataifa yanavyohitaji bidhaa. Mamlaka itakayoanzishwa, itazingatia suala la uzalishaji na uboreshwaji wa bidhaa. Katika kutekeleza jukumu hili, Mamlaka itashirikiana na Wizara na taasisi nyingine kama vile Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti wa Mazao. Ukiangalia kifungu cha 5(1)(c), kinaainisha suala hili, pale inaposema kutakuwa na *product promotion;* maana yake ni kuhakikisha kwamba, Watanzania wazalishaji wanazalisha kile ambacho kinahitajika nje. Kwa maana hiyo, itashiriki sana katika kutoa mafunzo, semina na hata warsha za kuwafanya Watanzania wajue huko nje kunahitaji vitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kaboyonga amesema Uwanja wa Maonesho wa Dar es Salaam uboreshwe ili utumike kwa lengo la maonesho. Hapa tunaahidi kwamba, Mamlaka itaendelea na juhudi za kuendeleza maonesho ya kisekta, kwa lengo la kuzipa sekta fursa ya kuonekana na kujitangaza zaidi. Vilevile tunatambua umuhimu wa uwanja huo wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na tutajaribu kadiri ya uwezo wetu, kuupa sura ya kimataifa kadiri uwezo wa kifedha utakavyoongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Kaboyonga amesema, ipo haja ya kuiangalia Bodi ya Wakurugenzi, kwa sababu imelenga zaidi kuwa na watumishi wa Serikali badala ya wadau wa biashara. Nataka nimhakikishie kwamba, hilo tumeliangalia. Kifungu cha 27, kinamruhusu Mheshimiwa Waziri, kufanya marekebisho katika jedwali na hivyo kuwezesha uteuzi wa Wajumbe kutoka kwa wawakilishi wa wadau wengine na hata kwenye Kamati tuliliongea sana. Imeonekana ipo haja siyo tu ya kuwateua kwa sababu wanatoka kwenye taasisi nyingine, lakini vilevile anayepatikana

awe ni mtu ambaye kwa kweli anahusika katika kazi ya biashara ili alete uzoefu mpana katika masuala haya ambayo tunamteulia kwayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni hoja ya Mheshimiwa Zitto; kwanza, nataka nimshukuru sana Mheshimiwa kwa maelezo yake mazuri kuhusu umuhimu wa Muswada huu. Amesema Muswada umechelewa, ulipaswa kuanza mapema, tunakubali kabisa na hata Mheshimiwa Mramba na wachangiaji wengine wameeleza mchakato ulivyokwenda kwa miaka. Ametueleza umuhimu wa Mamlaka hii kwamba, itasaidia *economic integration* kwa maana ya kwamba, itaweza kuoanisha biashara ya ndani na ya nje. Vilevile ametoa angalizo kuhusu urari wa biashara, amesema nakisi inazidi sana na kwamba ni vizuri Mamlaka hii ikasaidia sana katika kushughulikia tatizo hilo la kupunguza nakisi hiyo katika urari wa biashara.

Mheshimiwa Zitto anasema ni vizuri chombo hiki kikawa ndiyo kinashughulikia mambo ya Sera ya Biashara. Alizungumzia kuhusu suala la *market intelligence,* suala la ufahamu wa masoko na kadhalika. Namshukuru sana kwa haya yote.

Mheshimiwa Mbunge, ameuliza hapa kwamba, kuna uwezekano tukawa labda tunakwenda kinyume na sheria kwa sababu suala hili ni la biashara ya kimataifa na biashara ya ndani kwa pamoja. Sasa mambo ya biashara ya ndani Zanzibar na Bara, yanashughulikiwa na Wizara mbalimbali. Tunakubali na kwa kweli tumelishughulikia; ni bahati mbaya labda Mheshimiwa Zitto hakupata *schedule of amendment* ambayo ilizungushwa asubuhi. Katika ile *schedule of amendment,* kwenye *clause two* pale tumesema kwamba, Muswada huu utahusika na mambo yote Tanzania Bara na Visiwani; na tukaongeza maneno pale *except for matters related to internal trade,* itakuwa ni mambo ya nje.

Vilevile ninamhakikishia Mheshimiwa Zitto kwamba, pamoja na sheria, lakini tumejitahidi sana kuwa na mawasiliano ya karibu kati ya Waziri mhusika wa Sheria upande wa Bara na yule wa Visiwani, kuhakikisha kwamba, Muswada huu utakuwa na tija kwa pande zote mbili za Muungano, achilia mbali yale ambayo yapo katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, maoni ya Mheshimiwa Zitto, yatazingatiwa sana na sina haja ya kujibu moja baada ya lingine, kwa sababu ni maoni mazuri na mengi ni ya utendaji. Tunamhakikishia kwamba, yatazingatiwa katika kuandika kanuni.

Mheshimiwa Zitto, pia ameulizia kuhusu uteuzi wa Bodi, nadhani ni sawa na alivyouliza Mheshimiwa Kaboyonga; kwamba, uteuzi wa Bodi uzingatie sheria. Kwanza, amepongeza kwamba Bodi hii imekaa vizuri, kwa maana ya kwamba, ipo kwenye sheria kabisa; inaelezea ni watu wa namna gani wawe katika Bodi. Amesisitiza kwamba ni vizuri Waziri azingatie katika uteuzi. Tunamhakikishia kwamba, hilo litafanyika na pale Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatumia kanuni kubadili Muundo wa Bodi ni baada ya kupata maoni hasa ya Kamati yetu ya Viwanda na Biashara, kuhakikisha kwamba maslahi ya nchi yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji mwingine ni Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum. Yeye ameupongeza Muswada huu na akasikitika kwamba, Uwanja wetu wa Sabasaba ni kama unafanya kazi mara moja tu kwa mwaka. Ameshauri kwamba ni vyema Mamlaka itakayoundea ijue namna nzuri ya kuutumia uwanja huu kwa ajili ya shughuli nyingine za kuleta tija. Tunapokea ushauri huu ni mzuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ameshauri kwamba, tufanye kazi na TAMISEMI kwa karibu; tunafanya hivyo ndio maana Maafisa Biashara wengine wapo pale Wizarani na wengine wapo katika Halmashauri zetu. Ninamuahidi kwamba, Mamlaka hii itaendelea kufanya hivyo.

Ametoa wazo zuri hapa kwamba, TANTRADE iwe na kanda za kufanyia kazi na TANTRADE ambayo ni Mamlaka hii, itoe mafunzo ili kujenga uwezo; ni mawazo mazuri ambayo tutayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lupembe pia amesema, Maafisa Biashara hawana kazi wapo tu kwa mfano walioko TAMISEMI. Mimi naomba hapa nitofautiane naye kwamba, Maafisa hawa wanajitahidi, tunachopaswa kufanya hapa ni kuwapa zana zaidi za kufanyia kazi na kutia msisitizo kwamba, Mamlaka itakapoundwa, ijaribu kuangalia zaidi, ikiwa ni pamoja kuwapa zana za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Lupembe, atakumbuka kwamba, tunapoongelea *decentralization by devolution*, maana yake siyo tu kupeleka fedha, lakini kupeleka hata wataalam katika ngazi ya Halmashauri, mojawapo ni hawa Maafisa Biashara. Kazi zao kubwa ni kuhimiza uanzishwaji na uendelezaji wa biashara katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yaani Mikoani na Wilayani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji mwingine ni Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza; ametoa mawazo mengi sana mazuri na hasa ametoa msisitizo kuhusu bidhaa za kilimo na bidhaa za mifugo. Amesema Mamlaka hii inayoundwa, iwe chachu ya kuonyesha kwamba bidhaa hizi za kilimo na mifugo, zinaunzwa nje kwa faida ya Mtanzania. Amesikitika tu kwamba, baadhi ya shughuli nyingine za biashara zinafanyika, bidhaa ya Tanzania inauzwa nje yule mtu anabadilisha fedha anakuja kununua kwa fedha ya Tanzania. Ameomba sana kwamba, Mamlaka hii inayokuja, ifanye kazi ya kulidhibiti hilo.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mntangi kwamba, mawazo haya yatazingatiwa, Mamlaka itakuwa makini. Natumia fursa hii, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Mheshimiwa Mntangi mwenyewe, tushirikiane katika hilo. Tutakuwa tayari kupokea mawazo, maoni na taarifa mbalimbali za kufanya basi hilo ambalo Mheshimiwa Mntangi anasema liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mntangi, vilevile amesisitiza umuhimu wa kutumia Balozi zetu katika kufanya kazi za Mamlaka hii zifanikiwe. Tunashukuru sana kwa ushauri huo tutauzingatia. Amesisitiza utoaji wa elimu ili bidhaa zinazoagizwa zisipotee, alipokuwa anazungumzia kwamba, mtu anaagiza bidhaa halafu kwa sababu labda ni mbovu au ni

feki inaharibiwa, kwa hiyo, fedha inapotea; elimu itolewe. Napenda kumuahidi kwamba, hilo tunalizingatia sana. Utakumbuka hata Muswada wa jana, wakati tunapitisha Muswada ule wa Viwango tulisema, *TBS* ile Mamlaka ya Viwango, isibaki tu kukamata bidhaa au kucheki, isipokuwa vile itoe mafunzo ili watu waanze kuagiza bidhaa nje ya Tanzania zikiwa nzima na nzuri, badala ya kungojea mpaka zifike hapa ziharibiwe. Katika hili, tunazishirikisha taasisi nyingine kama Mamlaka ya Chakula na Dawa, *TBS*, na *TANTRADE* hata *Fair Competition Commission (FCC)*, hii tume ya ushindani wa bei. Vilevile tunahakikisha kwamba, wote kwa pamoja wakishirikiana, basi wanamfanya Mtanzania ajue kwamba, bidhaa hii ninapoiagiza haijakiuka masharti yoyote ya uingizaji nchini na vile vile haitaharibiwa na kumletea hasara.

Amezunguza kwa uchungu sana kuhusu machungwa ya Muheza. Tunakuhakikishia Mheshimiwa Mntangi kwamba, tutashughulika tutahakikisha kwamba, Mamlaka hii inaangalia bidhaa kama machungwa na bidhaa nyingine Tanzania, ambazo ni kama hatuzitumii kwa maana ya kupata fedha za nje. Tutahakikisha kwamba, bidhaa hizi zinapewa kipaumbele ambacho kinastahili.

Amehimiza kutambuliwa kwa madalali ili kufanya bidhaa zetu zikienda nje kule zikubaliwe. Huu ni ushauri, tutauzingatia na sioni tatizo hapa; kutambua madalali ni mojawapo ya taratibu za kazi ambazo nafikiri zinaunganishwa kwenye kanuni za utendaji wa kazi wa Mamlaka hii.

Amezungumza vizuri sana kuhusu biashara ya ng’ombe, mbuzi, kupitia Bara au Zanzibar kwenda nchi jirani na kwamba, wananunua kwa fedha ya Kitanzania. Hili ni angalizo zuri Mheshimiwa Mntangi, tutaliangalia na sasa hivi tunakaribia kuandikiana Makubaliano na nchi ya Comoro katika hilo ili kuhakikisha kwamba, wale wafanyabiashara wakija wananunua kama watu wengine wanavyonunua bidhaa kwa fedha za kigeni. Umeonya sana Mheshimiwa Mntangi kuhusu mambo ya uchafu; dampo na gereji ambazo zinazunguka Uwanja wetu wa Maonesho ya Sabasaba. Tunakuhakikishia kwamba, Mamlaka itakapoundwa, itazingatia hilo kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine zimetolewa na Mheshimiwa Mramba. Mheshimiwa Mramba ni mzoefu katika sekta hii. Namshukuru sana, ametumia muda mwingi kujaribu kutueleza maeneo ambayo tunaweza tukajifunza namna gani ya kuboresha biashara, kwa kutoa mifano ya mikoa ambayo ana uzoefu nayo. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge tumesikia na Watanzania wamesikia tujaribu, siyo kila kitu cha Kitanzania ambacho labda kilikuwepo tangu mwanzo ni cha kutupa, bali vile vizuri tujaribu kuviiga tuviendeleze.

Ameshauri sana kwamba, tuwe na *trade centres* ambazo zitakuwa kila mahali Tanzania hii; ni sawa na Mheshimiwa Lupembe aliposema tuwe na kanda. Nafikiri ndio mawazo kama hayo ya Mheshimiwa Mramba kwamba, badala ya kuwa tuseme na Maonesho ya Sabasaba pale Dar es Salaam, tuwe na maeneo ya kanda ambako mambo haya yanafanyika. Niseme tu hapa kwamba, nia ya kuunganisha biashara ya ndani na biashara ya nje ni kufanya hili ambalo Mheshimiwa Mramba na Mheshimiwa Lupembe wamelima, liweze kufanikiwa kwa maana ya kwamba, sasa badala ya wale kujikita tu

kujaribu ku-*promote* biashara ya nje, basi wanakwenda na Tabora, Songea na kule Mara, kuhakikisha kwamba bidhaa za maeneo yale nazo zinakuwa *promoted* halafu zinapata masoko.

Jambo lingine kubwa ambalo amelisema na ambalo tunalipokea ni umuhimu wa Baraza la Ushauri au tunasema ni *Stakeholders Forum.* Hili ni wazo zuri na ninakubali kwamba, tuliliongea kwenye Kamati tukasema litaletwa tena hapa Bungeni kwa njia ambayo ameileta. Suala hili tutalileta kwenye sheria ili *forum* hii iwepo na itambuliwe kisheria. Forum hii kama tulivyosema ni ya ushauri, ambayo wanakaa pamoja wanaelezana hali halisi ya biashara, hali halisi ya upatikanaji wa biashara, hali halisi ya upatikanaji wa mazao, bei zilizoko duniani na kadhalika. Vilevile wana kazi kubwa ya kumshauri Waziri na kuishauri hata Mamlaka yenyewe, kuhusu hali halisi ya biashara katika nchi. Nafikiri ushauri wao utakuwa wa maana sana, ukizingatia kwamba, kanuni zitaelekeza kwamba, linapoundwa lishirikishe wadau kutoka maeneo mbalimbali.

Hapa ninao mfano, ambao Mheshimiwa Mramba ameniletea kwa maandishi, napenda niseme tutakwenda kuangalia baadaye. Wazo ni zuri, amesema kwamba, tuongeze katika Muswada huu sehemu inayosema *functions; to organize stakeholders' forum to address and advise the Authority and Government on general or specific trade matters for consideration.*

Mimi nafikiri haya ni mawazo mazuri, napenda kumuahidi Mheshimiwa Mramba kwamba, tutayazingatia wakati tunaweka mawazo haya katika Muswada huu, hiyo *forum* iweze kufanya kazi ya kuishauri Serikali na wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji mwingine ni Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni. Yeye amesisitiza elimu ya biashara na mambo ya semina ni muhimu sana tukayazingatia. Amesema miundombinu ya biashara, ndiyo inafanya labda hata biashara ya ndani isikue kwa kiwango ambacho tungependa. Napenda kumhakikishia kwamba, ndiyo maana tunaunda Mamlaka hii ili kuangalia na hilo ambalo limekuwa tatizo kubwa, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wametoa mifano. Mheshimiwa Zitto, ametoa mfano na Mheshimiwa Mramba naye ametoa mfano kwamba, kutokana na miundombinu ya biashara kutokuwa imara, basi unakuta bidhaa sehemu fulani bei yake ni ndogo sana na sehemu nyingine bei yake haishikiki.

Mheshimiwa Vuai ameshauri kuwa, mabenki yamjali Mtanzania wa kawaida; tunazingatia maoni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine aliyechangia ni Mheshimiwa Pindi Chana, ambaye kama alivyofanya jana, ametushauri kuhusu *interpretation of Local Government Authority Cap. 2287 and 288,* yeye anaona kwamba tuweke miaka au mwaka. Ukimuuliza mwanasheria mwingine, anasema hakuna haja, ukishaweka *Caps.* inaeleweka. Sisi hatuoni kama kuweka mwaka au kutokuwepo pale kuna mgogoro wowote; tutazingatia ushauri wake na tutashauriana na wanasheria na ikiwezekana, tutamtashirikisha na yeye, kwa sababu naona kuna utata; wanasheria wengine wanasema

hakuna haja ya kuweka tena, lakini yeye anaona kwamba tuweke. Hiki ni kitu ambacho hakibadilishi Muswada huu kwa namna yoyote.

Vilevile Mheshimiwa Pindi Chana, amezungumzia adhabu; amesema adhabu zile ambazo tumeziweka pale kwenye Sura ya 22 na 23, sura ndogo ya nne ni kubwa mno Mtanzania hawezi kulipa. Sasa Mheshimiwa Pindi Chana, naomba kwa heshima tu nikwambie kwamba, adhabu hii ni muafaka kwa sababu imezingatia sana madhara ambayo yatapatikana kama sheria hii itavunjwa na siyo uwezo wa kulipa. Kwa mfano, ukiangalia Sheria ile utaona kwamba ni mambo ya kutoa siri za biashara, pale ambapo hazitakiwi kutolewa. Nafahamu siri hizi zikitolewa zinaweza zikaleta madhara makubwa, kwa hiyo, tunapoweka pale mtu alipe milioni kumi ni kweli tunajua kwamba inaweza ikawa ni fedha nyingi, lakini ndiyo lengo la adhabu yenyewe kumfanya huyu mtu asifanye hilo kosa na kama kuna mwingine ambaye angependa kufanya hilo, basi aone kuna ugumu.

Mheshimiwa Mhagama, Mheshimiwa Mbunge wa Peramilo, amesema ana mengi mazuri sana. Amempongeza Mheshimiwa Rais, kwa kulitekeleza kwa vitendo lile ambalo aliahidi wakati anaunda Baraza la Mawaziri. Ameipongeza Wizara yetu na wadau wengine, amesema wakati sasa umefika wa Mamlaka hii kufanya kazi ya kumkomboa Mtanzania, kwa maana ya kukuza viwanda. Anarudia pale ambapo tulikuwa tunaongelea kuhusu *promotion,* kwa maana ya kuangalia uzalishaji, vilevile Mamlaka hii ijaribu kuwasaidia Watanzania ili waweze kuzalisha bidhaa bora, ambazo zitaweza kuuzwa. Ameongelea kuhusu kuongeza thamani ya bidhaa zetu na amesisitiza sana, umuhimu wa kujenga mahusiano na wenzetu wa nje, tuwaangalie tuhakikishie kwamba mahusiano hayo yanamfanya Mtanzania ananufaika na siyo kuwa ni mtu tu anayemlimia mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo hayo tumeyapokea, ameyasema kwa uzuri sana na tutayazingatia yote katika kuendeleza biashara hapa Tanzania.

Mheshimiwa Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, amesema maneno kama alivyosema mwenyewe machache, lakini mazito na yote yalikuwa ni ushauri. Mheshimiwa Kumchaya, ushauri wako tumeupokea, tutaufanyia kazi kuhakikisha kwamba, Mamlaka hii itakapoanza, kutaonekana mabadiliko kwa jinsi ambavyo Mtanzania anafanya biashara ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tu kusema kuwa, Wizara itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati ya Kumudu ya Bunge, Kambi ya Upinzani na michango ya Waheshimiwa Wabunge, hata kama kuna Mbunge labda kaandika wakati naondoka kuja hapa, kwa sababu kuna wengine kama wawili wameniandikia wakati nakuja hapa na sijaweza kujibu hapa, napenda kuwahakikishia kwamba tutawajibu kwa maandishi. Vilevile hapa nina ki-*note* kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Biashara na Viwanda, ambaye amesema nimemsahau Mwenyekiti wa Kamati.

Napenda kusema kwamba, Mheshimiwa Owenya naomba radhi kwa kutokutambua. Napenda nimtambue Mheshimiwa Lucy Owenya, japokuwa kwenye hoja

nimetaja kila wakati kama Mheshimiwa Owenya.  Kwa hiyo, itoshe tu kwamba kutokumtaja pale mwanzoni, tunasema ni *error of omission* anisamehe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba niseme kwamba, michango ya Waheshimiwa Wabunge wote tutaizingatia, hasa katika mambo yafuatayo:  Kwanza kabisa, kuwasaidia wajasiriamali na wenye viwanda vidogovidogo, kuhusu masuala ya biashara ya ndani na nje.

Kanuni za Muswada huu zitaelezea kwa kina, jinsi ambavyo taasisi hii inayoundwa itashirikiana nao na kufikia hatua ya kuuza bidhaa zao nje ya nchi.

La pili, ambalo tutahangaika nalo ni kujumuisha suala la ufuatiliaji wa maendeleo ya biashara na tafiti za masoko, kama jukumu mojawapo la taasisi hii.

Tatu, kuhakikisha Wajumbe wa Bodi wanakuwa na sifa zinazoendana na majukumu ya Mamlaka hii kuwa na mwakilishi kutoka viwanda vidogovidogo na kuzingatia jinsia.

Nne, kufanya uteuzi wa Watumishi wa Mamlaka kwa kufuata Taratibu na Kanuni za Ajira Serikalini na kuzingatia ushindani.

Tano, kuondoa suala la Mamlaka kupokea zawadi na hivyo kukwepa uwezekano wa kuwepo na upendeleo.

Sita, kushirikiana na taasisi na programu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutumia Maafisa Biashara Mikoani na Wilayani, kuhakikisha kuwa tunaimarisha biashara ya ndani katika ngazi zote Wilayani, Mikoani, Kikanda na hata Kimataifa.

Saba, kuhakikisha kuwa Mamlaka inayoanzishwa inatoa msukumo mkubwa wa kuendeleza maonesho ya kisekta kwa lengo la kuzipa sekta fursa ya kuonekana na kujitangaza zaidi badala ya kutegemea tu Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, yaani Sabasaba.

Maonesho haya ya kisekta ni elimu, uchapishaji, chakula na usindikaji bidhaa za sanaa za mikono, bidhaa za nguo, ngozi, usafirishaji na *logistic*.  Kadhalika, Maonesho ya Tamasha la Uhuru, yanayolenga kuwapa fursa wajasiriamali nchini kote kujitangaza, ambalo linafanyika kila mwaka litaimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Waheshimiwa Wabunge kuwa, kuimarisha biashara ya ndani itakuwa kichocheo kikubwa kwa biashara ya nje.  Hayo ndiyo maudhui ya Muswada huu, changamoto kubwa iliyo mbele yetu, baada ya Waheshimiwa Wabunge kuridhia Muswada huu ni kutayarisha Kanuni ambazo zitajibu na zitaelezea kwa mapana, hoja nyingi zilizojitokeza.  Tutajitahidi kukamilisha kanuni hizi mapema iwezekanavyo ili Mamlaka hii muhimu ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, ianze kazi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine, nikushukuru wewe binafsi, kwa kusimamia kikamilifu majadiliano ya Muswada huu. Nawashukuru Wafanyakazi wa Wizara, pamoja na *Board of External Trade,* kwa jinsi ambavyo wamefanya kazi vizuri na kuwezesha Muswada huu kujadiliwa katika Kamati na hapa Bungeni bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, umetoa hoja na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania wa Mwaka 2008 *(The Tanzania Trade Development Authority Bill, 2008)*

Ibara ya 1

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha kwanza, kwa maana ya *Part One - Preliminary Provisions* ndiyo hiyo.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Okay! Nakwenda *part one, three* kwenye *interpretation* tu.

**MWENYEKITI:** Hatujafika *three*.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mramba tafadhali.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri amekubali kimsingi, pendekezo lililokuwa kwenye Kamati ya Biashara na Viwanda,

ambalo nimelizungumzia hapa; labda niombe mwongozo wako; ningependa sasa ku-*introduce* kifungu kipya cha (r), yaani kifungu cha (5)(1) kiendelee mpaka (r) badala ya (o) katika ukurasa wa tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mramba hatujafika huko, tupo fungu la pili tu.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Fungu la pili pale, *Okay*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja marekebisho yake)*

Ibara ya 3

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha tatu – *interpretations*; nimeangalia hizi *interpretations* ukurasa wa kumi, *section* ya 19, sioni mahali ambapo pana-*define superannuation* fund ambayo inatumika katika *context* kwamba kutakuwa na michango ambayo itakwenda kwenye *superannuation fund;* sasa *superannuation fund* ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoelewa mimi, tupo ukurasa wa tatu, kama nilikuwa ninakufuata sawasawa; kwa mujibu wa hii niliyonayo mimi inasema: *"In this Act, unless* the *context otherwise requires, Authority means the Tanzania Trade Development Authority, established pursuant to section (4).* Sasa hilo la *superannuation*, sioni ambapo linajitokeza kwenye hii *section* ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyonga, hebu liweke vizuri swali lako.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza ufafanuzi; tupo kwenye *interpretation* kwa hiyo ni ukurasa wa tatu, *section three - interpretations*. Nilipozitazama *interpretations* zote kama zilivyo na kwa kuwa nimekwisha usoma huu Muswada kariby wote, nilipofika ukurasa wa kumi, section 19, kwenye *margins* kuna kitu kinasema *superannuation benefits; context* (b) inasema: *"Shall contribute to a superannuation fund.* Sasa swali langu ni kwamba; *what is superannuation fund,* kwenye *interpretation* haipo, sisi tumezoea ama ni *NSSF*, *PSPF* au *Local Government Pension Fund,* vitu kama hivyo?

**MWENYEKITI:** Natumaini umeshampata sasa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshampata.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo analosema Mheshimiwa Kaboyonga ni sahihi, kwa maana kwamba, yeye amezoea labda *NSSF* au *PPF* na kadhalika. Tunachosema hapa ni kwamba, Sheria inaweka wazi kwamba, Mamlaka hii itakuwa na mfumo vilevile wa kuwapa watu pensheni zao.

Sasa endapo kanuni itasema kwamba, Mamlaka iamue iende *NSSF* au *PPF;* hilo ni la kanuni hatuingilii katika sheria hii. Tunachoweka hapa ni kwamba, kutakuwepo na Mfuko kama huo; kama wewe ni Mfanyakazi wa Mamlaka ya Biashara Tanzania, utajua kwamba ukistaafu kila baada ya mwaka utapata malipo yako. Kitachoamuliwa sasa ni kwamba, Mamlaka itakapoundwa ndiyo wataamua wajiunge na Mfuko upi, wakiamua kwamba wanaunda namna yao nyingine ya kulipa pensheni, hilo litaangaliwa mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nasema kwamba, kwenye kifungu kile cha 5 ukurasa wa 4, kinaanza na (a), (b), (c) na kinaendelea mpaka ukurasa wa tano, ambapo pana *amendment* hiyo iliyosomwa sasa hivi na hiyo *amendment* ni (p) na (q) *among others*, yaani (b), (p) na (q).

Sasa mimi nataka hii *amendment* ninayoipendekeza na ambayo Waziri alikubali kuizingatia kwamba, iwe sasa ni (r), yaani waongeze tu iwe ni (r) na ihusu yale mambo niliyokuwa nimeyaeleza hapa ya kuwa na ile *Forum* ya Wafanyabiashara, ambao watakutana na kuishauri Mamlaka na Serikali yenyewe. Wao wanaweza wakaangalia ile *wording* kama kiingereza changu ni kibaya, waweke sawasawa lakini dhana ndiyo hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mramba, nakumbuka yale uliyoyaandika uliyompelekea Mheshimiwa Waziri naye akasema hapa kwamba, kwa ujumla wake anayaafiki, lakini tatizo letu ni kanuni. Kanuni ya 88(2) inasema kwamba, *"Mabadiliko yoyote yaliyopendekezwa kufanyika katika Muswada wa Sheria sharti yawekwe katika Jedwali la Mabadiliko litakaloandaliwa kwa ajili hiyo na kugawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge na katika kujadili na ama kuyapitisha au kutoyapitisha, vyovyote itakavyokuwa, mabadiliko hayo yatashughulikiwa kwa utaratibu huo."*

Tunazo kanuni zetu, kwa hiyo, inakuwa ni vigumu sana hapa, Bunge litakuwa halina hakika linapitisha kitu gani. Mheshimiwa Mramba.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa ruhusa yako labda niulize kwamba, sasa Waziri atakuja kuyaweka wapi; atajua mahali pake mwenyewe? Anihakikishie ataweka mahali fulani jambo hilo, ili sheria hii isipite kabla jambo hilo halijakuwepo na yeye alishakubali. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Mheshimiwa Mramba, atafuata maelekezo yako, Bunge lako likaridhia; sisi hatuna shida ya kuweka katika mlolongo kama alivyokuwa anashauri. Vilevile kama kutakuwa na matatizo, kwa sababu ni wazo zuri ambalo halina kipingamizi, ninamuahidi kwamba, litakuwa kwenye kanuni.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa kuwa taratibu hazikufuatwa, ibara hiyo ya tano inaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 15, naomba ufafanuzi *what is the maximum period* ambayo *accounts* hizi zitatakiwa ziwe tayari baada ya kufungwa? Kwa maana hiyo, ninaomba ufafanuzi kwenye vifungu vya 15 (2) na (3). Nikija kwenye kifungu cha 16 ndio hoja yangu ya kuomba ufafanuzi inakuwa nzito zaidi kwamba; kifungu cha 15(2) kinasema: *"Within six months of the close of each financial year, the Board of Directors shall cause the accounts including the balance sheet of the Authority to be audited by Controller and Auditor General."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofuata kinasema: *"As soon as the accounts of the Authority have been audited, and in any case, not later than six months after such audit, the Board of Directors shall submit to the Minister a copy of the audited accounts."* Kifungu cha 16 kinasema: *"The Board of Directors shall be …"*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyonga, hatujafika kifungu cha 16.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, akivisoma vyote kwa pamoja, ataona hoja yangu *essentialy* ni muda gani hapa unaotakiwa? *Is it within six months?* Ukizisoma zote hizi kwa pamoja, zinatufanya tuone kwamba itachukua takriban mwaka mzima toka *accounts* zinapokuwa *audited* mpaka kumfikia Waziri na huo ni muda mrefu sana kwa *accounts* zilizokuwa *audited* kuwa *meaningful.* Naomba ufafanuzi

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hii nakala yangu hapa, *section 15(2)* inasema: *"Within six months of the close of each financial year."* Ina maana kwamba, inawezekana baada ya miezi miwili hiyo kazi ikaisha, lakini isizidi miezi sita. Ukija kifungu cha 16 pale inasema kwamba: *"The Board of Directors shall, within six months of the close of the financial year."* Ina maana kwamba, Bodi inalazimishwa hapa kuhakikisha kwamba, mambo haya yote mawili yanafanyika ndani ya miezi sita.

Sasa watajipanga wenyewe; wakiweza kufanya labda ndani ya miezi miwili wakamalizana na *Controller and Auditor General* halafu miezi miwili iliyobaki wakapeleka kwa Waziri kwa ajili ya kuwa *approved,* hiyo ni sawa sawa, lakini yote mawili ni lazima yafanyike ndani ya miezi sita. Si kwamba, miezi sita iishe halafu ndio uiandike miezi sita hapana; ni ndani ya miezi sita mambo yote yawe yamekamilika na Bodi inapewa uhuru wa kuangalia *flexibility* katika hilo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati*

*ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania wa Mwaka 2008**
***(The Tanzania Trade Development Authority Bill, 2008)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Tanzania Trade Development Authority Bill, 2008,* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yote yaliyofanyika. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huo sasa ukubalike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wa Sheria wa Kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, umepitia hatua zake zote katika Bunge letu na hapa tulipofikia ndio mwisho wa shughuli hii.

Kwa kuwa *Order Paper* yetu ya leo inaonesha kabisa kwamba, tumekamilisha shughuli zote, basi tumefikia tamati ya shughuli zetu za Bunge kwa siku ya leo. Naomba kwa hali hiyo basi, niahirishe Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.06 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 30 Januari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*